

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

### BUNGE LA TANZANIA

### MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA PILI

Kikao cha Kwanza – Tarehe 26 Januari, 2016

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

### WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa)

### D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, Kikao cha Kwanza cha Mkutano wetu wa Pili ni leo, tunaendelea na utaratibu, sasa ninamwomba Katibu atuongoze.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:** Kiapo cha Uaminifu.

### KIAPO CHA UAMINIFU

Waheshimiwa Wabunge wafuatao waliapa kiapo cha uaminifu:-

Mhe. Dkt. Abdallah Saleh Possi  
Mhe. Deogratias Francis Ngalawa  
Mhe. Godbless Jonathan Lema  
Mhe. Goodluck Asaph Mlinga  
Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa  
Mhe. Omari Abdallah Kigoda  
Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango  
Mhe. Rashid Mohamed Chuachua  
Mhe. Shabani Omari Shekilindi

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Wabunge wote kuwapongeza Wabunge wapya ambao tumewaapisha katika siku hii ya leo, hongereni sana na karibuni mjengoni. Katibu!

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:** Hati za Kuwasilisha Mezani.

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU:**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu tarehe 4 Novemba, 2015 kama ifuatavyo:-

- (i) Toleo Na. 06 la Tarehe 06 Novemba, 2015;
- (ii) Toleo Na. 13 la Tarehe 13 Novemba, 2015;
- (iii) Toleo Na. 47 la Tarehe 20 Novemba, 2015;
- (iv) Toleo Na. 08 la Tarehe 27 Novemba, 2015;
- (v) Toleo Na. 46 la Tarehe 04 Desemba, 2015;
- (vi) Toleo Na. 50 la Tarehe 11 Desemba, 2015;
- (vii) Toleo Na. 51 la Tarehe 18 Desemba, 2015;
- (viii) Toleo Na. 52 la Tarehe 25 Desemba, 2015;
- (ix) Toleo Na. 01 la Tarehe 01 Januari, 2016; na
- (x) Toleo Na. 02 la Tarehe 08 Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Katibu.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:** Maswali.

#### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 1

#### **Tatizo la Njaa Wilaya ya Mpwapwa**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa wanakabiliwa na tatizo kubwa la njaa, na katika msimu wa mwaka 2014/2015 mvua hazikunyesha kabisa na kusababisha wananchi wengi kukosa chakula kutokana na ukame; na Serikali imekwisha tamka kwamba hakuna mwananchi atakayekufa kwa njaa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kugawa chakula cha njaa Wilaya ya Mpwapwa?

#### **NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU - (MHE. DKT. ABDALLAH S. POSSI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa hakuna mwananchi anayekufa kwa njaa kutokana na ukosefu wa chakula, Serikali imekuwa ikifanya tathmini ya hali ya chakula na lishe katika maeneo mbalimbali nchini na kutoa chakula cha msaada kwenye Halmashauri zilizoonekana kuwa na upungufu wa chakula ikiwemo Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Disemba, 2015 Serikali ilitoa chakula cha msaada tani 200 za mahindi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa. Aidha, kati ya tarehe 4 na 7 Januari, 2016

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Serikali imepeleka Wilayani Mpwapwa chakula cha msaada tani 1,619 na shilingi milioni 35 kwa ajili ya kununua mbegu za mtama na mihogo. Hivyo jumla ya chakula cha msaada kilichopelekwa Wilayani Mpwapwa mwezi Disemba, 2015 na Januari, 2016 ni tani 1,819.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoe chakula cha kupunguza makali ya bei ya soko tani 6,000 kwa Mkoa wa Dodoma kuitia wafanyabiashara wa Mkoa huo ili kuwezesha upatikanaji wa chakula chenye bei nafuu kwa wananchi wa Halmashauri zote za Mkoa wa Dodoma ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa wito kwa wananchi waliopo kwenye maeneo yenye ukame wakiwemo wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa kuhakikisha kuwa wanalima mazao yanayostahimili ukame na kufuata kanuni bora za kilimo ili kupunguza tatizo la upungufu wa chakula.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa George Malima Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwanza napenda niishukuru sana Serikali kwa kutupatia kiasi kidogo cha chakula katika Wilaya ya Mpwapwa.

Kwa kuwa, Wilaya ya Mpwapwa ina Majimbo mawili, Jimbo la Mpwapwa na Jimbo la Kibakwe, na kwa kuwa chakula hicho ambacho tumepatiwa ni kidogo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutuungezea chakula cha njaa Wilaya ya Mpwapwa?

Swali la pili, kwa kuwa hivi sasa baadhi ya wananchi wameacha kulima mashamba yao wanalima vibarua ili wapate hela ya kununua chakula. Je, utakubaliana na mimi kwamba iko haja sasa ulete chakula hicho haraka kwa Wilaya ya Mpwapwa na Wilaya ya Kongwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo muhimu kabisa. Ni ukweli kabisa Wilaya ya Mpwapwa na Kongwa hali ya chakula ni mbaya sana. (Kicheko)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU - (MHE. DKT. ABDALLAH S. POSSI):** Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa Mheshimiwa George Malima Lubeleje, kwamba Serikali inatambua jukumu lake la kuwalinda na kuwasaidia wananchi wote wanaopatwa na matatizo mbali mbali, ikiwemo baa la chakula.

Kuhusu swali lake la pili, tunafahamu umuhimu hiyo na tathmini itafanywa ili kuwezesha upatikanaji wa chakula hicho kwa haraka. (Makofi)

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Bura swali la nyongeza.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na njaa iliyowakumba wananchi wa Mpwapwa, Kongwa, Bahi, Chemba, Kondoa na maeneo mengine ya ukame katika Mkoa wa Dodoma, lakini mvua iliyonyesha na inayoendelea kunyesthesia imeleta mafuriko makubwa kwa baadhi ya vijiji na vyakula ambavyo wananchi walikuwa navyo vimesombwa na maji, mahitaji ya ndani, magodoro, vitanda, vyombo vimesombwa na maji.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Je, Serikali iko tayari kuwasaidia wananchi hao kwa kushirikiana na Wabunge? (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenister Mhagama.

### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU:**

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekumbwa na mabadiliko ya tabianchi na kusababisha majanga ya mafuriko katika maeneo tofauti katika nchi yetu ya Tanzania. Sisi wenyewe kama Serikali tumekuwa tukitembelea maeneo hayo nakuona madhara yaliyopatikana.

Mheshimiwa Spika, inawezekana tukaweza kufanyakazi ya kuwasaidia Watanzania kwa namna ile ambayo Serikali ina uwezo kwa sasa. Kwa hivyo, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, tutajitahidi kuendelea kufanya tathmini na kuona tunafanya nini kutoka eneo moja hadi jingine, lakini ninaziomba kamati za maafa kwenye ngazi ya Kata, ngazi ya Wilaya, ngazi ya Mkoa kuona yale yanayoweza kufanyika ndani ya uwezo wao, na yanayoshindikana wayalete Serikalini ili tuweze kushirikiana kwa pamoja. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante nakushukuru sana, nilikuona Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbewe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swalii.

Mheshimiwa Spika, hali ya ukame wa chakula katika nchi yetu, kimsingi inasababishwa na matatizo mawili makubwa. Tatizo la kwanza na matatizo yote mawili yanatokana na maji. Aidha, kunakuwa na ukame kwa maana ya kukosekana kwa maji, ama kunakuwa na mafuriko kwa maji kuwa ya ziada. Suluhisho la kudumu la tatizo la chakula katika maeneo mengi ya nchi, mbali na Serikali kuendelea kutoa misaada ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la muda mrefu ni kufanya water management kwa njia mbili.

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo yenyeye mafuriko kufanya *flood management* na kwenye maeneo yenyeye ukame wa maji kufanya *water conservation* yaani hifadhi ya maji hususani wakati wa mvua.

Mheshimiwa Spika, sasa swalii ni hili, kwa nini Serikali isiweke mpango maalum kuititia Halmashauri za Wilaya mbalimbali kwa kila Halmashauri kuwa na mpango wake wa kuangalia namna bora ya uhifadhi wa maji kwa wakati wa mafuriko, vilevile uhifadhi wa maji wakati wa msimu wa mvua ili yatumike kwa ajili ya unyweshaji maji. Vilevile utaratibu wa uzuaji wa mafuriko (*flood management*) wakati wa mafuriko ili tuepukane na hili tatizo la chakula kwa utaratibu wa kudumu zaidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Engineer Lwenge.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba nijibu swalii la Mheshimiwa Mbewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la kuvuna maji ya mvua tutaliletu kwenye awamu ya pili ya programu ya maji. Ni wazo la msingi kwamba ni lazima sasa tuelekee kuvuna maji ya mvua. Pia masuala ya kuweza kuzuia mafuriko ni jambo ambalo tutalifanya kwenye *program* ya pili. Kwa hiyo, tutaleta mpango huo ambao kila Halmashauri tutaangalia kwamba kila mwaka ikiwezekana wawe na mpango wa kuweza kujenga mabwawa madogo madogo ambayo yako chini ya uwezo wao. Wizara ya Maji itakwenda kusimamia na miradi mikubwa ya *strategic dams* hiyo itasimamiwa na Wizara ya maji.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**SPIKA:** Ahsante sana, tuendelee Waheshimiwa Wabunge na swali linalofuata la Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge wa Mlalo. Samahani kidogo Mheshimiwa Rashid, karatasi yangu ina shida kidogo. Tuanze na swali la Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mbunge wa Vwawa. Samahani Mheshimiwa Japhet.

Na. 2

### Tatizo la Ajira kwa Wahitimu

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza:-

Tatizo la ajira nchini kwa wahitimu wa vyuo vya kati na juu ni kubwa sana:-

(a) Je, ni wahitimu wangapi hawana kazi hadi sasa kutoka Vyuo vya Elimu ya Juu nchini?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ajira kwa wahitimu au kuwawezesha kujajiri hasa vijana?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU - (MHE. ANTONY P. MAVUNDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali namba mbili la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2014 vijana wahitimu wa elimu ya juu wasio na ajira wanakadiriwa kuwa 27,614 ambapo kati yao 14,271 ni wanawake na 13,343 ni wanaume. Hata hivyo, Serikali inaendelea na mikakati mbalimbali ya kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana wahitimu wa Elimu ya Juu kwa kuweka mazingira wezeshi ya kuajiriwa au kujari.

(b) Mheshimiwa Spika, jukumu kubwa la Serikali ni kusimamia Sera na Sheria mbalimbali ambazo zinaweka mazingira bora ya uwekezaji katika sekta zenyne uwezo mkubwa wa kuzalisha ajira ikiwemo kilimo na biashara), pia kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vidogo, vya kati na vikubwa ili viweze kuajiri sehemu kubwa ya nguvu kazi nchini na wengine kujajiri wenywewe.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo la ajira kwa wahitimu wa elimu ya juu, Serikali inatekeleza mipango ifuatayo:-

Kwanza, kuimarisha Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA) ambao una jukumu la kuwaunganisha watafuta kazi na waajiri wa ndani na nje ya nchi.

Pili, kuandaa Mkakati wa Kukuza Ujuzi Nchini ambao utaanza kutekelezwa mwaka ujao wa fedha wa 2016/2017, Mkakati huu umejikita zaidi katika kuwezesha mafunzo ya vitendo yatakayofanyika maeneo ya kazi ili wawe na ujuzi unaohitajika katika maeneo ya kazi.

Tatu, kuendelea kusimamia utekelezaji wa Program ya Taifa ya Kukuza Ajira kwa Vijana, ambayo imelenga kuwajengea uwezo vijana kwa njia ya mafunzo ya stadi za ujasiriamali, stadi za maisha na stadi za kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga swali la nyongeza.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Tatizo la ajira katika nchi yetu, na hasa kwa wahitimu wa Vyuo Vikuu limekuwa ni kubwa sana, kama kwa mwaka mmoja inaonyesha idadi hiyo bado hawana ajira.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuliambia Bunge hili ni lini hasa watakuja na mkakati wa kuanza kutoa labda mikopo midogo midogo ambayo itakuwa ni mitaji kwa hawa vijana ambao wanamaliza Vyuo vya Elimu ya Juu amba hawana kazi kwa muda mrefu?, hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa sasa inaonekana kwamba Serikali bado haina orodha kamili ya wahitimu wa Vyuo Vikuu amba hawana kazi.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kukubaliana na mimi kwamba umefika wakati sasa kuanza kuwa na data bank ya kujua wahitimu wote wa Vyuo vya Elimu ya Juu ili kuweza kujua ni ujuzi wa aina gani na weledi wa namna gani amba upo katika nchi hii, na kuweza kuwashauri waajiri mbalimbali na sehemu mbalimbali? Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hasunga, majibu ya swali hilo Mheshimiwa Mavunde, Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU - (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Spika, katika hoja ya kwanza ya mikopo midogo midogo Serikali inatambua ya kwamba asilimia kubwa ya wahitimu hawa amba wengi wangependa pia kufanya shughuli za kujajiri wanakabiliwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa programu ambayo itasaidia katika upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi waliohitimu elimu ya vyuo vikuu ambapo ziko fedha, ambazo zitatolewa kwa ajili ya wahitimu hao kupitia vikundi vyao na kampuni mbalimbali ambazo zitaundwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ipo Kampuni ya Wahitimu kutoka SUA ambayo inaitwa SUGECO, wenyewe walipatiwa fedha za mikopo na wanaendelea na shughuli za uzalishaji mali. Kwa hiyo, mipango hiyo ipo na itaendelea kuwepo.

Pili, katika suala la orodha kamili ya wahitimu, Serikali imekuwa ikifanya tafiti kila mwaka kuweza kubaini ni asilimia ngapi ya vijana amba hawana kazi waliohitimu Elimu ya Vyuo Vikuu na Elimu ya Juu. Ilianza kuanzia mwaka 2006 kutumia utafiti wa labour force survey ambayo ilifanyika mwaka 2006/2014. Utafiti huo unahitaji fedha, kila mara fedha inapopatikana utafiti huu umekuwa ukifanyika na huwa unafanyika kila baada ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kufanya utafiti kupata taarifa kamili ya vijana hao ambao wamehitimu elimu ya juu na hawana ajira ili tuone hatua stahiki za kuchukua.(Makofij)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na swali la TAMISEMI la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad Mbunge wa Viti Maalumu Shinyanga.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MHE. AZZA H. HAMAD** aliuliza:-

Mradi wa maji kisima kirefu katika Mji Mdogo wa Tinde umechukua muda mrefu sana kukamilika:-

Je, ni lini sasa mradi huo utakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kwa kutambua tatizo hilo la maji, Serikali katika mwaka fedha 2014/2015 ilitenga shilingi milioni 100 ambazo zilitumika kwa ajili ya kulipia gharama za uchimabaji wa kisima kirefu katika Mji wa Tinde, ujenzi wa vituo vinne vyta kuchotea maji na ujenzi wa nyumba ya pampu. Katika bajeti ya mwaka 2015/2016, Serikali imepeleka jumla ya shilingi milioni 200 ambazo zimepokelewa mwezi Novemba, 2015 na zitatumika kwa ajili ya ununuzi na ufugaji wa pampu na mfumo wa umeme wa jua pamoja na miundombinu yake yote. Kazi nyingine zinazofanyika ni ujenzi wa msingi wa kitako pamoja na ununuzi wa matenki ya kuhifadhi maji yenye ukubwa wa mita za ujazo 20, na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa mita 5,200. Aidha, kazi hii inafanywa na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Shinyanga na inatarajiwu kukamilika mwezi Aprili, 2016.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Azza Hillal.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa mradi huu wa kisima kirefu cha maji Mji Mdogo wa Tinde gharama yake halisi iliyotolewa na SHIWASA ilikuwa ni milioni 400 na mpaka sasa hivi Serikali imeshatoa milioni 300 kwa awamu.

Je, ni lini Serikali itakamilisha kutoa milioni 100 ili kukamilisha mradi huo?

Swali la pili, mradi huu wa maji, unategemewa kuhudumia zaidi ya watu 10,000 katika Mji mdogo wa Tinde. Vituo viliviyowekwa vyta kuchotea maji havitoshelezi kabisa ukilinganisha na idadi iliyopo.

Je, Serikali haioni kuna umuhimu mkubwa wa kuongeza vituo vyta kuchotea maji ili wananchi waweze kuchota maji hayo bila bugudha?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri - TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikiri kwamba katika Bunge lililopita hapa la Bajeti, kwa kumbukumbu zangu Mheshimiwa Azza alishika mshahara wa Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya tatizo la maji. Kwa hiyo, hapa ninakiri kwamba Mheshimiwa Azza amekuwa akipigania jambo hili kwa muda mrefu sana, hilo suala la kwanza.

Mheshimiwa Spika, suala zima la mradi huu bajeti yake ni shilingi milioni 400, lakini mpaka sasa tumepeleka milioni 300. Nadhani hata Mbunge atakiri hapa wazi kwamba upelekaji wa

## Nakala ya Mtando (Online Document)

milioni 100 za awamu ya kwanza, upelekaji wa milioni 200 ambao umefanyika mwezi Novemba, bado milioni 100. Suala hili nadhani kila Mbunge hapa atasimama na kusema mradi wake hapa haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa ni kwamba upelekaji wa fedha hivi sasa Serikali imejipanga, na ninyi wote ni mashahidi kwamba katika kipindi hiki mchakato wa kukusanya mapato ya Serikali umekuwa mkubwa sana lengo lake ni kwamba kuhakikisha viforo vya miradi vyote inatekelezeka ndani ya muda.

Mheshimiwa Spika, naomba nikuambie Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali imejipanga lengo kubwa ni kwamba *commitment* ya Serikali na Mheshimiwa Rais aliyoitoa kwa Tanzania kumwondoa ndoo kichwani mwanamama, hii ni ajenda kubwa tutaendelea kuifanya. Naomba uiamini Serikali yako itaenda kufanya mchakato mpana ili mradi huu ukamilike na wananchi wapate huduma.

Mheshimiwa Spika, swali lingine la pili, ni jinsi gani mradi ulikuwa na vituo vinne lakini *population* ni kubwa, naomba niseme kwamba Mamlaka ya Maji sasa iangalie ni jinsi gani ya kutatua kwa sababu *population* imeongezeka. Hali kadhalika, watu wa Tinde, hata huyu Mheshimiwa Mbunge alikuwa ana changamoto kubwa sana wakati wa kampeni, hali ilikuwa ni tete pale Tinde. Lakini ukija kuangalia sasa hata huo mradi ukikamilika ukiweka vituo vinne bado changamoto ya maji katika Mji wa Tinde kwa sababu ya *population* itakuwa ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ajenda kubwa hapa ni kama nilivyosema ni lazima kama Wabunge tushikamane tukusanye mapato ya Serikali ili mapato yale yasaidie hata ule mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka katika Mji wa Kahama pale, yanakuja Tinde yanaenda Nzega, yanaenda Igunga mpaka Tabora. Ni mkakati mpana kusaidia ukanda ule wote uondokane na tatizo la maji. Kwa hiyo, tumesikia hiki kilio Serikali itaifanya kazi. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Silinde nilikuona, swali la nyongeza fupi.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, asante sana. Tatizo la maji Tanzania ni kubwa na ndiyo maana kwenye Bunge letu kila Mbunge akiulizwa atakueleza hilo. Sera ya Maji ya Taifa inataka mwananchi wa kawaida apate maji umbali wa mita 400 toka makazi anayoishi. Sasa Mheshimiwa Waziri, na Naibu Waziri atueleze ni lini Sera hiyo ya Taifa itaanza kutekelezwa kikamilifu ili Watanzania waondokane na hii kero ya maji?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Maji, Engineer Gerson Lwenge.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Silinde kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Sera ya Maji ya mwaka 2002 tunasema kwamba umbali wa mtu kupata maji kwenye kichoteo ni mita 400. Kazi hii tulishaianza kuitekeleza kuanzia mwaka 2007 katika awamu ya kwanza ya programu ya maji ambayo imeishia Disemba, 2015.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya awamu ya kwanza ni mazuri ijapokuwa hatukufikia lengo ambalo tulitaka kufika, sasa ile miradi ambayo tayari imeshanza kwenye programu tunaiingiza kwenye programu ya pili ambayo inaanza Januari mwaka huu. Ili kukamilisha miradi ile iliyokwisha kuanza ili tuweze kufikia azma hiyo ambayo kila mwananchi atapata maji kutoka umbali wa mita 400.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie wakati wa kampeni Dkt. John Pombe Magufuli aliahidi adhima hiyo maeneo mengi na Serikali ya awamu ya tano itahakikisha kwamba suala la maji ni ajenda ya kwanza, na kuhakikisha kila mwananchi atapata maji, ijapokuwa tunasema asilimia 95 Mijini na asilimia 86 Vijiji, azma ya sasa ni kwamba tunataka tupate maji kwa asilimia 100 katika miaka mitano ijayo. (Makofii)

**SPIKA:** Asante sana kwa majibu hayo mazuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo.

Na. 4

### Hitaji la Maji Safi na Salama - Kata za Jimbo la Mlalo

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaharakisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wa Kata za Manolo, Shume, Sunga na Mbaru ili kuwaondolea usumbufu Wananchi wa maeneo hayo ikiwemo ushiriki hafifu kwenye shughuli za kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais- TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mlalo linakadiriwa kuwa na wakazi wapatao 196,258 kati yao ni asilimia 69 tu wanaopata huduma ya maji safi na salama. Aidha, kwa kutambua tatizo hilo, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ina mradi wa maji wa Shume, Madala na Manolo. Mradi huu unatarajiwu kugharimu jumla ya shilingi bilioni 2.96 hadi kukamilika ambapo kampuni ya Orange Contractor Ltd. kwa kushirikiana na Linda Technical Service Ltd. kutoka Mjini Lushoto na tayari mkatiba umesainiwa. Hata hivyo, kazi hii inasubiri upatikanaji wa rasilimali fedha. Mradi huu unatarajia kuhudumia wananchi wapatao 33,541 katika Kata hizo. Mradi huu utakuwa na urefu wa kilomita 55, vituo 70 vya kuchotea maji pamoja na matenki matatu ya kuhifadhia maji.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Mbaru, Halmashauri kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la CHAMAVITA liliufanya ukarabati mradi mkubwa wa maji wa Rwangi. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 CHAMAVITA ilitumia shilingi bilioni 96.0 kwa ajili ya kuboresha mradi huo kwa kupanua mfumo huo kutoka Kijiji cha Nkelei hadi Vijiji vya Mamboleo na Kalumele ambavyo viro Kata ya Mbaru. Wananchi wa Vijiji hivi wanapata maji kutoka kwenye tanki la maji kwa Kwekidevu lenye ujazo wa lita 22,500.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kata ya Sunga yenyewe Vijiji vitano vya Sunga, Kwemtindi, Masereka, Nkukai na Mambo inakadiriwa kuwa na wakazi wapatao 12,122. Huduma ya maji kwa Kijiji cha Mambo inapatikana kuitia visima vifupi viwili vyenye pampu ya mkono pamoja na vituo vinne vya kuchotea maji kutoka kwenye Mradi Mdogo na Mserereko ambaao hauna tanki la kuhifadhia maji. Mradi huu mdogo ulijengwa na Mwekezaji wa Mambo View Hotel kwa gharama ya shilingi milioni 5.0. Katika mwaka wa fedha 2012/2013. Kwa wastani Kata ya Sunga wananchi wanaopata huduma ya maji safi na salama ni asilimia 16 tu.

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Sunga, Kwemtindi, Masereka, Nkukai na Mambo katika Kata ya Sunga vitapewa kipaumbele mara tu baada ya vijiji kumi vya awamu ya kwanza ya programu ya maji kukamilika. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha huduma ya maji katika Jimbo la Mlalo na maeneo mengine nchini kadri rasilimali fedha zinavyopatikana.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri yenye kutia matumaini ya Naibu Waziri, naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Je, ni lini Serikali itakuja na mpango wa muda mfupi wa kuwapatia japo huduma ya visima virefu wakazi wa vijiji vya Maseleka, Madala na Tema wakati wanasubiri utekelezaji wa mradi huu mkubwa? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo fupi Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Selemani Jafo.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Shangazi nadhani ni Mbunge kijana na ni mara yake ya kwanza ameingia Bungeni lakini ameonesha ni wazi kwamba kuingia kwake moja kwa moja ameenda katika ajenda kubwa ya suala zima la matatizo ya wananchi kuhusu suala la maji.

Mheshimiwa Spika, kutopteka na ajenda hiyo naomba Serikali ichukue wazo hili, naomba tuangalie kwamba ni jinsi gani tutafanyakazi kwa pamoja ili wananchi wa Mlalo waweze kupata huduma hii ya maji. Naomba nichukue jambo hilo na naomba nimuahidi kwamba Ofisi yetu, Mheshimiwa Waziri wangu nadhani ataniruhusu nitafika kule Mlalo, licha ya ajenda ya maji nadhani ana changamoto nyingi kama Mbunge kijana lazima tumsaidie ili Jimbo lake liende vizuri.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa jibu hilo, tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, swali linaulizwa na Mheshimiwa Maryam Salum Msahaba, kwa niaba yake namwona Mheshimiwa Paresso.

Na. 5

### **Watoto Wanaoishi katika Mazingira Magumu**

**MHE. CECILIA D. PARESSO (k.n.y. MHE. MARYAM SALUM MSABAHA)** aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko la watoto wanaoishi katika mazingira magumu katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Dodoma, Mwanza na kadhalika. Watoto hawa wengi wao hawaendi shule na kazi yao ni kuomba omnia barabarani:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha watoto hao wanarudishwa shulen kusoma?

(b) Je, ni lini Serikali itawachukulia hatua wale wote wanaowatumia watoto hao kuombaomba?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dkt. Kigwangalla.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

## *Nakala ya Mtando (Online Document)*

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Mpango Kazi wa II wa Taifa wa huduma kwa watoto walio katika Mazingira hatarishi wa mwaka 2013/2017, ambao umeainishwa majukumu ya Serikali Kuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na wadau wengine.

Mnamo mwaka 2011, Wizara yetu ilifanya utafiti ili kubaini ukubwa wa tatizo la watoto wanaoishi na kufanyakazi mitaani, katika Mkoo wa Dar es Salaam ambapo watoto wapatao 5,600 walibainishwa. Baada ya utafiti huu uliandaliwa mradi wa majaribio wa namna ya kuwaondoa watoto hao mitaani kati ya mwaka 2011 hadi 2014 ambapo watoto wapatao 226 waliweza kuunganishwa na familia zao.

Mheshimiwa Spika, watoto 179 waliweza kurudishwa mashulen, watoto 196 walipatiwa huduma za afya na 1,000 walipatiwa unasihi. Aidha, mradi huu ulibainisha Mikoa tisa (9) ambayo inaongoza kwa kuleta watoto katika jiji la Dar es Salaam. Mikoa hii ni Pwani, Iringa, Lindi, Morogoro, Dodoma, Mwanza, Kilimanjaro, Tanga na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, baada ya utafiti, Wizara yetu iliandaa mpango kazi unaolenga kuzuia watoto kuingia mitaani, kuwarejesha na kuwaunganisha na familia zao na kufanya ufuatilaji.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuondoa ombaomba mijini wakiwemo wanaowatumia watoto kwa mfano, kwa Mkoo wa Dar es salaam mwezi Septemba, 2013 ombaomba 253 na watoto 135 walirejeshwa makwao kati ya watoto 33 walirejeshwa shuleni katika Mikoa walikotoka. Zoezi hili linaendelea katika mwaka huu wa fedha 2015/2016 ambapo watoto 47 wameunganishwa na familia zo na kati yao 35 wamerejeshwa shuleni.

Mheshimiwa Spika, suala la ombaomba ni mtambuka, linazihusisha mamlaka za Serikali Kuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Taasisi zisizo za Kiserikali, jamii na familia. Nachukua fursa hii kutoa wito kwa kila mdau kutekeleza wajibu wake katika suala hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Paresto swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika ahsante, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, Waziri amekiri hapa kwamba kati ya mwaka 2011/2014 waliandaa mpango wa majaribio wa kuwaondoa watoto hawa wanaoishi katika mazingira hatarishi, na suala la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi linaeleweka, na ni kubwa ndani ya nchi hii. Ni kwa nini Serikali hii ya CCM mnafanya mipango ya majaribio ambayo inatumia muda mrefu, fedha nyngi na yenye matokeo machache au matokeo kidogo?

Swali la pili, umekiri katika majibu yako kwamba meaandaa Mpango Kazi wa kuweza kuwaondoa watoto hao wanaoishi katika mazingira hatarishi. Ni kwa kiasi gani Mpango Kazi huu umekuwa shirkishi kwenye Serikali zetu za Mitaa kwa maana ya Halmashauri, ili na wao waziweke katika bajeti yao, ili kwa pamoja waweze kuona watoto hawo wanaondoka katika mazingira hatarishi? (Makofii)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Afya na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

## Nakala ya Mtando (Online Document)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Asante, nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii, na ninakushukuru Mheshimiwa Paresso kwa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kwamba ni kwa nini Serikali inaandaa mpango wa majaribio ni kwa sababu za kitaalamu. Hauwezi ku-embark kwenye mradi mkubwa utakaolihusisha Taifa zima kwenye Mpango Mkakati wa kuwaondoa watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu bila kufanya pilot study. Labda kiswahili tu kinaweza kikawa kinasumbua lakini kwa namna yoyote ile kwenye operational research na kwenye programming huwa tunaanza kwa kufanya pilot study ambayo ikifanikiwa tutakuwa tumejifunza changamoto zilizopo na baada ya hapo sasa tunaweza tuka scale up kwenye eneo kubwa zaidi. Kwa hiyo, kuanza na pilot study ni taratibu za kawaida tu kwenye programming.

Swali la pili, ni kwa namna gani mpango huu umekuwa shirikishi, majibu ni kwamba wakati unafanya pilot study jambo la kwanza ambalo unalolifanya ni kufanya table research. Ni kufanya utafiti wa mezani, unasoma tafiti mbalimbali, unaangalia nyaraka mbalimbali lakini baada ya hapo unatengeneza dodoso ambalo unawashirikisha wadau mbalimbali, na mwanzoni sasa unafanya formative assessment maana yake unawakusanya wadau, unawashirikisha kwenye utafiti wako wa awali ambao umeufanya kwa kutumia nyaraka mbalimbali na baada ya hapo sasa wale wadau waliopo watakupa, mawazo utajifunza changamoto kutoka kwao, utaziona fursa kutoka kwao, utaweza kupanga mbinu kwa pamoja na wao na kwa maana hiyo wanakuwa sehemu ya mradi husika.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. (Makofii)

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata. Waheshimiwa Wabunge wageni, naomba kwa wale wenye nia na wenyeji pia kwa wale wenye nia ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais, muendelee kutujazia zile fomu za kuomba kuchangia ziwe zinakuja kwenye meza yangu hapa kwa Makatibu ili tutengeneze orodha mapema, kwa sababu unavyozidi kuchelewa ndivyo ambavyo utachelewa pia kupangwa katika orodha ya wachangiaji na huenda ukakosa nafasi. Kwa hiyo, *the earlier, the better!*

Swali la Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini, Mheshimiwa Maftaha.

Na. 6

### Hitaji la Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA** aliuliza:-

Serikali kwa miaka mingi imekuwa na mpango wa kujenga Hospitali za Rufaa za Kanda; na tayari Kanda zote zina hospitali hizo isipokuwa Kanda ya Kusini tu:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanza kujenga hospitali hiyo ya Kanda ya Kusini ambapo tayari eneo la Mitengo Mikindani limetengwa kwa zaidi ya miaka saba na hakuna kinachoendelea?

(b) Je, ni Serikali haioni kama hawatendei haki wananchi wa maeneo ya Kanda ya Kusini kama wananchi wa maeneo mengine?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, Mheshimiwa Dkt. Kigwangallah.

## *Nakala ya Mtando (Online Document)*

### **NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini ningependa kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa Serikali kila Kanda inatakiwa kuwa na Hospitali ya Rufaa ya Kanda, katika Kanda saba zilizopo ni Kanda nne tu ambazo zina hospitali za Rufaa za Kanda.

Kwa Kanda ya Mashariki Serikali ilipandisha hadhi Hospitali ya Lugalo ya Jeshi kuwa Hospitali ya Rufaa ya Kanda. Kanda ya Ziwa kuna Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Bugando ambayo ilijengwa na taasisi ya hiari. Kanda ya Kaskazini kuna Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya KCMC inayomilikiwa na Taasisi ya hiari. Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuna Hospitali ya Rufaa ya Mbeya inayomilikiwa na Serikali. Kanda tatu ndizo bado hazijapata Hospitali za Rufaa za Kanda ambazo ikijumuisha kanda ya Kati yenye Mikoa ya Dodoma Singida ambapo ni Makao Mkuu ya Serikali. Kanda ya Magharibi ikijumuisha Mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi na Kanda ya Kusini yenye mikoa ya Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha A. Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali tayari ilikwishaanza ujenzi wa hospitali ya Kanda ya Kusini katika eneo la Mitengo Mikindani na hatua zifuatazo zimetekelawa na zinaendelea kutekelezwa kwa awamu. Maandalizi ya mpango kamambe yaani masterplan na michoro pamoja na makabrasha ya zabuni kwa ajili ya mradi yalikamilika tangu mwaka 2009. Awamu ya kwanza ya utekelezaji ilikuwa kujenga uzio kuzunguka eneo lote la hospitali na tayari ujenzi wake umekamilika. Awamu ya pili ilikuwa kujenga jengo la wagonjwa wa nje ambalo hadi Disemba, 2015 ujenzi wake ulikuwa umefikia asilimia 85. Serikali inatoa kipaumbele cha kipekee katika ujenzi wa hospitali hiyo na uongozi wa juu wa Wizara umekuwa ukitembelea na kukagua maendeleo yake mara kwa mara.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kuliari Bunge lako Tukufu kuwa si kweli kwamba Serikali haiwatendei haki wananchi wa maeneo ya Kanda ya Kusini na pia Serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo haibgui Kanda au eneo lolote. Vilevile usanifu wa hospitali hii ya Kanda ya Kusini ulizingatia mahitaji ya sasa katika hospitali ya ngazi ya Kanda. Hospitali hii itakapokamilika itakuwa ya kisasa zaidi ikilinganishwa na Hospitali za Kanda zilizopo, na itakuwa ni ya pili ya Kanda kujengwa na Serikali yetu. Ya kwanza ikiwa ni ile ya nyanda za Juu Kusini ya Mbeya.

Aidha, napenda kutumia fursa hii kuyapongeza mashirika ya dini na taasisi binafsi kwa kuunga mkono juhudhi za Serikali katika kuanzisha Hospitali za Rufaa za Kanda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Mtwara Mjini swali la nyongeza.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza;

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini ujenzi ule kimsingi umesimama na hakuna kinachoendelea pale Hospitali ya Mitengo.

(a) Je, ni lini sasa Serikali itaanza kuendeleza ule ujenzi wa Hospitali ya Kanda pale Mitengo?

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ujenzi wa hospitali hii bado umesimama na wananchi wa Kanda ya Kusini na hasa wale wa Mtwara Mjini wana changamoto za kupata matibabu bora ya tiba, lakini kimsingi kwamba Hospitali ya Ligula, hospitali ambayo ni Hospitali ya Mkoa hakuna x-ray, x-ray zimeharibika na ni muda mrefu hivi sasa wananchi wanahangaika kutembea umbali mrefu kwenda kufuata x-ray Mkoa wa Lindi na Dar es Salaam. Je, Serikali ipo tayari hivi sasa kuleta x-ray mpya ambazo zitaweza kutumika kwa ajili ya kuboresha tiba za wananchi wa Mtwara? (Makofij)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza, kwamba ujenzi umesimama siyo kweli, kwa sababu mara tu baada ya mimi kupewa heshima hii ya kuhudumu kwenye Wizara hii kama Naibu Waziri nilipoanza kazi tarehe 19 Disemba, 2015 nilifika mimi mwenyewe binafsi kwenye Hospitali hii ya Kanda ya Kusini kwenye eneo la Mikindani.

Nilifika na nilijionea mimi mwenyewe na nilifanya ziara ya kushtukiza kwa maana hiyo hakuna hata mtu mmoja Mkoani Mtwara ama Lindi aliyekuwa anafahamu kwamba siku hiyo kuna Naibu Waziri wa Afya angefika, na wala hata Mkuu wa Mkoa hata RMO hawakujua. Nilifika na nikapitiliza mpaka site na nilikuta kuna mafundi wapo site wanaendelea na ujenzi. Kwa maana hiyo siyo siasa tu na ndiyo maana tukisema hapa kazi tu, tunamaanisha tupo kazini. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, swal i la pili kuhusu x-ray nimpongeze Mheshimiwa Nachuma kwa jithada zake anazozifanya kufuatilia uwepo wa vifaa tiba, vifaa na vitendanishi kwenye hospitali hii. Alifika kwenye ofisi zetu akiulizia lakini pia Mbunge mwingine wa Nachingwea naye alifika mpaka ofisini kwangu na bahati nzuri alinikuta na tukazungumza, labda niseme tu kwamba kuna matatizo ya hapa na pale kwenye vifaa vya *imagine*, x-ray, *Ct-Scanner*, *MRI* na vitu vingine kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini tupo kazini tunayafanyia kazi, tunabuni mbini mbadala za namna ya kuziwezesha hospitali zote nchini kuwa na vifaa vya uhakika kuititia mipango mbalimbali na muda si mrefu mikakati yetu ikiiva nchi hii, matatizo ya *Ct scanner*, matatizo ya *MRI*, matatizo ya x-ray yatakuwa historia.

Mheshimiwa Spika, mtupe muda kidogo tu mkakati huu utakapo kamiliika Tanzania mpya mtaiona ikiwa imefika na mtaanza kufaidi matunda ya uwepo wa Serikali ya Awamu ya Tano ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (Makofij)

Na. 7

**Kukamilika kwa Ujenzi wa Barabara ya Sumbawanga  
Hadi Mpanda kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

## *Nakala ya Mtando (Online Document)*

Ujenzi wa barabara ya Sumbawanga hadi Mpanda bado haujakamilika.

Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utakamilika?

### **NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Anna Lupembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya kutoka Sumbawanga hadi Mpanda umegawanyika katika sehemu nne ambazo ni Sumbawanga – Kanazi km 75, Kanazi – Kizi – Kibaoni km 76.6, Kibaoni – Sitalike km 72 na Sitalike – Mpanda km 36.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya ujenzi wa sehemu ya Sumbawanga – Kanazi umefikia asilimia 68.6 na mpaka sasa km 43.47 za lami zimekamilika, maendeleo ya ujenzi wa sehemu ya Kanazi hadi Kibaoni kupitia Kizi ujenzi umekamilika kwa asilimia 50.3 na mpaka sasa km 23.43 za lami zimekamilika. Maendeleo ya ujenzi wa sehemu ya barabara ya Sitalike – Mpanda ni asilimia 76 na mpaka sasa km 20 za lami zimekamilika. Ujenzi wa sehemu hizo tatu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, upembizi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu iliyobaki ya Kibaoni hadi Sitalike ambayo ni km 7.2 umekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hii imetumia muda mrefu takribani miaka sita kutoka Sumbawanga mpaka Mpanda haijakamilika na wakandarasi wanaingia na kutoka mpaka hatima yake sasa hivi barabara ile imeharibika kupita kiasi na pale Mpanda Mjini kuna shimo ambalo mkandarasi alilichimba katikati ya Mkoa halieleweki lile shimo litazibikeje.

Je, Serikali ina mikakati gani kwa ajili barabara hii imekaa muda mrefu mno mpaka wananchi wa Katavi wamechoka, itakwisha?

Mheshimiwa Spika, swalii langu la pili sasa hivi Mkoa wa Katavi mawasiliano hayapo, barabara ya kutoka Mpanda kuelekea Tabora haipitiki kabisa na wananchi wa Katavi wanategemea kwenda kuchukua bidhaa zao Tabora, Mwanza, maisha ya Mpanda yamekuwa magumu kutohana na hali ya hewa jinsi ilivyo.

Je, Serikali ina mikakati gani ya dharura ili kuwaokoa wananchi wa Mkoa wa Katavi kwa ajili ya barabara hizo? (Makofii)

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu barabara hiyo kuchukua muda mrefu ni kweli baadhi ya barabara zimechukua muda mrefu lakini siku kumi zilizopita Serikali imetoa takribani shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kuwalipa Wakandarasi mbalimbali hapa nchini. Tunaamini sasa, nachukua fursa hii kuwaagiza Wakanarasi wote kama nilivyowaagiza wataalamu wetu wa TANROADS kwamba sasa hivi waanze kwenda kwenye site ili kazi hizo zianze mara moja. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili ni kweli kuna changamoto kubwa huko sehemu ya Katavi, Mkoa wa Katavi kwa sababu barabara zimekatika. Lakini wataalamu wetu wa TANROADS sasa tumewaelekeza huko ili waweze kuzikarabati barabara hizo. Pia sasa hivi tumefungua njia yetu

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

ya reli kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa huko baina ya Katavi, Tabora na Dodoma ili waweze kupata huduma kama kawaida, asante.

**SPIKA:** Asante kwa majibu Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, nimekuona Mheshimiwa Saddiq Murad, swali la nyongeza.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, barabara ya Sumbawanga, Mpanda inafanana na barabara ya Magole, Mvomero - Turiani ambayo nayo ipo katika mapango wa Serikali wa kuweka lami na kwa kuwa kilomita nane za mwanzo zilishawekwa lami baada ya kuteuliwa na kuchaguliwa kuwa Mbunge nimefuatilia na nimeambiwa fedha za kumalizia mradi huo zinatafutwa na kwa kuwa kipindi hiki mvua kubwa zimenesha barabara hiyo imeharibika.

Je, Serikali ipo tayari kufanya kazi ya dharura, huku tukisubiri fedha za lami?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara nydingi hapa nchini sasa zimeharibika kutokana na hali ya mvua inayoendelea kunyesha. Lakini TANROADS imetenga pesa maalum kwa ajili ya kufanya ukarabati kwenye barabara zote ambazo zimeharibika ili tuhakikishe wananchi wanaweza kupata mawasiliano kama kawaida.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda naomba tuende Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, swali linaulizwa na Mheshimiwa, Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile Mbunge wa Kigamboni.

Na. 8

### **Mikakati ya Kuondoa Migogoro ya Ardhi**

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE** aliuliza:-

Hapa Tanzania kumekuwepo na migogoro mbalimbali ya ardhi kati ya wawekezaji na wananchi, wakulima na wafugaji, hifadhi na wananchi na baina ya wananchi wenyewe:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kupanga matumizi bora na endelevu ya ardhi ili kuondokana na migogoro?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuondokana na tatizo la maendeleo ya miji kutokuendana na kasi ya ukuaji wa miji?

### **NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha kuandaa Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi wa mwaka 2013 mpaka 2033. Mpango huu ndiyo kiunzi wa matumizi ya ardhi yaani National Land Use Framework Plan unaotoa maelekezo ya namna ya kupanga maeneo yote nchini kuanzia katika ngazi ya Kanda, Mkoa, Wilaya na Vijiji. Mpango huu umeanza kutekelezwa kupita programu sita za kipaumbele ambazo ni makazi na miundombinu mikuu ya

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

uchumi, kilimo na mifungo, ardhi ya hifadhi na utalii, maeneo ya nishati na madini, mipango ya matumizi ya ardhi kwa ngazi za chini, pamoja na programu ya kuboresha Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Kupitia programu hizi, ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii itategwa na hivyo kuondokana na migogoro baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi. Aidha, Serikali imeandaa programu ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi nchi nzima ili kuondokana na migogoro ya ardhi.

(b) Mheshimiwa Spika, katika miaka ya hivi karibuni kumekuwepo na ongezeko kubwa la wakazi mijini ambako kumepelekea mamlaka za upangaji na uendelezaji miji kushindwa kutoa huduma za kijamii na kiuchumi kwa kiwango stahiki na hivyo kufanya miji yetu kukua kiholela. Katika kukabiliana na changamoto hizi, Wizara yangu imeendelea kuratibu uandaaji wa mipango kabambe ya Majiji na Miji mbalimbali nchini ambayo itatoa muongozo wa uendelezaji wa miji kwa kuzingatia mahitaji mbalimbali na hivyo kuondokana na tatizo la ukuaji wa miji isiyopangwa. Hadi sasa mipango kabambe ya Majiji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Miji ya Mtwara, Musoma, Iringa, Bariadi, Bagamoyo, Kibaha na Shinyanga iko katika hatua za mwisho za maandalizi na itakamilika kabla ya mwezi Agosti, 2016. Aidha, Mipango Kabambe ya Miji ya Tanga Singida, Tabora, Songea, Morogoro, Sumbawanga, Geita, Njombe na Mpanda ipo katika hatua mbalimbali za maandalizi.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa mamlaka za upangaji ambazo hazina mipango kabambe kutenga fedha katika bajeti zao ili kuharakisha uandaaji wa mipango kabambe na mipango ya kina itakayotoa mwongozo wa uendeleshaji katika miji yao na hivyo kuzuia tatizo la ukuaji wa miji isiyopagwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Kigamboni Dkt. Ndugulile swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipatia fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Moja ya chanzo cha migogoro ya ardhi hapa nchini unatokana na kwamba katika nchi yetu sasa hivi kuna umiliki wa asili ambao unatambulika kwa mujibu wa sheria kama customary right of occupancy na umiliki kwa kupitia hati ambao unajulikana kama granted right of occupancy. Changamoto imekuwa ni kwamba katika umiliki wa asili umekuwa haupewi uzito ule ambao unastahili je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba umiliki wa asili unatambuliwa, unalindwa na kuhakikisha kwamba wamiliki wa asili wanaweza kutumia hati zao zile kwa ajili ya shughuli za kiuchumi.

Swali la pili, ujenzi holela kwenye maeneo mengi hususani katika Jiji la Dar es Salaam limekuwa ni kero kubwa sana. Sasa na moja ya changamoto ni kwamba kumekuwa na hali ambayo watumishi wapimaji pamoja na watumishi Maafisa Ardhi kushiriki katika mikakati hiyo.

Je, Serikali ina mkakati gani na nakumbuka kwamba Mheshimiwa Waziri alishawahi kutoa kauli ya kuwawezesha baadhi ya Wenyeviti wa Serikali za Mitaa pamoja na Waheshimiwa Madiwani kusimamia shughuli ya Mipango Miji na kuwapa ramani ili waweze kusimamia maeneo ya umma na kuzuia uvamizi, je, utekelezaji wa jambo hili umefikia hatua gani?

**SPIKA:** Asante sana, majibu ya maswali hayo yaye kwa kifupi, Mheshimiwa Angelina Mabula Naibu Waziri Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi naomba majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza Mheshimiwa ameulizia swali la miliki za asili ili kuwawezesha wananchi wetu, Wizara yangu iko katika mpango kabambe ambao unaendelea katika Halmashauri zote za

## Nakala ya Mtando (Online Document)

kuwezesha upimaji katika maeneo ambayo yapo watu waweze kupimiwa na kumilikishwa kulingana na hali halisi katika maeneo wanayoishi. Aidha katika vipao mbele vyta upangaji wa miji pia, mpaka sasa Wizara yangu imeshapima Majji matano, Manispaa 15, Miji 15 na Miji midogo 79, yote hii ni katika kuhakikisha kwamba kunakua na mipango mizuri ambayo itaepusha ujenzi holela na ukuaji holela wa Miji yetu katika maeneo ya nchi hii.

**SPIKA:** Swali la nyongeza nimekuona Mheshimiwa Gekul Mbunge wa Babati Mjini, Mheshimiwa Ndugulile kuna nini?

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri hajajibu swali langu la msingi la pili, lakini vile vile hajajibu part B ya swali la pili.

**SPIKA:** Hebu lirudie.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nililiza kuhusiana na umiliki wa asili na mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba umiliki wa asili unalindwa, kuenziwa na kutumika kwa wananchi kwa ajili za maendeleo. Lakini la pili, ni kuwawezesha wananchi, Serikali ilitoa tamko kuitia Waziri kwamba Wenyeviti wa Serikali za Mitaa watawezeshwa na kupewa ramani ili waweze kusimamia maeneo yao na kuzuia uvamizi wa maeneo, hilo swali halikuweza kujibiwa.

**SPIKA:** Kutoa ramani kwa Wenyeviti wa Mitaa ili waweze kuwezesha.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nadhani katika kujibu nimeeleza pengine labda hakusikia vizuri, naomba niseme kwamba, suala la maeneo kulindwa kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alielekeza tayari katika Jiji la Dar es salaam kwa kuanzia Wenyeviti wote wale wa Mitaa watawezeshwa kupewa ramani za maeneo yao, ili waweze kila mmoja kulinda eneo lake, aweze kutambua wapi ni eneo la makazi, wapi ni eneo la wazi, wapi ambapo pamepangwa kwa ajili ya kujenga ili watu waepukane na kuvamia viwanja na kufanya ujenzi usio na utaratibu.

Mheshimiwa Spika, swali lake lingine aliongelea suala la umilikishaji wa asili kwa maana ya kupata zile hati za kimila, nadhani nimeliongelea kwamba Halmshauri zinaendelea katika utaratibu huo na ndiyo maana kumekuwa na msisitizo wa kuwa na zile masjala katika maeneo yao ili pale ambapo mwananchi anakuwa amepimiwa eneo lake na tayari Kijiji kinakuwa au Mtaa unakuwa na hati yake, basi waweke pia na eneo la kuhifadhi. Maana yake huwezi kuwa na Mmliki wa Asili na kutoa hati ambazo huna namna ya kuweza kuzihifadhi, maeneo yote wameelekezwa kuwa na masjala ambazo zitatunza na tunaimani kwamba hati hizi zinawapa uwezo wananchi kiuchumi kwa hiyo suala hilo Wizara inaitilia kipaumbele ni wajibu wa Halmashauri zote kuzingatia na kufuata utaratibu huo. (Makofii)

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu kumekuwa na migogoro katika nchi yetu baina ya wananchi na hifadhi, lakini tatizo hili limekuwa haliishi kwa Wizara hizi mbili ya Ardhi na Maliasili kukaa pamoja na kumaliza matatizo haya.

Nahitaji kufahamu kutoka kwa Serikali ni lini Wizara hizi mbili watacaa pamoja kumaliza migogoro ya Wananchi katika Vijiji ambavyo vinapakana na hifadhi mfano, Wananchi wangu wa Wilaya ya Babati na hifadhi ya Tarangire. (Makofii)

## *Nakala ya Mtando (Online Document)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Gekul ndiyo maana kwa makusudi kabisa tumekupanga kwenye Kamati ya Ardhi na Maliasili, sasa huko ndio mtapambana kabisa.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Gekul, Mbunge wa Babati na Mjumbe wa Kamati ya Ardhi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba iko migogoro inayosababishwa na mipaka kati ya Vijiji na Hifadhi za Misitu, Hifadhi za Wanyama na migogoro hiyo tunajua na ni kweli kwamba hata katika maeneo anayotoka Mheshimiwa Mbunge ya Tarangire na sehemu nyingine tuliona hiyo. Sasa tumekubaliana ndani ya Serikali katika awamu hii ni kuhakikisha kwamba aina hii ya migogoro yote tunaondoa, na ndiyo maana nimeandika barua kuwapeni Waheshimiwa Wabunge nafikiri mtapewa leo. Nimeomba kila Mbunge aniambie aina ya migogoro iliyopo katika maeneo yake. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, najua kama Serikali tuna utaratibu wetu wa kupata taarifa lakini nilitaka nipaye taarifa za pande mbili. Iko migogoro kati ya vijiji na vijiji, iko migogoro kati ya mipaka ya vijiji na vijiji na Wilaya, iko migogoro kati ya vijiji na Hifadhi za Misitu na wanyamapor na mengine, kwa maana hiyo tukipata hizo taarifa na zile tulizoagiza Mikoani sisi kama Serikali tutakaa pamoja.

Najua hapa tunahusika, Waziri mwenzangu wa Maliasili anahusika, Waziri wa TAMISEMI anahusika tutakaa pamoja na tutaunda timu na sisi tutakwenda pamoja kuhakikisha kwamba tunaondoa migogoro hii kwa manufaa ya Wananchi wetu. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante sana nawashukuru, Waheshimiwa kwa sababu ya muda na maswali bado ni mengi naomba tuvumiliane tuendelee na swali la Maliasili na Utalii nalo linaulizwa na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti. (Makofii)

Na. 9

### **Uharibifu Unaofanywa na Tembo kwa Wananchi Maeneo ya Serengeti**

**MHE. MARWA R. CHACHA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na uvamizi wa tembo kutoka Hifadhi ya Serengeti na kipelekeea vifo na uharibifu wa mashamba katika Wilaya ya Serengeti na maeneo jirani:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kunusuru maisha na mali za Watanzania waishio Serengeti?
- (b) Je, Serikali ina mpango wa kutathimini upya fidia inayotolewa kwani haiendani na uhalisia wa uharibifu wa mali na upotevu wa maisha ya watu?

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa spika, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu katika jukumu hili nililopewa, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu na kwa kweli

## Nakala ya Mtando (Online Document)

namrudishia sifa na utukufu. Lakini pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa uteuzi huu na kwa kweli natoa ahadi kwamba sitomwangusha. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kutokana na madhara yanayosababishwa na wanyamapori hususani Tembo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kunusuru maisha na mali za wananchi waishio kando ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Hatua hizo ni pamoja na zifuatazo:-

i. Kuunda timu ya udhibiti wa wanayamapori hatari na waharibifu ambayo inajumuisha watumishi kutoka kikosi dhidi ya ujangili cha Bunda, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Pori la Akiba Ikorongo, Halmashauri ya Wilaya na Mwekezaji Grumeti Reserves. Lengo ni kuhakikisha kwamba tukio lolote la uvamizi wa tembo linashugulikiwa kwa haraka iwezekanavyo.

ii. Kuweka minara au madungu (*observation towers*) ambayo hutumiwa na Askari Wanyamapori katika kufuatilia mwenendo wa tembo ili wanapotaka kutoka nje ya maeneo ya hifadhi hatua za kuwadhibiti zichukuliwe mapema, kama ilivyofanyika katika Kijiji cha Rwamchanga mpakani na Pori la Akiba la Ikorongo.

iii. Kutumia teknolojia ya mizinga ya nyuki ambayo huwekwa pembenzoni mwa mashamba na kufanya tembo wanapoingia katika mashamba yenyе mizinga kufukuzwa na nyuki.

iv. Kutoa elimu ya uhifadhi kwa jamii ili wananchi waepuke kulima kwenye shoroba za wanyamapori pamoja na umuhimu wa kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyeikiti, aidha, Serikali ina mpango unaoendelea wa kutumia ndege zisizokuwa na rubani (*UAV*) kwa ajili ya kufukuza tembo. Mafunzo kuhusu matumizi ya ndege hizo yanaendelea kutolewa kwa watumishi kwa kushirikiana na Taasisi ya World Animal Protection (WAP).

(b) Mheshimiwa Spika, kulingana na Kifungu cha 71 cha Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009, Waziri mwenye dhamana ya Maliasili amepewa mamlaka kuandaa kanuni za malipo ya kifuta jasho au machozi kwa wahanga wa wanyamapori hatari. Aidha, Kanuni ya 3 ya Kanuni za malipo ya kifuta jasho au machozi za mwaka 2011, inainishaa kuwa malipo hayo yatafanyika endapo mwananchi atajeruhiwa au kuuawa, ama kuharibiwa mazao au mifugo na wananyamapori. Malipo hayo huzingatia uwezo wa fedha na upatikanaji wa taarifa za kweli kutoka kwa wahanga.

Mheshimiwa Mwenyeikiti, aidha, Wizara itaendelea kurejea kanuni na viwango kadri hali ya maisha inavyobadilika. (Makofii)

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba kutokana na uhifadhi unaofanywa na wananchi wa Serengeti umesababisha tembo kuongezeka kwa wingi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa sensa ambayo imefanyika 2006, kulikua na tembo 3000 na kwa sensa ambayo imefanyika mwaka 2014 tembo wako 7000 na wengi wamehamia maeneo ya West – Serengeti sasa kwa kuwa tembo wameongezeka imekua sasa ni laana kwa wananchi wa Serengeti.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, swali, kwa vyote hivi ambavyo Waziri amesema ni ukweli hakuna hata kimoja ambacho kimetekelizwa. Sasa swali kwa Waziri, la kwanza; tungetamani Wanaserengeti kila Kata iwe na game post ambayo game post itakua na gari, itakua na Maaskari na silaha. Je, Wizara iko tayari kujenga game post kwa kila Kata, ziko Kata 10 zinazozunguka hifadhi, mko tayari kutujengea game post na kila game post na askari wake wanalinda mipaka ya Kata husika dhidi ya tembo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nimepitia Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sheria Na. 5 ya Mwaka 2009, kuna kifuta machozi hakuna fidia. Na kifuta machozi kama tembo ameua mtu ni shilingi 1,000,000/= na kama wewe umeua tembo ni 25,000,000/=. Swali, kati ya tembo na mtu nani wa thamani? (Makof)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Injinia Ramo Makani, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Serikali katika hatua ya kwanza kabisa inampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia jithada za Serikali katika uhifadhi. Takwimu za ongezeko la tembo ni faraja kwa Taifa hili kwa sababu kila mmoja wetu anafahamu faida za uwepo wa wanyamapori na faida za uhifadhi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la hatua zilizochukuliwa napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ni wiki mbili tu zilizopita nilikuwa Serengeti na haya niliyoyasema hapa sikuyaandika tu kutoka kwenye karatasi isipokuwa nimeshuhudia yakiwa yametekelizwa katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu swali lake la uanzishwaji wa game posts katika kila Kata hili ni wazo jema, unapotaka kuanzisha jambo ambalo ni jipya ni lazima kujipa fursa kwanza ya kufanya utafiti uliokamilika uweze kujiridhisha juu ya umuhimu na uwezekano na ukaangalia kila aina ya jambo ambalo ni la umuhimu kabla ya kutekeleza mpango wowote unaoufikiria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunalipokea, tutalifanya kazi na itakapoonekana kwamba ni jambo ambalo ni vema tukalitekeleza basi Serikali italicitekeleza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kifuta machozi kuwa kidogo, katika jibu langu la msingi nimeeleza pale mwishoni kwamba Serikali inatambua juu ya changamoto ya kwamba kifuta jasho au kifuta machozi vyote kwa pamoja hivi kila kila kimoja havitoshi, yeye ameangalia tu upande wa maisha lakini pia hata kwenye mali, mali zinazoharibiwa wakati mwingine ukiweka ulinganifu wa kiasi cha mali kilichopotea na kiwango kile kinacholipwa mara nyingi kinakuwa ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, lakini nimesema kwenye jibu la msingi kwamba Serikali inachukua hatua ya kupitia viwango hivyo na upitiaji wa Kanuni utakapoonekana kwamba, iko haja ya kuweza kufanya mabadiliko basi tunaweza kufanya mabidiliko hayo kwa mujibu wa sheria.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mhesimiwa Spika, kati ya tembo na mtu nani wa thamani? (Kicheko)

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Kati ya tembo na binadamu nani wa thamani! Okey, Waziri amesimama...

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**SPIKA:** Majibu ya nyongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Profesa!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kutoa majibu ya nyongeza baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, ningependa sana niwapongeze wananchi wa Serengeti kwa moyo wao na juhudhi zao katika kuhifadhi wanyamapori, ninaamini kabisa kama wananchi wa Serengeti wangkuwa hawahifadhi wanyama wale walioko pale ingekuwa vigumu sana kwa pori lile kuwa zuri na pori ambalo lina kiwango cha pili kwa ubora dunia nzima. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, watu ambaa wanaua tembo ni majangili siyo wananchi wa Serengeti na ndiyo maana watu ambaa wanawaua wale tembo kama wanaua kwa makusudi kama ambavyo inatokea mara kwa mara ndiyo maana wanachajiwa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini malipo haya hayalinganishi binadamu na wanyama. Lengo ni kuhakikisha kwamba watu wenye nia mbaya hawaui wanyama bila sababu, lakini pia ni kuhakikisha kwamba Serikali inashirikiana na wananchi katika kuomboleza matukio ambayo yanaweza kutokea kwa wanyama kuwaa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya swali fupi la nyongeza. Najua hata Rombo kuna wanyama lakini tuvumiliane muda ni mdogo.

**MHE. ESHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, wananchi ambaa wanazungukwa na hifadhi kwa Mkoa wa Mara, Tarime, Serengeti, Bunda Mjini na Bunda, wamekuwa wavumilivu sana. Hivi tunavyozungumza hakuna mwaka ambaa tembo hawatoki kwenye hifadhi na kuja kwenye vijiji, nazungumzia kwenye Jimbo langu, Kijiji cha Serengeti, Tamau, Kunzugu, Bukole, Mihale, Nyamatoke na maeneo mengine. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tulienda na Mheshimiwa Jenista, akajionea mwenyewe tembo wanavyoharibu mazao ya wananchi, lakini bado fidia ni ndogo, shilingi 100,000/= mtu anaandaa shamba kwa milioni 10. Hivi karibuni Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.....

(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wanazungumza)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Komeni basi, kelele niongee!

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jenista wamepeleka magari mawili na askari sita kuhakikisha yale mazao ya wananchi yanalingwa. Tunaposema ni lini Serikali mtatafuta ufumbuzi wa kudumu ili hao wananchi waepukane na njaa wakati wana uwezo wa kulima na lini ufumbuzi wa kudumu utapatikana badala ya kupeleka magari na askari kwa ajili tu ya kulinda mazao ambayo yako shambani?

**SPIKA:** Ahsante sana, majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Profesa wakati Wazanzibar wanaendelea kushangaa tembo wanavyoharibu mashamba huko. (Kicheko)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya ziada ya kujibu swali la Mheshimiwa Ester Bulaya kama ifuatavyo:-

## Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu alikuwa kule na alitoa ahadi, alijionea mwenyewe na kutoa ahadi kwamba Serikali itafanya juhudhi ya kupeleka magari na askari wa ziada ili kuahakikisha kwamba tembo hawaharibu mazao ya wananchi. Ni wiki moja na nusu sasa magari yale yako kule yanafanya kazi na tunaamini kabisa kwamba hii ni hatua ya kwanza ya Serikali kulishughulikia jambo hili kwa hatua za kudumu.

Mheshimiwa Spika, tumeanza pia kutumia ndege ambazo hazina rubani, tumeanza majaribio katika Wilaya ya Serengeti na Wilaya ya Bunda ili kuzitumia ndege hizi kuwatisha tembo na kuwaondoa katika maeneo ambayo wako karibu na mashamba ya watu na tunategemea kwamba jambo hili litatatuliwa kwa kudumu kwa kutumia utaratibu huo wa teknolojia.

**SPIKA:** Ahsante sana, tunafurahi kusikia kumbe tembo wameongezeka Serengeti kwa miaka mingi walikuwa wachache mno katika hifadhi hiyo. Tunaendelea Waheshimiwa wabunge na swali la Nishati na Madini la Mheshimiwa John Wegesa Heche Mbunge wa Tarime Vijiji. Mheshimiwa Heche!

Na. 10

### Fidia kwa Wananchi Waliopisha Upanuzi wa Mgodi wa Nyamongo

**MHE. JOHN W. HECHE** aliuliza:-

Tathmini ya Mgodi wa Nyamongo (ACACIA) kwa wakazi wa Vijiji vya Nyakunguru, Kewanja, Nyangoto, Matongo kupisha upanuzi wa uzalishaji wa mgodi ilifanyika kuanzia mwaka 2012 ambapo wananchi walizuiwa kuendeleza maeneo yao:-

(a) Je, Wananchi hao watapewa lini fidia kutokana na maeneo yao kulingana na bei ya sasa?

(b) Je, fidia hiyo itaendana na usumbuu na hasara waliyoipata hadi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Wegesa Heche, Mbunge wa Tarime Vijiji, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi hawajaanza kulipwa fidia, ukweli ni kwamba fidia imeanza kutolewa na imelipwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kijiji cha Nyakunguru, awamu namba 24, awamu namba 34 na awamu namba 35 kijiji hiki kina ukubwa wa hekta 35. Makadirio ya fidia ilikuwa shilingi bilioni mbili, lakini zilongezeka hadi kufikia bilioni ishirini na saba kutokana na ujenzi holela na upandaji wa mazao unaofanywa na baadhi ya wananchi wasio waaminifu wakati wa fidia ikifanyika maarufu inaitwa mtegesho.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, mgodi umeamua kuliacha eneo hilo na kutumia njia ya uchimbaji wa chini ya ardhi yaani *underground mining method*. Aidha, awamu namba 22 mheshimiwa spika, 23, 25, 28, 29, 33 na 44 yenye ukubwa wa eneo la hekta 90.4 ambao fidia yake ni shilingi bilioni 12 ililipwa kati ya mwaka 2012 na 2014.

## Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kijiji cha Kewanja, awamu namba 30. Ukubwa wa kijiji hiki ni hekta 8.10. Makadirio ya fidia yalikuwa shilingi milioni 250 lakini kwa sababu ile ile ya ujenzi holela na upandaji wa mazao unaofanywa na baadhi ya wananchi wasio waaminifu, fidia pia iliongezeka kutoka shilingi milioni 200 hadi kufikia shilingi bilioni 8.3. Mgodi umeamua kuliacha eneo hilo kwa sababu hauna fedha ya kuwalipa, aidha awamu namba 26, 27 na 31 jumla ya hekta 26.8 zilipwa fidia ya shilingi bilioni 8.8.

Mheshimiwa Spika, kijiji cha Nyangoto, awamu namba 20, namba 36, namba 37, namba 38, namba 40, 41, 42 na 44, kijiji hiki kina ukubwa wa eneo wa hekta 115.79, jumla ya fidia iliyolipwa kwa mgodi huu ilikuwa ni shilingi bilioni 41.14.

Mheshimiwa Spika, ieleweke pia katika awamu ya 20, jumla ya hundi 157 zenye thamani ya shilingi bilioni 3.7 bado hazijachukuliwa na wafidia, baada yao kusingizia kwamba pesa hiyo waliyolipwa ni kidogo mno.

Mheshimiwa Spika, kijiji cha Matongo, awamu namba 39, mgodi ulihitaji eneo kwa ajili ya kinga ya kiusalama tu amba ni Bufferzone ya mita hasa 200 wakati wa ulipuaji baruti kati ya eneo la mgodi na wananchi, lakini kwa sababu ya tegesha ile ile, mgodi uliamua sasa kuachana na eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, fidia husika hulipwa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhii Na. 4 na Sheria ya Ardhii ya Vijiji Na. 5 zote za mwaka 1999. Fidia hii ni kulingana na thamani ya kipindi ambacho tathmini ilifanyika, lakini pia fidia hizi zilizingatia usumbu na uharibifu wa mali za wadai husika. Aidha, wananchi wa maeneo hayo wanatakiwa kujua kwamba viwango vya fidia vinavyotolewa na mgodi wa North Mara ni vikubwa zaidi ya viwango vinavyowekwa na Serikali. Kutokana na ukweli huo, wananchi wote wanaotakiwa kuchukua fidia na kupisha shughuli za uchimbaji wanashauriwa sasa wachukue fidia ili kupisha shughuli za uchimbaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Heche natumaini umeridhika na majibu. Swali fupi la nyongeza.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka niseme nimesikitika sana kwa majibu yaliyotolewa na Serikali na nataka niwahakikishie Bunge lako kwamba wananchi wa Tarime hawatakubaliana na hali hii. Nataka niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mhesimiwa Spika, katika sehemu ya kwanza ya majibu yaliyotolewa na Serikali, maeneo yote yaliyotajwa hapo, yaliyofanyiwa tathmini na mgodi wa North Mara na wakati fulani hivi baada ya tathmini, mgodi ulikwenda mbele zaidi kufyeka mazao ya wananchi na Mheshimiwa Spika kwa mujibu wa sheria ya madini, wananchi wanatakiwa wakae umbali wa zaidi ya mita 200 kutoka eneo ambalo uchimbaji unafanyika.

Mheshimiwa Spika, wakati wote wananchi walipofanyiwa tathmini wamezuiliwa kuendeleza maeneo yao, mashamba yao yameharibika, nyumba zimebomoka na nyingi zimebomoka kutokana na *blasting* inayofanywa na mgodi lakini naambiwa hapa kwamba hawatalipwa wakati walifanyiwa tathmini.

Sasa swali langu ni hili, ni kwa nini mgodi ulifanyia tathmini nyumba, maeneo na mazao ya watu na kuzuia kuyaendeleza na sasa inasema kwamba haiwezi kulipa wakati ilifanyia tathmini yaani evaluation?

Swali la pili, haya majibu ya kukurupuka yasiyo na research, Serikali imesema kwamba wanalipa kwa mujibu wa viwango na North Mara inalipa fidia kubwa kweli kuliko ya Serikali, sasa mimi nina cheque hapa mbili za wananchi wa Tarime walilipwa na haya ni matusi!

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Nyamakaya Mbusiro amelipwa na Mgodi wa North Mara shilingi 3,871/= kama fidia ya shamba lake na nitawasilisha mezani kwako, cheque ya pili Chacha Muhabe Mwita amelipwa na Mgodi wa North Mara shilingi 7,273/= na ni nyingi mno, mashamba ya wananchi masikini. Nauli ya kutoka eneo la Nyamongo, Nyamwaga mpaka kufika Tarime Mjini ni shilingi 15,000/=.

Je, hii fidia ndiyo Serikali ya CCM inawaambia wananchi kwamba ni kubwa kuliko viwango ambavyo vinatakiwa kulipwa? (Makofisi)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Heche. Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Nishati na Madini Dkt. Merdad Kalemani. Waziri mwenyewe amesimama, Waziri wa Nishati na Madini Profesa Muhongo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, mambo ya fidia ya Nyamongo historia yake imeanza toka miaka ya 1980 na Mheshimiwa Mbunge atastaafu bado madeni yale yakiwepo. (Makofisi)

Mimi mwenyewe nimekaa na wenyiji pale, kuna kitu kinaitwa 'mtegesho' na mtegesho umefanywa hata na wafanyakazi wa Serikali.

Kuna mtu anakuwa na nyumba, anamkaribisha mtu, watu wamejenga nyumba za thamani hata ya milioni 200 wakitegea mgodi uwalipe. Nimefanya vikao wakati ule na wenyiji wa Tarime, wenyewe baadaye wakasema hawa wenyewe mitegesho ndiyo wanakuja kuharibu taratibu za hayo malipo.

Kwa hiyo, hayo mashamba na hiyo ni kwamba tathmini ilifanyika na niliitisha kikao nikiwa na DC na wenyiji wananchi wa pale, nikleta na wazee nikajaribu hata kuweka viongozi wa madhebu ya dini, Mheshimiwa Heche tumeongea naye nikasema baada ya Bunge suala la Nyamongo itabidi tuende tukae pale kama siku tano na itakuwa ya ukweli.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mheshimiwa Heche asiondoke tutaenda, hayo mashamba saa zingine ni mtu anatafuta kaeneo, anaweka mimea usiku, asubuhi anataka tathmini ndiyo maana inakuja shilingi 3,000/=.

Kwa hiyo, kutatua tatizo la Nyamongo, itabidi mimi, Mheshimiwa Heche, DC, wale wananchi na viongozi wenyewe twende eneo moja baada ya lingine. (Makofisi)

**SPIKA:** Ahsante sana, matatizo ya Nyamongo jamani Mheshimiwa Waziri amesema mtaenda huko mtayamaliza huko huko, kwa hiyo naomba tuwe na subira, baada ya ziara yenu ya huko sasa mtatueleza nini kinaendelea. Naomba tuendelee na wizara ya ulinzi na jeshi la kujenga taifa, swali la Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo.

Na. 11

### Utoaji wa Ajira kwa Wazanzibari Katika Vikosi vya Ulinzi

**MHE. MATTAR ALI SALUM** aliuliza:-

Kikosi cha Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) huandaa vijana kwa mafunzo mbalimbali kwa ajili ya kusubiri ajira katika vikosi vya ulinzi vya Muungano:-

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

(a) Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kutoa ajira kwa upande wa Tanzania Zanzibar?

(b) Je, ni asilimia ngapi ya vijana wanaoajiriwa kutoka upande wa Zanzibar?

(c) Je, kwa nini utoaji wa ajira katika Wizara hii kwa upande wa Zanzibar usijielekeze katika kwenye kikosi cha Jeshi la Kujenga Uchumu (JKU)?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali Salum. Majibu yake Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa Dkt. Hussein Mwinyi.

### **WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mattar Ali Salim Mbunge wa Shaurimoyo lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lina utaratibu wa kuandikisha Askari wapya kupitia Makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa. Jeshi la Kujenga Taifa hutoa nafasi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar nafasi hizo hutolewa kupitia Wizara inayoshughulikia Vikosi Maalum vyta Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Vijana hao husailiwa kwa utaratibu uliowekwa na wanaofaulu hupelekwa katika Makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa kufanya mafunzo sawia na vijana wa kutoka Bara.

(b) Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania halina utaratibu wa kuandikisha vijana kwa kufuata asilimia, bali ni vijana wanaokuwa na sifa zinazohitajika kuandikishwa bila kujali wanatoka upande gani wa Muungano.

(c) Mheshimiwa Spika, uandikishaji askari katika Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania haujielekezi moja kwa moja kupitia Jeshi la Kujenga Uchumi kwa sababu Kambi za JKU hazina utaratibu wa kuaweka vijana wao makambini kama inavyofanyika katika Kambi za Jeshi la Kujenga Taifa. Vijana hao huripoti asubuhi na kurejea majumbani kwao ifikapo jioni, hivyo kusababisha kwa kutokuwepo kwa muendelezo mzuri wa mafunzo na malezi ya vijana wakiwa kambini. Kwa mantiki hiyo vijana hao hawapati mafunzo yaliyokamilika ikilinganishwa na vijana wenzao wanaopata mafunzo katika Kambi za Jeshi la Kujenga Taifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali Salum swali la nyongeza.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafsi hii, kwanza nishukuru sana kwa kuwepo kwangu hapa leo.

Mheshimiwa Waziri hizi ajira kwa upande wa kule kwetu Zanzibar zimekuwa hali ngumu kweli upatikanaji wake na ili uipate basi ufanye kazi ya ziada kubwa sana. Je, ni kwa nini Wizara yako isikae na Wizara husika ya Zanzibar ajira hiyo ipitie sehemu ya JKU peke yake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Dkt. Hussein Mwinyi naomba majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu imeshakaa na Wizara inayoshughulikia vikosi vya SMZ na katika mazungumzo yetu tumewaeleza kwamba sisi tutatoa nafasi za kuijunga na JKT kupitia Wizara hiyo. Na ni hiari yao wao Wizara hiyo inayoshughulikia na vikosi kuamua endapo watawachukua vijana walioko JKU ili waje kuijunga na JKT au watazigawa kama wanavyozigawa sasa kupitia Wilaya na Mikoa.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, ninachosema ni kwamba kukaa tumeshakaa, uamuzi bado unabaki kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nataka nifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba, kuna idadi maalum isiyopungua vijana 300 kila mwaka, zinapelekwa kama nafasi za kujunga na JKT kutoka Zanzibar.

Kwa hiyo, vijana hao huwa wanapatikana kwa njia tofauti Wilayani na Mikoani na hatimaye wakishajiunga na JKT wakati wa usaili wa vyombo vyatia na Usalama vyote, Jeshi la Wananchi lakini pia Magereza, Uhamiaji, Polisi na kadhalika wanachukua vijana kutoka JKT na wale ambao wana sifa zinazotakiwa wanapata ajira katika vyombo hivyo.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Ally Saleh, swali fupi la nyongeza.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika ahsante, Mheshimiwa Waziri katika majibu yake alizungumza kwamba watu ni lazima watoke Zanzibar waingie katika Kambi za JKT ili waweze kuajiriwa, lakini nafikiri hilo ni tatizo.

(a) Je, Waziri anajua kwamba kuna suala kubwa la rushwa katika kupata ajira?

(b) Kuna wadowezi wanaotoka Maafisa wa Kijeshi walioko Zanziabar ambao wanatumia nafasi ambazo ziko *allocated* kwa Wazanzibari kuwapatia watu wao kutoka Tanzania Bara nafasi zile ambazo zimetengwa kwa Zanzibar?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa Mheshimiwa Hussein Mwinyi majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu suala la rushwa wakati wa usaili wa ajira, taarifa hizo mimi binafsi sijazipokea lakini namuomba Mheshimiwa Ally Saleh kama anao ushahidi wa kutosha wa kijana yeyote aliyeombwa rushwa, walete taarifa hizo na tutazifanya kazi kwa kuchukua hatua stahili kwa wale wote ambao wanajihuisha na vitendo hivyo. (*Makofii*)

Kuhusu swali la pili la nafasi za Zanzibar kuishia kupewa watu wa Bara pia naweza kusema kwamba mimi sina taarifa na utaratibu tuliuweka ni mzuri sana, kwa sababu tunapopata nafasi 300 za vijana wa Zanzibar kujunga na JKT, tunazikabidhi kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ni wajibu wao kuhakikisha kwamba nafasi hizo wanazigawa vile ambavyo wanapenda.

Mheshimiwa Spika, taarifa nilizonazo mimi, ni kwamba kwa utaratibu wa sasa nafasi hizo zinagawiwa kwa Wilaya na Mikoa.

Kwa hiyo, Kamati na Ulinzi za Usalama za Wilaya na Mikoa wanatakiwa wahakikishe kwamba wao ndio wateuzi wa vijana hao, inatokeaje mtu wa Bara anakuja anachukua nafasi zile kuwapa watu wa Bara wenzake, hilo nadhani siyo sahihi na kama ni sahihi basi udhaifu huo uko kwa wale wanakabidhiwa nafasi hizo.

**SPIKA:** Kiongozi wa Upinzani tafadhali, kifupi.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, majeshi yetu ni vyombo vyatia na Usalama, na ni vyombo ambavyo wote tunastahili kuviheshimu, lakini kwa muda sasa kumekuwa na utamaduni wa

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

kuwatumia askari kutoka Bara kuwapeleka Zanzibar, kuwaandikisha Zanzibar wakati wa uchaguzi na kuwatumia kupiga kura katika mazingira ambayo hayapo wazi.

Je, Mheshimiwa Waziri una taarifa za upelekaji wa vikosi Zanzibar kwa jukumu moja tu la kupiga kura na kisha kurejeshwa Bara? (Makofi)

**SPIKA:** Hili swali naona kama liko nje ya... (Kicheko)

**WABUNGE FULANI:** Aaaah! (Kicheko/Makofi)

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Waziri; una taarifa? (Kicheko)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwanza tutambue kwamba majeshi yetu ni ya Muungano. Kwa maana hiyo, Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania anaweza kupangiwa kufanya kazi yake sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu kuandikishwa kupiga kura, Mheshimiwa Mbewe nataka uelewe kwamba utaratibu wa kupiga kura Zanzibar unafahamika na uko wazi. Huwezi kwenda leo ukaandikishwa, ukapiga kura. Ili uweze kupiga kura, ni lazima uwe ni Mzanzibari mkaazi. Hiyo ipo na ushahidi tunao. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, ambacho tunaweza kusema hapa kwa ufupi ni kwamba wanajeshi wanapopelekwa Zanzibar ni kwa ajili ya kulinda usalama wakati wa uchaguzi. (Kicheko/Makofi)

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah! (Makofi)

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini.

Na. 12

### **Kurudisha Kituo cha Polisi Bonde la Mto Yayedha Chini**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Kutokana na wizi wa mifugo uliokithiri katika Bonde la Yayedha Chini, Serikali ilianzisha kituo cha polisi na sasa kimeondolewa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukirudisha kituo hicho ili wananchi wapate huduma za ulinzi wa mifugo na mali zao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kituo cha polisi cha Bonde la Mto Yayedha Chini kilianzishwa kutokana na matukio ya kukithiri kwa matukio ya wizi wa mifugo. Kufuatia hali hiyo, Jeshi la Polisi lilipeleka gari PT Na. 1008, Landrover kituo cha polisi cha Hydom kinachotoa huduma ya ulinzi wa eneo hilo na kuanzisha doria za mara kwa mara ili kupambana na wimbi la wizi wa mifugo. Kwa hivi sasa, hali ya wizi wa mifugo na uhalifu mwininge katika eneo hilo umepungua.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kituo hicho hakijaondolewa bali taratibu za kutoa huduma za ulinzi zimebadilika; ambapo askari hupangwa kwa kazi za ulinzi wa doria eneo hilo kwa kipindi maalum na kwa awamu. Jeshi la Polisi litaendelea kutathmini na kuzingatia hali ya uhalifu wa eneo hilo katika kutoa huduma stahiki za ulinzi na usalama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay nimekuona, swali la nyongeza!

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninaomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa uhalifu umeongezeka katika bonde la Yayed Chini, hasa ubakaji na mengineyo mengi; gari liliosemwa hapo kwanza ni bovu au chakavu katika eneo hilo la polisi au kituo cha polisi, Hydom. Lakini hiyo haitoshi hapo, mvua ikinyesha kidogo bonde la Yayed Chini halipitiki kutoka Haidom kwa gari lolote.

Je, Serikali haioni kwamba bado wananchi wa Yayed Chini wana haki ya kulindwa wao na mali zao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa wananchi wa Yayed Chini wanahitaji kulindwa: Je, tukiwhamasisha, Serikali iko tayari ku-*chip in* ili kujenga kituo hicho pamoja na wananchi? (Makofii)

**SPIKA:** Majibu mafupi ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Engineer Masauni!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, ni kwamba hatua zilizochukuliwa kwa kiasi fulani zimesaidia sana kupunguza tatizo la uhalifu, hasa wizi wa mifugo katika Bonde la Yayed Chini. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba jitihada hizo zinahitaji kuongezwa ili kuondosha kabisa masuala ya uhalifu, hasa wizi wa mifugo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, hii inadhihirisha kutokana na ukweli kwamba kwa mfano kwa takwimu za mwaka 2014/2015 katika Wilaya ya Mbulu ambayo imeonesha kwamba kuna matukio karibu 21 ya wizi wa mifugo, eneo la Yayed Chini lilikuwa na takwimu ya matukio matano ambayo ni makubwa zaidi ukilinganisha na maeneo mengine katika Wilaya hiyo. Hata hivyo, kwa mfano, katika Mkoa mzima wa Manyara, Wilaya ya Mbulu ndiyo iko chini ukilinganisha na Wilaya nyingine kama Kiteto ambayo inaongoza kwa matukio 71, ikifuatiwa na Babati yenye matukio 41 pamoja na Simanjiro 27 na Hanang 26. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kutokana na hayo basi, naomba nichukue fursa hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge akubaliane nami kwamba baada ya Bunge hili tukae pamoja ili kujiridhisha kwamba kama kuna haja ya kuchukua hatua zaidi. Hatua zaidi zitategemea mambo makubwa matatu; kwanza, siyo tu kwamba kutokana na wingi wa matukio ya uhalifu, lakini inategemea vilevile na idadi ya watu, inategemea hali ya kijirografia ya sehemu husika pamoja na upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo, tutakapokuwa tunafanya ziara pamoja na Mheshimiwa Mbunge, tutajua jinsi ya kufanya kulingana na upatikanaji wa fedha kadri utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili kwamba wananchi wa Jimbo lake na yeye mwenyewe wakishirikiana Serikali itachukua hatua gani? Mimi nataka nimpongeze sana kwa hatua zake hizo nzuri kwamba tunaamini kabisa kwamba Serikali ina ufinyu wa bajeti na hivi sasa vituo karibu kumi ambavyo viko katika hatua za ujenzi vimekwama kutokana na upungufu

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

wa fedha. Sasa ikiwa Mheshimiwa Mbunge atashirikiana na wananchi wake katika kuwahamasisha ili kuisaidia nguvu Serikali, basi tutamuunga mkono.

Mheshimiwa Spika, nataka niahidi tu kwamba Serikali itakuwa pamoja kushirikiana naye pamoja na wananchi wake kuhakikisha kwamba inasaidia kuimarisha ulinzi katika eneo hilo.

**SPIKA:** Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe!

Na. 13

### **Mikopo kwa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu Nchini**

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa mujibu wa Sheria, Wizara ya Fedha inatoa Mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu nchini Tanzania.

Je, ni utaratibu gani mzuri wa kuondoa usumbufu kwa wanafunzi kupata mikopo yao kwa wakati?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI** alijibuti:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utoaji wa mikopo na ruzuku kwa wananafunzi wa elimu ya juu nchini unazingatia Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Na. 9 ya mwaka 2004 kama ilivyorekebishwa, Kanuni za Utoaji Mikopo za mwaka 2008 na Mwongozo wa Utoaji Mikopo na Ruzuku kwa mwaka 2015/2016 ili kuweka vigezo, uwazi na urahisi katika utoaji wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, fedha za mikopo zinalipwa kwa wanafunzi kuitia vyuo wanavyosoma ili kuhakikisha kuwa fedha zinawafikia walengwa kwa wakati. Tangu kuanza kwa utaratibu wa kuwalipa wanafunzi fedha za mikopo kuitia vyuoni, malalamiko yamepungua kwa takriban miaka minne sasa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa mafanikio katika utekelezaji wa utaratibu huu, bado kuna changamoto katika ulipaji wa fedha hizo kwa wanafunzi kwa wakati kwa baadhi ya Vyuo Vikuu. Changamoto hizo husababishwa na ufinyu wa bajeti. Baadhi ya Vyuo Vikuu vyenye matawi kuwa na akaunti moja ya benki hali ambayo huchelewesha fedha kufika katika matawi; uongozi wa Chuo husika kutowapa wanafunzi taarifa ya kwenda kusaini kwa wakati ili walipwe mikopo yao; pamoja na baadhi ya wanafunzi kutosaini wakidhani wasiposaini hiyo mikopo hawatadaiwa watakapomaliza masomo yao.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na changamoto hizi, Serikali kuitia Wizara ya Fedha na Mipango, itaendelea kulipa kipaumbele suala la mikopo ya wanafunzi kwa Bodi ya Mikopo kupewa fedha kwa wakati. Serikali kuitia Bodi ya Mikopo, imeagiza Vyuo Vikuu vyote vyenye matawi kuhakikisha kuwa kila tawi linafungua akaunti ya benki ambayo fedha za wanafunzi wanaosoma katika matawi hayo zitaingizwa.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo pia imetoa Waraka wa kuagiza vyuo vyote kuhakikisha wanafunzi wanalipwa ndani ya siku saba baada ya kupokea fedha kutoka Bodi ya Mikopo, kwani fedha hizo siyo za kuwekeza, bali ni kwa ajili ya wanafunzi.

Aidha, Wizara yangu imeiagiza Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kufuatilia kwa karibu fedha zinazopelekwa Vyuni zinawafikia wanafunzi wa katii. Sambamba na hilo, ili kuratibu upatikanaji wa taarifa za wanafunzi kwa wakati, kila Chuo kimeelekezwa kuwa na dawati maalum la Mikopo pamoja na Afisa Mikopo mwenye uwezo wa kushughulikia changamoto mbalimbali za mikopo ya wanafunzi katika chuo husika.

**SPIKA:** Swali la nyongeza, Ndugu Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe!

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Baada ya majibu hayo, nitakuwa na swali moja tu la nyongeza

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko makubwa sana hasa kwa baadhi ya wanafunzi wenyewe familia masikini na wenyewe sifa za kupata mkopo huo, lakini wameshindwa kupata mikopo hiyo na kuendelea na masomo yao jambo ambalo linawadhoofisha wanafunzi wenyewe, lakini pia, linadhoofisha familia zao na Taifa kwa ujumla. Mheshimiwa Naibu Waziri anawaeleza nini wananchi kuhusiana na madai haya? (Makofi)

**SPIKA:** Jibu Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu madai hayo!

**NAIBU WAZIRI ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni kweli kabisa mikopo inayotolewa kwa sasa haiwezishi kuwapa wanafunzi wote wakiwemo watoto wa masikini. Hiyo ni kutokana na uhalisia kwamba nchi yetu inayo mahitaji mengi katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nachukue nafasi hii pia kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutambua tatizo hilo. Katika mwaka huu wa fedha tulikuwa na bajeti ya shilingi bilioni 306 tu, lakini baada ya kuingia kwake madarakani ameweza kuongeza shilingi 132, 299,067,500/= ambazo zimevezesha sasa kuwapa mikopo wanafunzi ambaao walikuwa wanaendelea na wale ambaao wanaanza mwaka wa kwanza. Mpaka sasa, jumla ya wanafunzi takribani 121,000 watafaidika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kwa kutumia nafasi yetu hii ambayo sisi ndio tunaopitisha bajeti, nawaomba wakati wa bajeti ukifika tulipe kipaumbele eneo hili. Ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kwa sababu ya muda. Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda!

Na. 14

### Utoaji wa Elimu Bure na Kuanzisha Chuo cha Veta Ndanda

**MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza:-

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha wanafunzi hawarudishwi shule kwa sababu ya michango ya mlinzi, madawati na chaki?

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

(b) Je, Serikali ina mpango wa kuanzisha Chuo cha Ufundi (VETA) kwenye Jimbo la Ndanda?

### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sera ya Elimu bila malipo, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi imetoa Waraka wa Elimu Na. 6 wa mwaka 2015 unaofafanua majukumu ya kila mdau katika utekelezaji wa elimu msingi bila malipo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa utoaji wa elimu msingi bila malipo ambapo jumla ya shilingi bilioni 15.71 zimepelekwa katika Shule za Msingi na Sekondari za Umma kwa mwezi Disemba, 2015. Fedha hizi ni kwa ajili ya ruzuku ya uendeshaji shule, fidia ya ada kwa shule za sekondari za bweni na Kutwa na chakula kwa wanafunzi wa bweni.

Mheshimiwa Spika, Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule wamepewa Mwongozo wa matumizi ya fedha hizo ambazo zitatumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, zikiwemo chaki, gharama za ulinzi, mitihani na chakula. Aidha, Serikali kuititia Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji itahakikisha inatenga fedha kila mwaka kwa ajili ya ununuzi wa madawati. Sambamba na hilo, wananchi na wadau wengine wa elimu wataendelea kusaidia kuchangia katika upatikanaji wa madawati kwa kadiri watakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba hakuna Mkuu wa Shule au Mwalimu Mkuu yeyote ambaye atamrudisha mwanafunzi nyumbani kwa kutolipa michango ya mlinzi, madawati na chaki kwa sababu, majukumu hayo ni ya Serikali. (Makofii)

Serikali ina dhamira ya kuendelea kuboresha utekelezaji wa mpango huu kadiri ya tafiti zitakavyoonesha, pamoja na maoni ya wadau mbalimbali yakiwemo ya ninyi Waheshimiwa Wabunge. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, nimekuona, Mbunge wa Ndanda.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, bado hajamaliza kujibu.

**SPIKA:** Ahaa, bado jibu! Ooh, Mheshimiwa Naibu Waziri, endelea.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi katika Wilaya zote zisizo na Vyuo vya Ufundi Stadi vya Serikali au visivyo vya Serikali. Wakati utafiti wa kubaini Wilaya zisizo na Chuo unafanyika, Wilaya ya Masasi ilikuwa na Vyuo viwili vya ufundi stadi kikiwemo Chuo cha Ufundi Stadi Ndanda, chenye uwezo wa kudahili wanafunzi 180 na Lupaso chenye uwezo wa kudahili wanafunzi 38, vinavyomilikiwa na madhehebu ya dini. Kwa kuzingatia kigezo hicho, Jimbo la Ndanda ambalo lipo katika Wilaya ya Masasi, haipo katika mpango huu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo katika kutekeleza azma hii ya kila Wilaya kuwa na Chuo cha Ufundi Stadi, Serikali imeviwezesha Vyuo 25 vya Maendeleo ya Wananchi vilivyopo katika Wilaya mbalimbali ili kutoa mafunzo ya ufundi stadi kikiwemo Chuo cha Maendeleo cha

## Nakala ya Mtando (Online Document)

Wananchi Masasi kwa kuwajengea uwezo Walimu, kuboresha miundombinu na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Utekelezaji wa utoaji wa mafunzo ya ufundi stadi katika chuo hicho ulianza mwaka 2012/2013. Napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Ndanda kutumia Vyuo hivyo vilivyopo Wilayani Masasi ili kupata mafunzo ya ufundi stadi. (Makofij)

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini ningependa kuuliza swali la nyongeza lenye sehemu (a) na (b).

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa tufahamu wazi kwamba Serikali sasa hivi imeamua kutoa elimu ya bure, lakini hata hivyo haikujipanga nayo. Nawea nikatoa ushahidi katika hili kwa sababu katika Jimbo la Ndanda kuna shule inaitwa Liloya, wamepelekewa pale shilingi 86,000/=. Hii ni shule yenye idadi ya wanafunzi 600, na hiyo ni sawasawa na shilingi 146/= kwa kila mwanafunzi kwa mwezi mmoja. (Makofij)

Je, Serikali haikuona kwamba jambo hili ingeliacha kwanza mpaka pale itakapokaa Bunge la Bajeti na kuitisha bajeti ambayo itakidhi mahitaji ya wakati badala ya kukurupuka kufanya jambo ambalo haijajipanganalo? (Makofij/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili la msingi niliuliza kwamba lini Serikali itakuwa tayari kupeleka ruzuku katika Chuo cha Ufundu Ndanda ili kiweze kudahili wanafunzi wengi zaidi kwa sababu kile ni Chuo kilicho bora kuliko vyuo vyote vya Serikali vinavyotoa elimu ya ufundi vilivyopo katika Mkoa wa Mtwara na Lindi? Naomba kuwasilisha maswali yangu. (Makofij)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundu; Mheshimiwa Stella Manyanya!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundu, naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge wa Ndanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haijakurupuka. Haijakurupuka kwa sababu Serikali hii ndiyo inayoishi na wananchi na kufahamu matatizo yao. Ndiyo inayofahamu hali halisi ya mazingira tuliyonayo na ndiyo maana ikajiwekea mpango kuititia llani yake ya Uchaguzi wa CCM kwamba itatoa elimu bure kuanzia Chekechea mpaka kidato cha nne. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo basi, kama ambavyo tumejionea katika mipango mingine tuliyokuwa tumeianza, ikiwemo na Mipango ya MMEM, Mipango ya MMES na mipango katika sekta nydingine, kila wakati tumekuwa tukianza na tunaboresha kadiri tunavyoendelea. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, kama ambavyo nimesema, kimsingi tunafahamu hata baadhi ya shule, tulipowaambia walete idadi ya wanafunzi pamoja na mahitaji kulingana na uhalisia, kuna wengine walileta sawa, kuna wengine hawakuleta vizuri. Pamoja na hayo, tumeshadhamiria kuona ni namna gani tunaendelea kufanya uchambuzi na kuboresha kadiri itakavyowezekana.

Hivyo tunasema kwamba katika majukumu yale yanayoishus Serikali kwa sababu elimu inaendeshwa kwa ubia baina ya Serikali na wananchi; wazazi kwa ujumla, kwa hali hiyo, katika yale majukumu yote ambayo tumejipangia, tutahakikisha Serikali inatimiza wajibu wake. Huo ndiyo msimamo wa Serikali yangu. Katika swali la pili...

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tundu Lissu swali fupi la nyongeza!

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**WABUNGE FULANI:** Aah, bado hajamaliza.

**SPIKA:** Bado!

**WABUNGE FULANI:** Eeee!

**SPIKA:** Eh, Mheshimiwa Naibu! (Kicheko)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Najibu swali la nyongeza la pili. Katika swali la nyongeza la pili la Mheshimiwa Cecil, kimsingi swali la mwanzo ulikuwa unahitaji ujenzi wa Chuo na sasa hivi umezungumzia juu ya utoaji wa ruzuku.

Kwa sasa hivi bado hatujafikiria kutoa ruzuku katika Chuo hicho ambacho kipo Ndanda. Hata hivyo, ni suala la kuangalia, kama kuna uwezekano na itaonekana lina faida kufanya hivyo, basi tutazidi kushauriana na kuona suala hilo linaweza likafanyika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kuhusiana na tatizo la Madawati. Mwaka 2015 tuliletewa taarifa na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kwamba kila Halmashauri ya Wilaya ya nchi hii imepelekewa madawati siyo chini ya 708 yaliyotokana na chenji ya rada iliyotoka Uingereza. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri yangu ya Wilaya ya Ikungi haijapata dawati hata moja. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri atueleze, madawati 708 ya Halmashauri ya Ikungi yalipelekwa wapi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, majibu! Mheshimiwa Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua upungufu wa madawati hasa zaidi kwenye Shule za Msingi na hata Sekondari. Serikali katika jithada hiyo, tulianza kuamua kama Taifa kuhakikisha kwamba tunaondokana na tatizo la watoto wetu kukaa chini. Pia tukapatu fursa inayotokana na fedha ya chenji ya rada ambayo Mheshimiwa amejaribu kuuliza na madawati yametengenezwa na baadhi ya Halmashauri nchini zimepata. Nakumbuka nina shule zangu kama mbili ikiwemo Shule ya Msingi Malolo, imepata.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Sasa kwa sababu Mheshimiwa ameitoa hii taarifa, tutajaribu kuangalia tupitie tuweze kuona kwa nini kama alikuwa yupo kwenye mgawanyo wa yale madawati katika Jimbo lake, hayakuweza kufika na yako wapi? Siyo rahisi kupata jibu la moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Serikali tunatambua hili na tumejipanga. Tunataka kuhakikisha kwamba ndani ya muda mchache sana ujao tunakuwa na madawati kwa nchi nzima. Nitakuja na Mpango na Maelezo, nitaomba Waheshimiwa Wabunge wote mniunge mkono. (Makofii/Kicheko)

**SPIKA:** Nilikuona Mbunge wa Vunjo, Mheshimiwa Mbatia.

## Nakala ya Mtando (Online Document)

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa dhana ya kuhakikisha Serikali inadhamini kutoa elimu ni jambo la msingi. Tatizo lililopo sasa ni miundombinu katika shule nyingi. Jimboni Vunjo tuna shule zaidi ya 16 ambapo nyingine hazina vyoo na matatizo makubwa kweli, ambapo ni janga hata zile shule kuendelea kufanya kazi sasa kwa sababu zinaweza ikasababisha majanga makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiweka utaratibu ukaifuata inakuwa ni jambo jema. Serikali haioni umuhimu wa kuleta *mini budget* ili Bunge liweze kutekeleza wajibu wake ili fedha hizo ziumike kwa utaratibu ambao tumejiwekea Kikatiba badala ya Serikali tu kusema inaagiza, inapeleka huku, inapeleka huku, kwa utaratibu ambao haueleweki na unaoleta utata? (Makofii)

**SPIKA:** Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa George Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa najaribu ku-pause wazo zuri, kubwa na lenye mtazamo mpana. Hata hivyo Serikali imeanza kutekeleza mpango ule wa kuhakikisha kwamba tunatoa elimu ambayo hailazimishi wazazi na hasa maskini kutoa mchango ndipo mtoto aende shule. Hili kusema ukweli ukilitafsiri kijuu juu utorialiona ni jepesi, lakini unapomzungumzia maskini, Serikali hii ya awamu ya tano imeanza kujaribu.

Mheshimiwa Spika, tumejaribu kuji-confine kwenye bajeti ya mwaka 2015/2016, maana kwenye bajeti hiyo kuna fedha iliyotengwa na Bunge, lakini kuna ile fedha iliyopatikana. Sasa tumejaribu kucheza kwenye ile *difference*. Mheshimiwa Rais akasema, basi tuanze kutoa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shule inayoitwa *capitation*, itolewe *in full amount* kama ilivyokuwa imepitishwa siku za nyuma shilingi 10,000/= ambapo shilingi 6,000/= itaenda kwa ajili ya kila mtoto shulenii na shilingi 4,000/= itawekwa pamoja kwenye Wizara na kununua vitabu na kuwagawia, kupeleka kwenye mashule. Tumeondoa ile ya kununua vitabu kila mtu anakotaka.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali imefidia ada ambapo kwa Shule za Kutwa ni shilingi 20,000/=. Ilikuwa ni lazima kila mtoto, mzazi achangie; imefuta! Pia shilingi 70,000/= kwa watoto wa bweni, Serikali imefuta, imechukua huo mzigo. Pia tutapeleka fedha ya chakula shilingi 1,500/= kwa kila mtoto wa shule za bweni na Shule Maalumu za Msingi. Hizi zote kusema ukweli zilikuwa haziendi vizuri, sasa tunazipeleka kabla ya mwezi. (Makofii)

Vilevile tutapeleka fidia ya mitihani. Mtakumbuka, kila mtoto hasa wa sekondari kidato cha nne alikuwa analipia Sh. 50,000/= kwa ajili ya mitihani. Hizi Serikali itazilipa yenewe kwenye Baraza la Mitihani. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Serikali hii imejipanga kutumia shilingi bilioni 18.77 kwa kila mwezi. Kwa hiyo, nikijibu na swali la rafiki yangu pale ni kwamba fedha hii ni kila mwezi. Hivi sasa tunajandaa kupeleka nyingine.

Mheshimiwa Spika, kumejitokeza tu changamoto ya idadi ya wanafunzi na records zilizokuja, ndio maana fedha zimeenda vibaya, lakini uzoefu tuliuopata kwa mwezi huu, sasa naamini mwezi unaokuja tunaweza tukarekebisha hayo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nakubaliana suala la miundombinu kwamba ni changamoto, lakini tumeeleza wajibu wa Serikali, lakini tukaeleza pia wajibu wa wadau wa maendeleo na wazazi katika masuala mazima ya kuhakikisha kwamba Taifa letu linatoa elimu iliyo bora na ambayo ni nzuri na ya kueza kufanya Jamii yetu iweze kubadilika na ku-meet viwango vinavyotakiwa. Ahsante sana.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo Waheshimiwa Wabunge, litaulizwa na mama yetu, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo.

Na.15

### **Kuanzisha Mradi wa Maji Mto Ugalla Kwenda Urambo**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Urambo imebahatika kuwa na Mto Ugalla unaopita Kusini kwake kuelekea Mto Malagarasi ukiwa na maji ya kutosha.

Je, kwa nini Serikali isianzishe mradi wa kuvuta maji ya Mto Ugalla kupeleka Mji wa Urambo ambaa unakuwa kwa haraka na wananchi wake wamekuwa wakikabiliwa na uhaba mkubwa wa maji kwa muda mrefu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hili kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mji wa Urambo unakuwa kwa haraka na wananchi wake wanakabiliwa na uhaba wa maji kwa muda mrefu. Katika kutatua tatizo la maji kwa Mji wa Urambo, Serikali imepanga kuupatia Mji huu maji kutoka chanzo cha Mto Ugalla.

Katika kutekeleza azma hii ya kutoa maji kutoka Mto Ugalla, Serikali imeendelea na upembizi yakinifu ili kutathimini wingi wa maji na pia ili kupata muafaka na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kuhusiana na kutekeleza Mradi ndani ya Hifadhi ya Ugalla.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali imepanga kuanzisha mradi mwengine wa kutoa maji Mto Malagarasi kwa ajili ya kuleta maji Mji ya Urambo, Kaliua, Mji mdogo wa Nguruka, baadhi ya vijiji vilivypo Wilayani Uvinza na maeneo mengine ya Wilaya ya Uyui, Manispaa ya Tabora na vijiji vitakavyokuwa umbali wa kilomita 12 kando kando ya bomba kuu. Mradi huu utasaidia kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wakazi wengi zaidi kwa kuwa Mto Malagarasi una maji mengi yanayotiririka wakati wote wa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Mhandisi Mshauri anaendelea na kazi ya upembizi yakinifu, usanifu wa kina, pamoja na uandaaji wa makabrasha ya zabuni. Kazi hii ilianza mwezi Julai, 2015 na inategemewa kukamilika mwezi Februari, 2016. Aidha, katika mwaka huu wa fedha 2015/2016, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kazi ya usanifu wa mradi mkubwa na utekelezaji wa mradi mkubwa na utekelezaji wa miradi ya muda mfupi ya kuboresha huduma ya maji katika Mji ya Urambo na Kaliua.

**SPIKA:** Ahsante sana Engineer Kamwelwe, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Mama Sitta!

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu aliyoyatoa, pamoja na majibu mazuri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:

Kwanza nakubaliana kabisa na Serikali kwamba jawabu la haraka la matatizo ya Urambo kuhusu maji ni Mto Ugalla, kwa sababu ni kilomita 30 tu kutoka Usoke. Ninaamini kwamba tumefanya hivyo kwa sababu ya suala la quick win ili wananchi wapate maji haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza, katika kipindi tulichopita, katika maandalizi ya kupata maji kutoka Ugalla liliuja tatizo la mazingira kwamba kuna wanyama, sijui kuna misitu; naomba Serikali itoe kauli, tusije tukafika katikati wakaanza tena masuala ya wanyama na misitu wakati sisi tunapata shida ya maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni vizuri kweli miradi miwili hii ikaenda pamoja kwa sababu kwanza Mto Malagarasi unategemea hayo maji kutoka Ugalla ambayo ndiyo yanatoka Urambo. Kwa hiyo, nashukuru Serikali hivyo, lakini je, Waziri yuko tayari kwenda na mimi uko akajionee mwenyewe uharaka wa kupata maji katika Mji wa Urambo na Usoke? Lini twende naye tufuatane wote wawili? (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Waheshimiwa Wabunge, mkitaka kufuatana mpaka ruhusa ya Spika eeh! (Makofi/Kicheko)

Majibu tafadhal! (Kicheko)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Sera ya Maji ya mwaka 2002 inaendelea kutekeleza Mpango wa Sekta ya Maji nchi nzima ili kuhakikisha ifikapo mwaka 2020 zaidi ya asilimia 85 ya wananchi wanaoishi vijiji wanapata maji safi na salama. Kama alivyoongea Mheshimiwa Waziri, ni kwamba tunataraja ifikapo mwaka 2025 asilimia 100 ya wananchi wanaoishi vijiji na wale wanaoishi mijini waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea na usanifu wa mradi wa kutoka Malagarasi, kupeleka maji hadi Tabora ili kuhakikisha kwamba vijiji vingi vinapata maji hayo. Katika usadifu huo unaendelea, pia kuna sehemu ambayo itatafiti uwezekano wa kuchota maji, kuweka mradi wa maji kutoka Mto Ugalla na kupeleka Wilaya ya Urambo ambayo itahusisha pia kupeleka maji katika Kata ya Usoke.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta kwamba nitakuwa tayari kuambatana naye kwenda kuangalia tatizo la maji katika Mji wa Urambo. (Kicheko/Makofi)

**SPIKA:** Muuliza swali, Mheshimiwa Sitta kuna neno?

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri amejibu vizuri. Swali langu liliuwa ni kuhusu vipingamizi ambavyo vimekuwa vikitumika vya wanyama kwamba ni Mbunga ya Wanyama; na pili suala la misitu. Mimi naomba Serikali itoe kauli yake kwamba hivyo vipingamizi havitakuwepo.

**SPIKA:** Waziri wa Maji mwenyewe, Mheshimiwa Engineer Lwenge!

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Pia nampongeza Mheshimiwa Sitta kwa namna anavyofuatalia tatizo

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Ia maji kwa wananchi wa Urambo. Amekuja Wizarani, tumeongea naye na kimsingi tumekubaliana kwamba maji ya wananchi wa Urambo tutayatoa Mto Ugalla. Suala la kufanya upembuzi yakinifu ni jambo la msingi katika miradi yote. Ni lazima tufanye haya maana kule Ugalla ni Hifadhi. Sasa ni lazima tufanye mawasiliano nao kwamba tutapitisha mabomba sehemu zipi na itaathiri vipi! Masuala haya ni ya msingi lakini haitazuia mradi ule kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nikuhakikishie kwamba tutapeleka maji kupitia kwenye Hifadhi, lakini mawasiliano ya kimsingi kati ya Wizara husika; Maliasili na Utalii pamaja na Ofisi ya Rais, Mazingira, lazima tuyafanye ili tuweze kukubaliana vigezo vipi tuvifanye na mradi uweze kuwa endelevu kwa ajili ya faida ya nchi hii. Ahsante sana.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Keissy, swali fupi sana la nyongeza.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wizara ya Maji inafanya mikakati yake kwa kupata fedha; ni lini sasa Wizara ya Maji itakwenda Wilaya ya Nkasi kutumbua majibu ya ubadirifu wa hali ya juu katika Kijiji cha Chang'ombe, Matala, Kiando na Namanyere katika Miradi ya World Bank? (Makofii)

**SPIKA:** Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Keissy kuhusiana na matatizo ya utekelezaji wa miradi katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, nakiri kwamba tumeshawahi kuongea naye nje, amenitolea taarifa kwamba kuna miradi katika Wilaya yake ambayo haijaenda vizuri; sasa tumeanza kazi. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba sisi tunasema hapa ni kazi tu kwa kutekeleza kauli ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Nkasi, tatizo hili tunalifanyia kazi na imani yangu ni kwamba tutalipatia majibu kwa haraka sana.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Aboot.

**MHE. ABDULAZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Urambo linafanana na tatizo la Morogoro Mjini, wananchi wa Morogoro Mjini wanategemea maji Bwawa la Mindu. Vyanzo vingi vinavyomwaga maji katika bwawa la Mindu vimekauka. Kuna Mto Mgeta kilomita 60 kutoka Bwawa la Mindu.

Je, Serikali haiwezi ikaanzisha mradi wa maji kutoka Mto Mgeta ili kuweza kujaza Bwawa la Mindu na wananchi wa Morogoro wakaondokana na kero ya maji? (Makofii)

**SPIKA:** Majibu, Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, tutaangalia mapendekezo yake. Kwa sasa hivi tumeanzisha Awamu ya Pili ya Programu ya Maji katika nchi nzima.

Kwa hiyo, tutaangalia vyanzo vya maji vilivyopo na vingine vipyta ili kuhakishisha kwamba azma ya kupeleka maji kwa wananchi wote inatekelezeka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ushauri wako tutauzingatia.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**SPIKA:** Nashukuru. Naona muda wa maswali kwa kweli umepita sana. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tupunguze maswali ya nyongeza kwa maana ya urefu wa maswali, lakini upande wa Serikali na wenyewe tujitahidi vilevile kupunguza majibu yetu yawe mafupi zaidi ili muda wetu utoshe. Vinginevyo kila siku tutakuwa tunaenda nje kabisa ya muda wa maswali. Ila kwa kuwa ni mwanzo huu, naamini tutaendelea kuboresha kadri tunavyoenda.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni waliyoko Bungeni asubuhi hii. Wageni kumi wa Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ambao ni walemaru, watu wa familia yake wakiongozwa na Ndugu Mwita Possi. Simama! Karibu sana; Profesa Mwajabu Possi, karibu sana; Profesa Shaban Mlacha, karibu sana popote pale ulipo. Natumaini huyo ni Profesa wa UDOM.

**MBUNGE FULANI:** Yupo hapa.

**SPIKA:** Yupo hapo eeh! Karibu sana Profesa.

Wageni saba wa Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango ambao ni familia yake wakiongozi na Ndugu Mboni Mpango, mke wa Mheshimiwa Philip, karibu shemeji na Ndugu Flatery Seba Mpango ni kaka wa Mheshimiwa. Karibu sana. (Makofi)

Wageni kumiwa Mheshimiwa Rashid Chuachua ni ndugu na familia wakiongozwa na Ndugu Rajab Chuachua na Ndugu Joyce Mkaugala, karibuni sana. Wageni wa Mheshimiwa Godbless Lema, ambao ni Madiwani 14 wa Halmashauri ya Jiji la Arusha na viongozi mbalimbali wa CHADEMA na baadhi ya wananchi kutoka Arusha. Pale mlipo hebu simameni. Karibuni sana. Natumaini mmefuatilia kuhakikisha Mbunge wenu anaapishwa. Kazi hiyo tumeshaifanya. Sasa kazi kwake Mheshimiwa Lema kufanya kazi ya Ubunge. Karibuni sana ndugu zetu kutoka Arusha. (Makofi)

Wageni wa 15 wa Mheshimiwa Shaban Shekilindi kutoka Jimboni kwake wakiongozwa na Ndugu Roman Shekumkali na Ndugu Monica Shekumkali. Karibuni sana. (Makofi)

Wageni wa Mheshimiwa Goodluck Milinga, ambao ni Waheshimiwa Madiwani wanne, viongozi wa CCM wa Wilaya na wananchi, wakiongozwa na Ndugu Halid Nalioti - Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya na Ndugu Mathias Mbogo, Katibu wa Chama wa Wilaya. Naomba msimame! Karibuni sana. (Makofi)

Wageni kumi wa Mheshimiwa Deogratius Ngala wa wakiongozwa na Ndugu Thobias Thobias, Ndugu Kelvin Thobias na Ndugu Felician Haule. Wageni wa Mheshimiwa Ngala simameni! Ahsante na karibuni sana. (Makofi)

Naomba nimirambue mgeni wa Spika, Ndugu Dkt. Festus Limbu, ambaye yuko kwenye jukwaa la Spika pale, ni Mbunge wa Bunge la Kumi liliopita. Mheshimiwa Limbu karibu sana. Alikuwa Mbunge wa Magu, safari hii ameamua kuwa Mbunge mstaafu na pia alikuwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Bajeti ya Bunge. (Makofi)

Matangazo mengine ni haya yafuatayo; Mheshimiwa Hawa Gharia Mwenyekiti wa Bajeti anaomba Wajumbe wake kukutana mara baada ya matangazo hayo katika ukumbi wa Msekwa 'B'. Mheshimiwa Hawa Gharia, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti anaomba Wajumbe wa Kamati yake mkutane Msekwa 'B' baadaye kidogo.

Mheshimiwa Katibu wa Bunge analeta tangazo kwenu Waheshimiwa Wabunge wote kuwa wataalam wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) watakuwepo hapa Bungeni ili

## Nakala ya Mtando (Online Document)

kutoa huduma ya kupiga picha kwa ajili ya Vitambulisho vya Taifa kwa Wabunge na Watumishi wa Bunge ambao hawana vitambulisho hivyo. Zoezi hilo litafanyika kuanzia leo tarehe 26 Januari hadi tarehe 4 Februari, 2016 saa 3.00 asubuhi hadi saa 10.00 jioni wakati wowote unapopin pale chumba ni Na. 3 ghorofa ya kwanza ukumbi wa Pius Msekwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ambao hamna vitambulisho naomba mwende huko.

Tangazo lingine ni la Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa Kepteni George Mkuchika anasema kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo Jumanne, tarehe 26 Januari mara baada ya kusitisha Bunge saa 7.00 mchana, ukumbi Na. 229 ghorofa ya pili Jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho. Mtakumbuka kwamba niliwaarifu kuhusu kifo cha Bwana Oscar Godfrey Mtenda aliyekuwa Mshauri Mkuu wa Bunge wa Masuala ya Sheria katika Ofisi yetu ya Bunge, kilichotokea tarehe 24 Januari, 2016 katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma alipokuwa amelazwa kwa matibabu. Ibada ya kuaga mwili kuelekea Kijiji kwake Chikuyu itafanyika leo tarehe 26 Januari, 2016 kuanzia saa 6.00 mchana nyumbani kwake eneo la Wajenzi. Mazishi yatafanyika kesho na ratiba imetoka. Chikuyu siyo mbali sana kutoka hapa, ni kama saa moja tu kwa Wabunge ambao watakuwa tayari kwenda kesho hiyo mchana, basi tutafanya utaratibu wa kiofisi.

Matangazo yameisha, sasa tunaendelea na ratiba yetu. Kabla ya Katibu, Mheshimiwa Chief Whip, tafadhalil!

### HOJA YA KUTENGUA KANUNI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo ya hoja ya kutengua Kanuni za Bunge.

KWA KUWA Mkutano wa Pili wa Bunge umepangwa kumalizika tarehe 5 Februari, 2016;

NA KWA KUWA muda huu ni mfupi kwa Bunge kuweza kukamilisha shughuli zote zilizopangwa kufanyika katika Mkutano huu;

NA KWA KUWA Kanuni ya 28(2) inaelekeza kwamba Bunge hukutana kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 7.00 mchana na kuahirishwa mpaka saa 11.00 jioni, Kanuni ya 28 (15) inaelekeza kwamba Bunge halitaendelea na shughuli zake siku ya Jumamosi, Jumapili au siku ya mapumziko; na kwa mujibu wa Kanuni ya 62(1)(a), kila Mbunge anayejadili hoja huruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika 15;

NA KWA KUWA Kamati ya Uongozi katika kikao chake kilichofanyika tarehe 24 Januari, 2016 iliafiki kwamba kanuni husika zitenguliwe ili kuwezesha Bunge kukamilisha kwa ufanisi shughuli zote zilizopangwa kwa wakati huu na kutoa fursa kwa Wabunge wengi zaidi kuchangia hoja hizo;

HIVYO BASI, kwa mujibu wa Kanuni ya 153(1) naomba kutoa hoja kwamba Kanuni ya 28(2) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Bunge litakutana hadi saa 7.00 mchana na kuahirishwa hadi saa 11.00 jioni itenguliwe na badala yake Bunge lirejee saa 10.00 jioni.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kanuni ya 28(15) ambayo inaelekeza kwamba Bunge halitakutana siku ya Jumamosi, Jumapili na siku za mapumziko, itenguliwe na badala yake

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Bunge likutane siku ya Jumamosi, yaani tarehe 30 Januari, 2016, isipokuwa siku hiyo Bunge litaanza saa 3.00 asubuhi hadi saa 8.00 mchana na hakutakuwa na kipindi cha maswali.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 62(1)(a) ambayo inaelekeza kwamba kila Mbunge anayejadili hoja hataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika 15 itenguliwe na badala yake kila Mbunge ajadili kwa muda wa dakika 10 ili kuweza kuwa na wachangiaji wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa hoja; na imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, mapendekezo yaliyoko mbele yetu kama yalivyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, ni kwamba katika siku zote hizi tutakazokuwa na Bunge, tuwe tunaanza session yetu saa 10.00 jioni, lakini pia amependekeza uchangiaji wetu uwe ni wa dakika 10 badala ya dakika 15 za kikanuni ili wengi zaidi tupate nafasi na vile vile amependekeza tukutane katika siku ya Jumamosi.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**SPIKA:** Nawashukuruni sana. Huo ndiyo utakuwa utararibu wetu wa kazi. Katibu!

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge.

### UCHAGUZI WA WENYEVITI WA BUNGE

**SPIKA:** Naomba nikuite Katibu wa Bunge ambaye ndiye msimamizi wa uchaguzi ili uweze kutoa maelezo ya uchaguzi huo.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 11(1), katika Mkutano huu kutakuwa na Uchaguzi wa Wenyeviti watatu wa Bunge ambao watakuwa ndio wasaidizi wa Spika na Naibu wa Spika. Kwa sababu hiyo basi, naleta taarifa hii na kutoa maelezo ili Bunge lako liweze kufanya uamuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(8) ya kanuni za Bunge, Toleo la mwezi Januari, 2016, Kamati ya Uongozi imejiwekewa utaratibu wa kupendekeza majina matatu kutoka mionganini mwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti ili kupata majina ambayo Bunge lako litaridhia waweze kupata uamuzi wa kuwa Wenyeviti.

Kwa kutekeleza hilo, Kamati ya Uongozi iliyokutana ambayo wewe ulikuwa Mwenyezekiti wake ilifanya uamuzi na kuwapendekeza Wenyeviti wa Bunge watatu ambao nitayataja majina yao ili Bunge lako liweze kufanya uamuzi. Waliopendekezwa na Kamati ya Uongozi, Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wa Bunge watakaochaguliwa watashika madaraka yao kwa muda ambao wataendelea kuwa Wenyeviti au Makamu Wenyeviti wa Kamati zao za Kudumu za Bunge mpaka mwisho wa Mkutano wa Kumi wa Bunge ambao ndiyo unakamilisha nusu ya kwanza ya maisha ya Bunge. Hata hivyo, Wenyeviti hao wanaweza kuchaguliwa tena kuwa Wenyeviti wa Bunge katika kipindi cha pilii kilichobaki cha maisha ya Bunge la kipindi

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

kinachohusika iwapo tu watachaguliwa tena kuwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 11(2).

Hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya (5) na uamuzi wa awali yaani conventions Wenyeviti huwa wanapita bila kupingwa wanapopendekezwa bila kuwa na wagombea wengine. Kwa sababu hii, ninalileta kwako ili Bunge lako liweze kufanya uamuzi. Ahsante.

**SPIKA:** Sasa Waheshimiwa Wabunge naomba kwanza tuamue kuhusu utaratibu. Kama alivyoeleza Katibu, tukishawasikiliza na kuwaliza maswali kama yapo, nitatoa fursa hapo baadaye kidogo. Kisha mtaniruhusu nihoji ili tuwapitishe kwa utaratibu huo. Sioni mantiki ya kusema tupige kura kwa kila mmojawapo. Kama mnakubaliana kuhusu huo utaratibu! (Makofii)

Nawashukuruni sana kwa kunikubalia kuhusu utaratibu. Kwa sababu uchaguzi huu ni mdogo, tunaomba tukamilishe safu ya Spika, Naibu Spika na Wenyeviti watatu ili tukamilikie hapa mezani ili shughuli yoyote ile isiweze kukwama kwa sababu yoyote ile. (Makofii)

Kwa hiyo, Kamati ya Uongozi ilikaa na kupendekeza majina haya matatu. Hawa watatu watatusaidia kwa muda wa miaka miwili na nusu hadi katikati ya miaka yetu. Baada ya hapo, tuta-*confirm* tena kama wataendelea kuwa Wenyeviti au Makamu Wenyeviti wa Kamati kama futaaendelea nao au wengine kutohuna na Wabunge mtakavyoona inafaa. Kwa hiyo, bado liko mikononi mwetu, halina tatizo.

Basi namwita Mheshimiwa Mary Mwanjelwa aje hapa ajieleze dakika tatu na kama kuna maswali tumwulize. Baada ya hapo, atafuata Mheshimiwa Andrew Chenge na Mheshimiwa Najma ajiandae. Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, tafadhali. (Makofii)

Karibu sana Mheshimiwa Dkt. Mary dakika mbili tatu ajieleze kidogo. Karibu!

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Mawaziri, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Asalaam Aleykum!

**WABUNGE FULANI:** Waaleykum Salaam!

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Bwana Yesu Asifiwe!

**WABUNGE FULANI:** Amen!

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Waheshimiwa Wabunge, mimi naitwa Mary Mwanjelwa, ni Mbunge mwenzenu, mnanifahamu, nimesimama hapa kwa heshima na taadhima kuwaomba mniamini mnipe kura zenu zote za ndiyo kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania bila kujali itikadi kwa faida ya Taifa letu la Tanzania. Naomba kura zenu, naomba mniamini na sitawaangusha, naomba mnitume kazi hiyo, ahsanteni sana. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsanteni sana. Mheshimiwa Mary usiondoke. Kama kuna mwenye swali, Mheshimiwa Masoud, swali la kwanza.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mary Mwanjelwa, umesema kwamba tukuamini utatutumikia bila kufuata itikadi. Uzoefu wa Bunge liliopita, Wenyeviti katika kipindi kilichopita, waliomalizia malizia, hasa wakati wa kipindi cha maswali ya nyongeza upande huu wa Upinzani macho huwa yanafumbafumba kidogo.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Je, wewe tukikupa Uenyekiti, unawaambia nini upande huu wa kwetu wa UKAWA huku Upinzani kutupa nafasi inavyostahili kama sehemu nyingine akiwemo na Mwalimu wako?

**SPIKA:** Mheshimiwa Masoud anakuuiliza jicho lako la kushoto linafanya kazi vizuri?

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Masoud, nakushukuru sana kwa swali lako zuri. Kama nilivyosema katika maelezo yangu ni kwamba nitawatumikia kwa faida ya Taifa letu la Tanzania pasipo kujali itikadi kwa kuzingatia pia Kanuni za Bunge letu zinasema nini. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante. Naona hakuna swali lingine.

**MBUNGE FULANI:** Yapo!

**SPIKA:** Yapo! Ahsante sana. Karibu kaka.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mary Mwanjelwa, nilitaka kujua, una kitu gani tofauti ambacho unaweza kuliahidi Bunge hili kwamba endapo utakuwa Mwenyekiti, basi uthalitumikia tofauti na Wenyeviti wengine waliopita?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Mary.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mtolea, nakushukuru sana, swali lako ni zuri na halipishani sana na la Mheshimiwa Masoud. Mimi bado nasisitiza, kwa kuzingatia kwamba hili ni Bunge ambalo lina changamoto nyingi, sitajali itikadi, nasisitiza kuangalia Utaifa kwanza. Ahsante. (Makofii)

**SPIKA:** Swali la mwisho litoke kwa mama sasa pale. Tunajali jinsia. Karibu Mheshimiwa.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naitwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize Mheshimiwa Mary. Nampenda sana lakini CV yake kidogo tuipate, maana sisi wengine wageni, tunaomba tujue tu CV yake ili tukichukua hatua, tuchukue hatua tukijua tunamchagua mwenzeru mwenye sifa gani. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naghenjwa. Mheshimiwa Mary kwa kifupi sana!

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Kaboyoka nakushukuru kwa swali lako zuri. Katika Bunge liliopita mimi nilikuwa ni Mbunge, nilikuwa ni Mwenyekiti wa Chama cha Kupambana na Wabunge wanaopingana na Rushwa (APNAC) Tanzania na Bara zima la Afrika. (Makofii)

Vilevile vile nilikuwa ni Naibu Katibu Mkuu wa Wabunge wote Tanzania bila kujali itikadi; na kabla ya hapo nilishakuwa Mkurugenzi wa Shirika la Kimataifa la PSI Tanzania. Nina Shahada ya Uzamili ya Mass Communication pamoja na Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia; na vilevile nasoma shahada yangu ya uzamivu katika Chuo Kikuu cha Open University Tanzania.

**SPIKA:** Maswali matatu tayari. Karibu sana Mheshimiwa Mary uende ukapumzike kwenye kiti chako. Nakuruhusu uende sasa, lakini sema maneno mawili ya kuondokea, uwaage tu Wabunge.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mwanasheria Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, pamoja na Kiongozi Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa heshima na taadhima naomba mniamini, mnipe kura zenu zote. Ahsanteni sana.

**SPIKA:** Ahsanteni sana. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mary Mwanjerwa. (Makofii)

Sasa nimwite Mtemi Andrew Chenge. (Makofii)

Mheshimiwa Andrew Chenge, mbele yako ni Wabunge. Tunaomba uongee nao kidogo, kuhusiana na jambo lililo mbele yetu. Mheshimiwa Chenge, karibu. (Makofii)

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wenzangu; Asalaam alekyum!

**WABUNGE FULANI:** Waaleykum Salaam!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Bwana Apewe Sifa!

**WABUNGE FULANI:** Amen!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Tumsifu Yesu Kristo.

**WABUNGE FULANI:** Amen.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, niliyesimama mbele yenu, kwa jina naitwa Andrew John Chenge, Mbunge wa Bariadi katika Mkoa wa Simiyu na Mtemi wa Itlima. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, nasimama mbele ya Bunge hili kama mionganoni mwa Wabunge watatu waliopendekezwa na Kamati ya Uongozi, kwa nafasi ya Mwenyekiti wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kuitia kwako napenda niliahidi Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kwamba hii ni dhamana nzito kumsaidia Spika na Naibu Spika, lakini niwahakikishie, nitatekeleza jukumu hilo kwa uadilifu na kwa uaminifu ili nitende haki inayoonekana na bila chuki wala upendeleo wowote kwa faida ya kujenga misingi bora ya Bunge letu hili, lakini pia kwa kuwatumikia Watanzania wote. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe nakuomba kura yako, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Freeman Mbowe na Wabunge wote, kwa pande zote, upande wa CCM na upande wa...

**MBUNGE FULANI:** UKAWA.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Hapana, UKAWA hakuna Bungeni. Ni Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naombeni kura zenu. Ahsanteni sana. (Kicheko)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa John Chenge. Naona hakuna swalii!

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MBUNGE FULANI:** Aaah, jicho lako la kushoto! Umeshaanza wewe!

**SPIKA:** Yapo maswali kushoto kwangu eeh!

**MBUNGE FULANI:** Hili hapa!

**SPIKA:** Haya, kuna swali hapo, moja kwa moja!

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, naitwa Cecil Mwambe, Mbunge kutoka Jimbo la Ndanda. Mimi nina swali kwa Mheshimiwa Chenge.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge lililopita, tutakubaliana na Wabunge hapo ndani kwamba Chama chake pamoja na Wabunge kwa ujumla walimwajibisha kwenye wakati ule kashfa ya ESCROW. Sasa hivi anaomba kuwa Mwenyekiti, je, siku akiwa analiongoza Bunge hili na hoja hiyo ikarudi tena ndani, yuko tayari kuisimamia? Ahsante.

**SPIKA:** Naona kama siyo swali hivi! (Kicheko)

**MBUNGE FULANI:** Sikio lako la kushoto halisikii vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chenge kwa kifupi!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, napenda nimjibu Mheshimiwa Mbunge wa Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bunge letu linaongozwa na Kanuni na pale ambapo inakuja hoja mbele ya Bunge hili au kwenye Kamati zetu ambapo inaonekana kuna maslahi fulani au inakuhusu wewe mwenyewe, ni busara tukazingatia Kanuni, nafasi hiyo wewe ukaacha mwagine akaifanya ili shughuli za Bunge zisiwe na makandokando ya aina yoyote. Nadhani niishie hapo. Ningewenza kusema zaidi ya hapo, lakini naona niishie hapo. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante sana. CCM wapo eeh! (Makofii)

Ahsante sana, pale nyuma, Mbunge hapo!

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika kwa jina naitwa Richard Mbogo, Mbunge wa Jimbo la Nsimbo.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize swali. Bunge linaendeshwa na Kanuni na Kanuni ya 64 mara nyingi inakiukwa, sasa ukiwa Mwenyekiti, utachukuwa hatua zipi? Kanuni ya 64 inasema; mtu ana uhuru wa kuongea, lakini kuna kauli huwa zinatoka mbaya na hasa kifungu cha (g), kinasema mtu hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine. Endapo itatokea hivyo, utachukua hatua zipi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Chenge, majibu!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, ningependa nimjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kanuni za Bunge kama zilivyo Sheria nyingine za nchi, zinakata kote kote; ni msumeno. Kwa hiyo, iwapo itathibitika kwamba Mheshimiwa Mbunge amekiuka Kanuni ya 64, kitikitizingatia baada ya kupima kauli, maelezo aliyojatoa, humu Bungeni.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Kwa hiyo, ndiyo Kanuni zetu zinatutaka hivyo, tuhakikishe kwamba tunayoyasema humu Bungeni yawe ya kweli na kweli tupu, yasiwe ya uongo. (Makofii)

**SPIKA:** Swali la mwisho itakuwa ni jinsia sasa.

**MBUNGE FULANI:** Huyu hapa! Kushoto hapa! Huku! jinsia hii hapa!

**SPIKA:** Nyuma pale! Pale nyuma kabisa!

**MBUNGE FULANI:** Aah!

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Chenge, nina hili swali kwako. Kutokana na kwamba ulikutwa na tuhuma za ESCROW na hii ilipelekea mjadala mkubwa sana baina ya wananchi, hauhisi kwamba kuendelea kugombea nafasi hii inaweza kupelekea wananchi kukosa uaminifu na Bunge hili ambalo litakuwa linaongozwa na Mwenyekiti kama wewe ambaye ulikutwa na hizo tuhuma? (Makofii)

**MBUNGE FULANI:** Siyo swalii!

**MBUNGE FULANI:** Limeishaulizwa hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Ghasia!

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumwuliza mgombea, Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge swalii lifuatalo:-

Kuanzia leo mchana tutakuwa tunajadili hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo ameitoa hapa Bungeni. Kama tunavyokumbuka, siku ambapo amekuja kutoa ile hotuba, kuna wenzetu ambaa walitoka nje.

Je, Mheshimiwa Chenge, tukikupa kiti utawaruhusu kuchangia watu ambaa walitoka nje?

**MBUNGE FULANI:** Siyo swalii! Yuuuuwiiii yuuwiiiiii! Siyo swalii!

**MBUNGE FULANI:** Wote Wabunge!

**SPIKA:** Hilo la Mheshimiwa Hawa Ghasia nalijibu mimi mwenyewe kwamba Wabunge wote mna haki ya kuchangia Hotuba ya Rais. (Makofii)

**MBUNGE FULANI:** Kwa hiyo, bado swalii moja tu. Bado swalii moja!

**MBUNGE FULANI:** Anatia aibu!

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo maana akapigwa chini yule! Alipoteza sifa.

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Chenge maswali yameisha, unaweza ukarudi kwenye kiti chako. (Makofii)

Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Najma. Karibu sana Mheshimiwa Najma Giga kutoka Zanzibar.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Kiongozi Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, Asalaam Aleykum!

**WABUNGE FULANI:** Waaleykum Salaam.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mimi niliyesimama mbele yenu naitwa Najma Murtaza Giga, kitaaluma mimi ni Mwanasheria. Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, kutokana na uzoefu wangu katika fani hiyo ya sheria, mniamini kabisa na kunipa nafasi hii ya Uenyekiti ambayo ninaahidi kwamba nitakuwa msaada mkubwa kwa Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Wenyeviti wenzangu, kuhakikisha kwamba Sheria na Kanuni zinatekelezwa katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofii)

Hivyo basi, bila kupoteza muda, kwa heshima zote kabisa, naomba Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri, pamoja na Wabunge wote kutoka pande zote mnichague kwa kura za ndio ili niweze kuwa Mwenyekiti. Ahsanteni. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante sana. Hakuna swali! (Kelele)

**MBUNGE FULANI:** Yupo mtu anataka kuuliza swali! (Kicheko)

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Gekul!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi nimwulize mgombea swali moja.

Mheshimiwa Mgombea umesema kwamba wewe kitaaluma ni Mwanasheria; na naamini umepitia Kanuni zetu hizi za Bunge ambazo hivi karibuni utakwenda kuzitumia.

Katika Kanuni zetu kuna Kanuni moja ambayo huwa wakati wa Bajeti inaumiza sana Wabunge kujadili masuala ya wananchi na ni Kanuni ambayo inazungumzia masuala ya guillotine. Naomba nifahamu, msimamo wako juu ya Kanuni hiyo.

**SPIKA:** Unamtaka apinge Kanuni! Maana Kanuni ni Kanuni iko pale. Wajibu wake yeye ni kuisimamia tu. Mheshimiwa Najma kama una mafupi ya kueleza!

**MHE. NAJMA M. GIGA:** Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyotangulia kusema hapo mwanzo, nitafanya kazi zangu za usimamizi wa Bunge hili kwa mujibu wa Kanuni na Sheria. Kwa hiyo nitafuata yale ambayo yanastahiki kwa uadilifu na uaminifu mkubwa. (Makofii)

**SPIKA.** Ahsante sana. Mheshimiwa Sanga nilikuona, ulisimama.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kuniona na kunipa hii nafasi. Bunge lililopita, baadhi ya Wenyeviti tulipokuwa tunachangia walikuwa wanapendelea sana upande ule wa pili. Je, wewe tukikupa uta-balance vipi ili wote tuwe na haki za kuchangia? (Kicheko/Makofii)

**MHE. NAJMA M. GIGA:** Ahsante Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri. Kwa hakika mimi nikiwa Mwenyekiti hapa, basi nitahakikisha kwamba naweka maslahi ya Taifa mbele kwa kuwapa nafasi wote wenye haki ya kufanya hivyo. (Makofii)

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Najma. Swalii la mwisho, twende kwenye gender pia. Aliyesimama peke yake, karibu Mheshimiwa!

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Naitwa Angelina Malembeka kutoka Kaskazini Unguja.

Nilikuwa napenda kumwuliza Mgombea, Bunge la sasa hivi karibu asilimia 34 ndio waliorudi kutoka zamani. Je, unaweza ukajenga ushirikiano ili wa zamani na wa sasa tuwe pamoja? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Najma!

**MHE. NAJMA M. GIGA:** Mheshimiwa Mbunge, mahusiano na ushirikiano inategemeana na sisi wenyewe, lakini mimi nikiwa kama Mwenyekiti, nitahakikisha kwamba mahusiano hayo yanakuwa mazuri baina ya Wabunge wapya na wale wa zamani. Ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana, naomba sasa uende ukakae. Nakushukuru sana! (Makofi)

Sasa Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyoniruhusu kwamba tuhoji kwa upamoja wake ili tuweze kuwapata Wenyeviti watakaosaidiana na mimi, nami nitashukuru sana kupata watu wa kunisaidia wakati kwa wakati.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Hoja ya kuwapitisha Wenyeviti wa Bunge bila  
kupingwa iliridhiwa na Bunge)

**SPIKA:** Nawapongeza sana Wenyeviti, Wabunge wapya, Mheshimiwa Mary Mwajelwa, Mheshimiwa Andrew Chenge na Mheshimiwa Najma Giga. Karibuni sana katika uongozi. (Makofi)

Kwa sababu ya muda, mtawapongeza siku hiyo mtakapokaa mezani hapa, lakini kwa sasa hivi, mniruhusu tuendelee. Katibu tuendelee!

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Hoja za Serikali!

**SPIKA:** Hoja za Serikali, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kama una la kusema.

### HOJA ZA SERIKALI

**Hoja ya Kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa ufunguzi wa Bunge la Kumi na Moja, Tarehe 20 Novemba, 2015**

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu hoja ya kujadili hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa tarehe 20 Novemba, 2015 wakati wa ufunguzi wa Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais imetoea mwelekeo na dira ya Serikali ya Awamu ya Tano itakavyoendeshwa na kutekeleza ahadi alizotoa kwenye ilani uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 na ahadi alizotoa katika mikutano ya kampeni katika maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais imemeleza vipaumbele mbalimbali vinavyotarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imejipanga kikamilifu kutekeleza vipaumbele vilivyotamkwa na ambavyo vimejiwekea mipango na mikakati madhubuti ya utekelezaji maeneo yote ya nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hotuba ya Mheshimiwa Rais kutolewa, Wizara na Taasisi zote ziliichambua hotuba hiyo, kuainisha maeneo mbalimbali ya utekelezaji katika bango kitita na kupanga mipango ya utekelezaji wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu na tayari utekelezaji wake umeshaanza kutekelezwa kwenye maeneo kadhaa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote wa vyama vyote kutumia fursa hii adhimu kutoa michango itakayosaidia Serikali katika utekelezaji wa mambo mbalimbali yaliyoainishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, pamoja na ukweli kwamba tayari utekelezaji wa mambo mbalimbali umeshaanza kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kaulimbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya "Hapa Kazi Tu", bado Serikali inahitaji sana michango yenu na mawazo yenu Waheshimiwa Wabunge ili iweze kuboresha maeneo ambayo tunaona ni muhimu yakaboreshwa, lakini pia yanahitaji usimamizi wa karibu katika utekelezaji. Napenda kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba michango yenu itaheshimiwa, itathaminiwa, lakini pia tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, nashukuru kwa fursa hii na ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkoo kwa hotuba fupi na nzuri. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kama kawaida ya hoja, itabidi tuiamue.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**SPIKA:** Naomba niwashukuru sana. Kwa hiyo moja kwa moja katika kuokoa muda tunaingia katika awamu ya uchangiaji. Namwomba sasa Mheshimiwa Naibu Spika aje ili anipokee na aendelee na uendeshaji wa shughuli za mezani.

Hapa Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumeletewa maombi kadhaa, kwa hiyo, tuna majina hapa kama alivyokuwa ametangaza kwamba mlete majina kwa ajili ya kuchangia. Kwa

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

hiyo, kwa muda wetu uliobaki tutaanza kwa kutaja majina kadhaa kwa ajili ya uchangiaji halafu tutaona tunakwenda mpaka saa ngapi halafu tutakutana hiyo saa 10.00 jioni kuendelea.

Mchangiaji wa kwanza ni Mheshimiwa Pascal Haonga atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Khatib Kai, halafu Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq. Karibu Mheshimiwa Pascal.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais na ninaomba...

### MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mwongozo!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo!

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo ni wapi?

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mimi hapa Mheshimiwa

**NAIBU SPIKA:** Nani aliyeomba Mwongozo?

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni mimi hapa!

**NAIBU SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Munde!

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi bado sijaelewa vizuri. Wenzetu wa UKAWA wakati Mheshimiwa Rais akilihutubia Bunge hili walitoka nje kwa kejeli, kwa matusi, kwa kuzomea na kwa dharau kubwa. Hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Watanzania wote wanatutazama, wanatupima kwa tabia zetu.

**MBUNGE FULANI:** Wewe vipi?

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Sasa naomba mwongozo wako, kwa nini watu hawa wapate uhalali wa kujadili hotuba ya Mheshimiwa Rais?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

(Hapa Wabunge kadhaa waliomba Taarifa,  
na wengine kusimama)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kabla Spika hajatoka hapa, hilo swali limeulizwa na baada ya kuuliza Mheshimiwa Spika ameshaliamulia jambo hilo. (Makofii)

## Nakala ya Mtando (Online Document)

**MBUNGE FULANI:** Watoke nje!

**NAIBU SPIKA:** Tusikilizane basi Waheshimiwa Wabunge. Mmeomba Mwongozo, natoa Mwongozo, tusikilizane.

Mheshimiwa Spika ametoa maelezo ya hilo jambo, ametoa fursa kwa Wabunge wote kuchangia hoja ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, baada ya kuyasema hayo, Mheshimiwa Haonga endelea.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nichangie ukurasa ule wa nane na wa 17 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa ule wa nane hotuba ya Mhesimiwa Rais imegusa suala la walimu pamoja na malalamiko yao kwamba wana malalamiko. Ni kweli kabisa kwamba suala hili ni suala ambalo lipo. Walimu wana malalamiko kwamba hawana nyumba, lakini pia imefika mahali wana madai ya muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali ya awamu ya tano ambayo ina slogan ya Hapa Kazi Tu; kama kweli itakwenda kujenga nyumba za walimu, italipa madeni sugu ya walimu ya muda mrefu sana, nadhani nchi hii kweli itakwenda, kwa sababu awamu zote zilizopita wote hawakuona umuhimu wa kuwalipa walimu madeni na kuwajengea nyumba bora. Kwa hiyo, nadhani Serikali hii ikifanya hivyo mambo yatakwenda vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano mdogo. Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi hivi ninavyozungumza inaonekana kwamba walimu waliosimamia mtihani wa kidato wa cha nne mwaka 2014 hawajalipwa fedha zao; na sio walimu tu lakini pia na Watumishi mbalimbali wa Halmashauri wakiwepo askari na madereva. Kwa hiyo, naomba katika haya maneno aliyoazungumza Mheshimiwa Rais muweze pia kuliangalia hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani kabisa kwamba Serikali yoyote ambayo iko makini inafika mahali deni la mwaka wa jana halijalipwa, lakini leo sina uhakika sana kama sisi Wabunge kuna Mbunge ambaye anaweza akawa anadai deni la mwaka wa jana au mwaka wa juzi. Inawezekana walimu wamesahaulika sana katika Taifa hili, ndiyo maana tunafikia hali kama hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba walimu wakumbukwe na deni hili lilipwe kwa kweli; walimu wa Halmashauri ya Mbozi na walimu wengine wowote wanaoidai Serikali. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichangie ukurasa ule wa 17. Wakulima imefika mahali wana malalamiko makubwa sana. Mheshimiwa Rais alipokuwa akilihutubia Bunge, alisema atawasaidia wakulima, ataondoa ushuru wa kwenye mazao. Kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi tunalima sana kahawa, wakulima wana shida kubwa sana, wanatozwa ushuru wa kahawa 5%, ambayo ni sawasawa na shilingi 175/= kwa kilo moja; lakini pia wanatozwa ushuru wa Bodi ya Kahawa; ushuru wa utafiti; wakulima wamebebeshwa mzigo mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali hii ya awamu ya tano iweze kuliangalia hili. alichokuwa anakizungumza Mheshimiwa Rais naomba akifanyie kazi kweli kweli na isiwe maneno tu. Ninaamini kabisa kwamba Mungu atambariki na atakwenda kuwasaidia wakulima wetu. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni mzigo, inafika mahali mkulima wa kahawa licha ya kwamba anatozwa ushuru huo ambaa nimesema ni 5%, pamoja na matatizo mengine lakini

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

mkulima huyu wa kahawa na mazao mengine ameshindwa kutafutiwa somo zuri na mwisho wa siku inaonekana kwamba anauza kwa bei ndogo sana. Kwa mfano, msimu uliopita wakulima wa Kahawa wameuza kahawa yao kwa bei ndogo sana.

Naomba Serikali iangalie suala hili maana bila kuwasaidia wakulima kwa kweli tutakuwa tunarudi nyuma, maana tunajua kabisa kwamba kilimo kinachangia zaidi ya asilimia 70 ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niweze kuzungumza kwa ufupi sana ukurasa wa nne wa hotuba ya Rais. Alizungumzia suala la siku ya uchaguzi kwamba ilikuwa na utulivu na amani. Naomba nizungumze tu kwamba katika hili nadhani Rais wetu atakuwa kidogo aliteleza. Siku ya uchaguzi tarehe 25 Oktoba, 2015 ilikuwa na amani na utulivu; hayo maneno sijajua vizuri kwamba labda alikosea au aliteleza.

Ni kwamba kuna maeneo mengi sana vurugu zilifanyika, kuna watu walipigwa, watu waliwekwa ndani, watu wamebambikiwa kesi, watu hadi leo wengine wamekimbia maeneo yao, halafu Rais anasema eti siku hiyo ilikuwa ya amani na utulivu. Mimi nadhani kuna watu labda walimpotosha Mheshimiwa Rais kwenye hili, nami naomba tu Mheshimiwa Rais inabidi kidogo afuatilie hili vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano natoa mfano mdogo wa Jimboni kwangu Mbozi. Jimbo la Mbozi uchaguzi siku ya Jumapili, tarehe 25 Oktoba, 2015 watu waliwekwa ndani wakiwa wanadai matokeo. Wamefunguliwa kesi hadi leo! Wengine wameshakimbia, hivi ninavyozungumza hawapo kwenye Jimbo langu. Mheshimiwa Rais anakuja anasema kwamba Uchaguzi ulikuwa wa amani na huru.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu kwamba siku nyingine Serikali tujipange vizuri. Kunapokuwa na uchaguzi tujaribu kutumia Jeshi la Polisi vizuri na yule aliyeshinda kihalali atangazwe haraka sana. Kwa sababu mambo yote haya yanajitokeza pale mtu ameshinda wanashindwa kutangaza matokeo mapema, inafika mahali watu wanadai matokeo wanaanza kupigwa, wanapelekwa ndani, wanafunguliwa kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili kwa kweli linasikitisha sana na machafuko mengi tu yametokea katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwengine mdogo tu naweza nikatoa. Hata ndugu zetu kule Zanzibar hali kwa kweli haiko shwari kabisa hadi hivi ninavyozungumza. Hali haiko shwari! Hili limejitokeza! Mwenyekiti wa ZEC amekaa peke yake anatangaza kwamba tunarudia uchaguzi wakati huo unaona kabisa kwamba hawajakubaliana na Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, imefika mahali na ushahidi upo, tutajaribu kuwasilisha kama utahitajika kwa muda ambao tutapangiwa, Makamu Mwenyekiti wa ZEC alikamatwa akawekwa ndani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haonga naomba umalize!

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Kwa hiyo, hali haikuwa nzuri, hapakuwa na utulivu wowote ule. Naomba tunapoelekea huko siku za usoni kweli kabisa tuishauri Serikali isimamie uchaguzi vizuri, aliyeshinda awe ameshinda na mambo yaweze kwenda vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichangie suala lingine. Kwenye kilimo kuna suala dogo nilikuwa nimelisahau, kuhusu mfumo wa vocha ambao Serikali inautumia kuweza kuwapa

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

wakulima. Mfumo wa vocha kusema ukweli siyo mzuri kabisa. Vocha hizi zinawanufaisha wale watendaji wachache, Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata na watu wachache, mara nyingi sana wanazigawa kwa kufuata itikadi ya Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hizi vocha za pembejeo zinazotolewa kuna mtu akiwa chama fulani cha upinzani vocha hizi hazimhusu, hata kama ni mnufaika, hapewi. Vocha hizi zinawanufaisha watu wachache sana. Natoa mfano mdogo tu, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, msimu wa kilimo huu uliokwisha vocha zilikuja 13,000 kwa Wilaya nzima ya Mbozi. Wilaya ina wakazi zaidi ya 500,000 vocha zimekuja 13,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwamba mfumo huu siyo mzuri kabisa, ni mfumo wa ubaguzi, hauwezi kuwasaidia wakulima wetu. Nasema kabisa kwamba kuna namna ambayo inatakiwa tuifanye ili kubadilisha mfumo huu wa kugawa vocha hizi za kilimo. Kama kuna uvezekano Serikali itafute utaratibu mzuri kwamba mbolea inapoingizwa nchini, kama Serikali inaweza ikatoa ruzuku moja kwa moja kwa ile mbolea inapoingizwa nchi nzima, inapouzwa basi iwe imeshalipiwa ruzuku na kila kitu, angalau sasa ionekane ni ya ruzuku nchi nzima, hata kama ni pesa kiasi kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mfuko wa mbolea leo unauzwa shilingi 70,000/=. Labda mfuko wa mbolea Dar es Salaam hapo unauzwa shilingi 70,000/=. Kama Serikali inaweza ikaweka pesa yake ya ruzuku kidogo pale, ikalipa kwa mfano hata 40% au 50%, maana yake shilingi 70,000/= inaweza ikashuka hadi kufikia shilingi 35,000/=hadi shilingi 40,000/=. Hiyo ni nchi nzima, maana yake watu wa Mbozi wanunue kwa bei hiyo, lakini pia watu wa Kigoma wanunue kwa bei hiyo kuliko mfumo wa sasa ambao unawanufaisha wafanyabiashara wachache, lakini pia ni mfumo wa kibaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba suala hili tuliangalie sana kwa sababu Tanzania bila kilimo haiwezekani, ninaamini Kilimo kinachangia asilimia kubwa sana katika pato la Taifa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Haonga, muda wako umekwisha.

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kidogo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haonga muda wako umekwisha tafadhali! Mheshimiwa Hajji Khatib Kai! Mheshimiwa Abdallah Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami kwanza nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Temeke kwa kuniamini na kunipa fursa ya kuwatumikia. Nawaahidi tu wasiwe na wasiwasi, nitawatumikia kukidhi mahitaji yao. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeipitia hii hotuba ya Mheshimiwa Rais na yako mambo ameyataja, lakini vizuri tungependa tuyaongezee nyama ili Serikali inapokwenda katika utekelezaji wake, basi iweze kuyatekeleza haya kwa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la afya. Kumekuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa huduma ya afya hasa kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam. Serikali iliwhahi kuzipandisha hadhi hospitali za Temeke, Amana na Mwananyamala kuwa katika hadhi ya Hospitali za Mkoa, lakini baada ya kuzifanya hivyo, haijawahi kuzipa support kwa maana ya

## Nakala ya Mtando (Online Document)

kuzihudumia kama Hospitali za Mkoa na badala yake majukumu hayo yameachiwa Halmashauri, na kwa uwezo wa Halmashauri zetu imekuwa ni vigumu kuhakikisha inaboresha huduma katika hospitali hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana sasa hivi hospitali hizi za Temeke, Amana na Mwananyamala zimebaki kuwa kama sehemu ya mifano mibaya, yaani ukitaka kutoa mifano mibaya au kuonesha watu kwamba huduma mbaya hospitalini zinapatikana wapi, basi ni vizuri ukawapeleka katika hospitali hizi, maana watashuhudia wagonjwa wanalala chini, dawa hakuna, au wengine wakilala watatu watatu kwenye vitanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Serikali hii ya Awamu ya Tano ikahakikisha kwamba matatizo ya vitanda, wauguzi na dawa hospitalini yanakwisha kabisa. Tupatiwe vitanda vya kutosha katika Hospitali ya Temeke, tupate madawa, wananchi watibiwe pale; na wakifika waone kwamba wamefika sehemu salama na magonjwa yao yatakwisha. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni elimu. Serikali imeanza kwa kuondoa michango na ada, lakini hili ni suala dogo sana katika matatizo ya elimu yanayoikabili nchi hii. Bado hizi shule, hasa Shule za Msingi. Kwa Dar es Salaam tu ukitembelea Shule za Msingi utagundua kwamba shule zina matatizo makubwa, achilia mbali tatizo la madawati, lakini majengo yenye, mapaa yametoboka, sakafu zimekwisha. Kuna madarasa ukipita unaweza kufikiri kwamba hapa ni kituo cha kuwekea ng'ombe kabla hawajakwenda kuchinjwa, lakini kumbe ni madarasa hayo, watoto wanakwenda kusoma pale. Unajiliza, mtoto huyu anawezaje kuipenda shule akiwa anakaa chini, hana madawati, sakafu imeharibika na juu kunavuja? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri tunakoelekea katika Bajeti ya mwaka 2016/2017 Serikali iamue jambo moja, itoe mikopo ya elimu kuanzia Shule za Msingi ili mzazi aweze kuchagua shule ya kumpeleka mtoto wake kulingana na viwango vya ufaulu na siyo kwa sababu tu hana ada. Hii itatusaidia kuondoa ile gap ya nani anasoma katika shule nzuri na nani asome katika shule mbaya. Maana yake anayesoma katika shule nzuri ndiye atafanikiwa; na hao ni watoto wa matajiri; hao ambaa wasoma kwenye shule hizo mbovu, hawawezi kufanikiwa, tunaua vipaji vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa napenda Serikali ilichukulie hili kama jambo muhimu sana. Tuondoe madaraja ya elimu kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake alizungumzia suala la Mahakama Maalum kwa ajili ya Mafisadi, lakini amesahau pia kuzungumzia Mahakama Maalum ya wale wanaowatesa na kuwaua ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi (albino).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu tumekuwa na hili tatizo. Albino wanauawa, wanakatwa viungo vyao, na hizi kesi zao zinachelewa sana Mahakamani. Mwisho wa siku hata wale wachache ambaa wamehukumiwa, hasa waliohukumiwa vifungo vya kunyongwa hadi kufa, inasemekana hakuna aliywahi kunyongwa. Hiyo ni kwa sababu kabla ya utekelezaji wa hiyo adhabu, Mheshimiwa Rais anahitaji kusaini kwa ajili ya kutekeleza matakwa ya kikatiba.

Sasa tumtake Rais huyu wa Awamu ya Tano atuneshe mfano kwamba na ye ye anachukizwa na mauaji ya albino. Atie nguvu kuhakikisha kesi zile zinasikilizwa na zinafika mwisho haraka. Waliohukumiwa kunyongwa, wanyongwe mpaka kufa ili jamii ione kwamba kweli Serikali imeamua kukomesha tatizo la mauaji ya albino. (Makofii)

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la uingizaji, usambazaji na matumizi ya dawa za kulevy. Kwa sisi tunaokaa Dar es Salaam hasa pale Jimboni kwangu Temeke ambako ni moja kat i ya maeneo ambayo yameathirika na matumizi haya ya dawa za kulevy, hatuamini kama kweli Serikali imewahi kuchukua jitihada za dhati au ina mipango ya dhati ya kukomesha uingizwaji na usambazwaji wa dawa za kulevy.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa uingizaji wa dawa za kulevy katika nchi hii haujawahi kuyumbishwa hata kidogo. Mfumo wa kuingiza mafuta ya petroli ukiyumba, siku mbili tu utaona watu wanahangaika kutafuta mafuta. Mfumo wa chakula ukiyumba, utaona watu wanahangaika kutafuta chakula, lakini niwahakikishieni, hatujawahi kuona hawa watumiaji wa dawa za kulevy wakihangaika kutafuta dawa hizo. Maana yake mfumo wa kuingiza na kusambaza haujawahi kuyumbishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaitaka Serikali hii ya Awamu ya Tano kuweka jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba inadhibiti uingizaji wa dawa za kulevy, lakini pia usambazaji huko mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila siku tunapishana na polisi na magari yao hayo maarufu kama defender, wamekamata wauza gongo na wauza bangi, lakini hatuoni wakikamata hawa wanaouza dawa za kulevy. Huwezi kuniambia kwamba wanaouza haya dawa za kulevy wanajificha sana, kwa sababu wale watumiaji wenye muda wote unawakuta kama wameshalewa, lakini akizunguka nyumba ya pili, ya tatu ameshapata, anatumia tena. Ni kwa nini Serikali haiwaoni? Kwa nini isidhibiti huku kwa wauzaji wadogo wadogo ambao ndio wanaotuharibia vijana wetu na ndugu zetu?

Kwa hiyo, tunaomba Serikali ya Awamu ya Tano iweke macho sana katika kukomesha uingizaji wa dawa za kulevy.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni hili la amani na usalama. Mheshimiwa Rais katika hotuba yake pale ukurasa wa kumi amesema kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kushirikiana na Chama cha Wananchi (CUF) na CCM zinafanya jitihada ya kuondoa tatizo la kisiasa lililopo Zanzibar. Hapa ukiangalia kauli hii ni kama vile Mheshimiwa Rais anajitoa katika kushughulikia tatizo la Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, unawezaje kuiachia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ishughulikie tatizo la Zanzibar wakati tatizo lenyewe linahusu kuiweka Serikali madarakani? Serikali imemaliza muda wake, Serikali nyingine haitaki kutangazwa. Tumtake Mheshimiwa Rais ambaye kimsingi wananchi tuna imani naye kubwa sana, ameanza kuonesha kwamba analolisema analitekeleza. Hebu aamue sasa kusema kwamba aliyeshindia katika uchaguzi wa Zanzibar tarehe 25 Oktoba 2015 atangazwe kuwa Rais. (Makof)

**MBUNGE FULANI:** Uchaguzi haujaisha! (Makof)

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kuona suala la Zanzibar kama ni la Zanzibar, lakini hili suala siyo la Zanzibar, ni suala la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii heshima ya amani na usalama ambayo Watanzania tunayo leo ni kwa sababu nchi nzima iko salama. Sehemu moja ikianza kutumbukia katika machafuko, hakuna atakayekuwa salama hata huku kwetu. Kwa hiyo, tulichukulie hili jambo kama suala la Kitaifa na siyo suala la kisiasa.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mtu anafahamu kilichotokea katika uchaguzi wa Zanzibar. Mshindi kapatikana na kama kuna matatizo kwenye baadhi ya Majimbo, uchaguzi urudiwe kwenye Majimbo hayo ambayo yana matatizo, siyo uchaguzi wote. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuiombe Serikali hii, tumwombe Mheshimiwa Rais ahakikishe...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtalea, ahsante. Naomba umalize.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumwombe Mheshimiwa Rais ahakikishe mshindi kwa uchaguzi wa Zanzibar anatangwazwa. Ahsante. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq atafuatiwa na Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo na mimi niwe mionganini mwa wachangiaji katika hotuba ya Mheshimiwa Rais alioitoa hapa Bungeni tarehe 20 Novemba, 2015 hapa Bungeni. Awali ya yote, naomba kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayofanya; na niwacombe sana Watanzania wote tumwombee na tumtakie heri aweze kutimiza malengo yake kwa faida ya Taifa letu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana wananchi wa Mvomero kwa kunikumbuka tena kwenye ufalme wao, hatimaye nimerudi tena mjengoni. Nawashukuru sana na ninawaahidi sitawaangusha. Nawaahidi wananchi wa Mvomero sitawaangusha, ujinga ni pa kwenda siyo pa kurudi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais katika maeneo mbalimbali na pia nimpongeze kwa juhudini kubwa alioianza katika kuboresha uchumi wa Taifa, katika kupambana na mafisadi, katika kuboresha mapato ya nchi yetu. Bado tuna mianya mingi, bado tuna kazi kubwa ya kumshauri na kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu. Yapo majipu mengine yeye hayajui, sisi tunaoishi na wananchi, tunaokaa kwenye Halmashauri tunayafahamu, ni wajibu wetu tumsaidie ili sasa turudi kwenye mstari. Taifa hili lina kila aina ya neema, ni nchi ambayo ina baraka kubwa za Mwenyezi Mungu. Tuna maziwa, tuna madini, tuna bahari, tuna ardhi kubwa, ni nchi ambayo inatakiwa isonge mbele kimaendeleo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na suala la wakulima na wafugaji. Katika Taifa letu lipo tatizo kubwa la wakulima na wafugaji hasa katika Wilaya yangu ya Mvomero. Eneo hili linahitaji kazi ya ziada. Nami napenda kuishauri Serikali kuititia kwa Wizara ya Ardhi, Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Mifugo na Kilimo na Wizara ya Maliasili zishirikiane kwa pamoja. Hawa wote ni wadau wakubwa katika eneo hili la kuondoa tatizo la wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo kubwa kwenye maeneo yetu lakini bado tuna maeneo ambayo ni hifadhi. Hifadhi zile zinabaki kuwa hifadhi, lakini baadhi ya maeneo ya wakulima wanahangaika, wafugaji wanahangaika, hifadhi nyingine hazina tija kwa Taifa letu.

Namwomba sana Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kama Waziri wa Kilimo, aliangalie hili, ashirikiane na wadau wenzake, tuwapatie maeneo wafugaji, tuwapatie maeneo ya ziada wakulima na tuweke sheria thabiti kuondoa maafa, kuondoa machafuko kati ya wakulima na

## Nakala ya Mtando (Online Document)

wafugaji. Tukiweka utaratibu huo mzuri, nasi kwenye Halmashauri zetu tukatengeneza sheria za kuwadhibiti tutaleta maendeleo ndani ya kilimo, ndani ya ufugaji. Kwa kuwa muda ni mdogo, naomba niende haraka haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niingie kwenye suala la uchumi. Naiomba sana Serikali ifanye kazi ya ziada kwa kuhakikisha kwamba tunaweka sera nzuri za kuendelea kuwatambua wafanyabiashara, kwa maana ya sekta binafsi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna nchi yoyote duniani ambayo imesonga mbele kiuchumi bila sekta binafsi. Sekta binafsi ni mhimili mkuu wa Taifa. Sekta binafsi inaweza ikaongeza pato la nchi yetu, lakini katika sekta binafsi wapo wafanyabiashara wana upungufu. Ni vyema sasa tukaweka utaratibu mzuri, tushirikiane na sekta hii kukuza viwanda na uchumi wetu. Yapo mambo mengi kwenye sekta binafsi yanatakiwa yashughulikiwe. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kwamba Mheshimiwa Rais ana ndoto kubwa ya viwanda katika Taifa letu. Tatizo lililopo katika suala zima la viwanda ni sera za nchi yetu. Yapo maeneo sera zinatubana. Ni vyema tukakaa tukarekebisha sera zetu, tukaangalia wapi tulikosea, wapi tupo na mabadiliko ya dunia ya leo yanensemaje. Tukibadilika katika utaratibu huo, sasa tunarudi kwenye kuanzisha na kusimamia viwanda. Hapo tutasonga mbele kwa hatua kubwa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la baadhi ya wafanyabiashara kutokuwa waaminifu. Naomba wanaohusika na masuala ya bajeti, wanaohusika na masuala ya uchumi, mfanyabiashara mwenye kiwanda cha mafuta ana-declare analeta crude oil kumbe anadanganya analeta semi. Hawa ndio amba wanadunisha, viwanda haviendelei, tunarudi nyuma, wao wanunuifaika. Wanacheza na Kamati ya Bajeti, wanacheza na wahusika, wanaingiza mambo yao kwenye bajeti. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha nina imani na wewe, najua uzoefu wako, anza kupambana na mambo haya katika bajeti ya mwaka huu. Usiruhusu wenye viwanda vya ndani walete udanganyifu. Tunachotaka, uchumi ukue tupate maendeleo. Mvomero tunahitaji barabara ya lami ikamilike, Mvomero tunahitaji umeme ufile vijiji vyote, Mvomero tunahitaji leo maji yafike maeneo yote. Lakini maji yale hayatafika kama uchumi utalegalega. Tutaisaidia Serikali, tutakaa na Mawaziri, dakika kumi hazitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la umeme. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri mhusika, lakini ushauri wangu katika suala la umeme tuongeze nguvu zetu katika kuzalisha umeme wa maji na umeme wa gesi badala ya kutegemea umeme wa mafuta amba unawanufaisha wafanyabiashara na Taifa tunabaki nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono juhudzi zote, umeme wa maji, umeme wa gesi na umeme wa mafuta haufai, haufai, haufai! Umeme wa mafuta ni biashara ya wakubwa. Wamejiandaa, wana mambo yao, wanafanya kazi zao. Sisi tuongeze nguvu kwenye gesi, maji na kwenye umeme wa upepo. Najua bado dakika zinaniruhusu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la vocha za mbolea. Kuna tatizo kubwa sana vijijini, kuna watendaji ndani ya Serikali ndani ya Halmashauri zetu sio waaminifu. Baadhi yao vocha hizi wanunuifaika wao badala ya kumnuifaisha mkulima wa kijijini. Mheshimiwa Mwigulu nakuaminia sana, umefanya kazi nzuri na unaendelea kufanya. Tuendelee kukusaidia kama Wabunge ili uboreshe eneo hili kwa faida ya nchi yetu.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uchaguzi wa Zanzibar ni suala la kisheria. Tuwatakie Wazanzibar uchaguzi mwema. Wanaopiga kelele, waendelee kupiga kelele, uchaguzi umetangazwa unarudiwa. Mheshimiwa Rais hawezi kuingilia tena. Tume ya Uchaguzi Zanzibar imetangaza uchaguzi urudiwe, tuwatakie uchaguzi mwema tarehe 20 Machi. Tutampata ambaye atachaguliwa kwa haki. Mizengwe mizengwe iliyokuwepo nyuma ndiyo imesababisha uchaguzi ule umefutwa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwe wa kweli. Sasa hivi tumtakie mema Rais wetu afanye mambo mengine makubwa, tusimchanganye. Tumepata Rais ambaye anaweza kutuvusha hapa tulipo, haogopi, ni mwewa, ni mwaminifu kwa Taifa lake. Ana ndoto nyingi ambazo anahitaji kuzitimiza kwa Taifa lake. Tumpe ushirikiano, tuache maneno maneno, tusonge mbele. Kama mlikuwa mna uchungu, mngemsikiliza Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Nawatachia kila la heri Watanzania wote. Ahsante sana. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sixtus Mapunda atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa muda tulionao.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia mchana wa leo. Awali ya yote nachukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi wapenda amani wa Jimbo la Mbanga Mjini kwa heshima kubwa walijonipatia, nami nawahakikishia tu kwamba sitawaangusha, nitawawakilisha kama wanavyotarajia. (Makofii)

Pia nachukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli kwa kutoa hotuba nzuri, iliyosheheni weledi, iliyoangalia kila sekta na kwa maoni makubwa na mapana kwa maslahi ya Taifa hili la Tanzania. Nawaomba tu Watanzania wote tuendelee kumwombea ili azma yake ya kuleta maendeleo ndani ya nchi hii ifanikiwe. Kusema ni rahisi, kutenda ni vigumu. Watapita wengi watakejeli, watapita wengi watasema lugha ambazo wanadhani zinastahili ili kuipunguza thamani hotuba ya Mheshimiwa Rais. Mimi niseme tu kwamba Mheshimiwa Rais ametenda, amesema, ameelekeza na utekelezaji tumeuona.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme neno moja tu kwa kifupi. Tunapozungumzia habari ya amani, umoja, mshikamano na utulivu wakati wa chaguzi, naomba niwakumbushe jambo moja. Watanzania tunaofanya active-politics tuko milioni tisa tunaotokana na vyama vyaa siasa. Milioni 50 ya Watanzania wote wanaobaki hawako kwenye active politics. Inapofika wakati wa uchaguzi, sisi milioni kumi tunajiona ndio wababe, tunaoweza kufanya kila kitu, tukawaacha Watanzania wengine, tunachoma matairi barabarani. Askari wakituzuia sisi wanasiaya, tunasema aaah, mnahatarisha amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tofauti kati ya kuhatarisha amani na kusimamia amani. Alichokieleza Mheshimiwa Rais katika hotuba yake, uchaguzi ulikwenda vizuri, zile rabsha rabsha mlizokuwa mnaziona za vyombo vyaa ulinzi na usalama vilikuwa ni kuhakikisha kwamba nchi hii inakuwa hamna amani. Nawashukuru sana Jeshi la ulinzi pamoja na Polisi kwa kazi kubwa waliyofanya. Sisi tutaendelea kuwatia moyo, fanyeni kazi kusimamia amani ili maendeleo yapatikane. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwenye sekta moja; sekta ya kilimo ukiondoa sekta nyingi ambazo Mheshimiwa Rais alizielezea katika hotuba yake. Katika hotuba yake Mheshimiwa Rais anakiri kwamba asilimia 95 ya chakula tunachokipata hapa nchini

## *Nakala ya Mtando (Online Document)*

kinatokana na Sekta ya Kilimo, lakini anakubali kwamba asilimia 30 ya mapato ya kigeni yanatokana na sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee niseme tu mambo machache kuhusu takwimu ya mwaka 2014, sekta gani ziliongoza kwenye kuleta pato la kigeni? Ukiondoa dhahabu ambayo ilileta shilingi bilioni 2,705, sekta zote zilizofuatia kwenye zile sekta tisa, zilikuwa ni sekta zenye uhusiano na kilimo. Korosho ilileta shilingi bilioni 647, Pamba ilileta shilingi bilioni 558, Tumbaku ilileta shilingi bilioni 319, Kahawa ilileta shilingi bilioni 204, Mkonge ulileta shilingi bilioni 111, Chai ilileta shilingi bilioni 72 na Karafuu ilileta shilingi bilioni 50. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo? Ukiangalia zile *top ten* unakutana na sekta ya kilimo kwenye uchumi wa nchi wetu. Pamoja na mchango wa kilimo kwenye uchumi wa nchi yetu, bado wakulima wadogo wadogo wana changamoto nyingi sana ambazo tunaiomba Serikali yetu itusaidie kwa haraka sana kuzitatau changamoto hizi. Changamoto ya kwanza ni ya pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru Serikali inatusaidia pembejeo kwenye kilimo cha mazao ya chakula, lakini ukifika kule kwangu Mbinga Mjini. Mbinga Mjini imegawanyika katika maeneo mawili. Kuna milimani ambako tunazalisha Kahawa na mabondeni tunalima mahindi, lakini wote hawa ni Watanzania, wote hawa wana mchango kwenye uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwa watu wa kule Mondeki, Miyangayanga, Luwaita, Utili kwenye milima kule, wale watu wanalima Kahawa, hawawezi kulima mahindi. Kutokuwapatia ruzuku ni kuwafanya wadumae na mwisho wa siku kilimo kitakuwa mzigo baada ya kilimo kuwa msaada kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni ukosefu wa centers za kufanya utafiti ambazo tunaweza tukajua eneo hili mbegu gani inaweza ikafaa, eneo hili aina gani ya mbolea inaweza ikafaa, mwisho wa siku tuweze kuleta kilimo chenye tija. Tukiulizana hapa sasa hivi ni maeneo gani, kuna hizi research centers ziko kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wa eneo husika, jibu utakalolipata litakuwa bado viko kwenye mchakato au vimekufa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ukosefu wa wataalamu, hawa tunaowaita Mabwana Shamba na mabwana mifugo. Tuzunguke kule vijijini tuulize lini Bwana Shamba alikwenda kumsaidia mkulima aweze kupanda kwa wakati, aweze kufanya palizi yake kwa wakati na kumpatia ile elimu ya kilimo bora. Utakuta kwenye sekta hii, sehemu ya wataalamu, Mabwana Shamba na Mabwana Mifugo hatujafanya vizuri sana. (Makofii)

Lingine ni kushuka kwa bei ya mazao. Mkulima analima kwa nguvu zake mwenyewe. Inapofika masuala ya bei, haitabiriki. Pembejeo ziko juu, gharama za uzalishaji ziko juu. Matatizo haya yote yanababisha kilimo kidumae na malengo tunayotaka ya kuajiri asilimia 75 ya Watanzania wote kutoka vijijini kwenye Sekta ya Kilimo, Mfugo na Uvvi itapata tatizo kubwa.

Changamoto nyingine inayotokana na hili eneo la kilimo ni kodi na tozo mbalimbali zinazowaumiza wakulima. Ukienda kwenye zao la kahawa, kodi na ushuru unaotozwa kwa wakulima unawatesa sana. Unakuta kuna kodi inaitwa *Tanzania Coffee Research Institute* ambayo ni 0.75, halafu kuna kodi nyingine inaitwa *Tanzania Coffee Development Fund* ambayo mkulima anatozwa 0.10 kwa kila kilo.

Lingine, kuna leseni ya TCB. Leseni ya TCB kabla ya mwaka juzi ilikuwa ni dola 24, sasa hivi imefika kuwa dola 24,000. Hivi mkulima wa kawaida atawezaje kwenda sambamba na

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

ongezeko hili la dola kwenye TCB? Hali inakuwa ngumu sana. Naiomba Serikali, ili kumwongezea Mheshimiwa Rais nguvu ya kuleta maendeleo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mapunda, muda umekwisha!

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Ahsante sana. Naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa session yetu ya asubuhi, lakini tangazo dogo tu niwakumbushe wale ambao hawajajaza fomu za kuchangia, kuna wengine wananiandikia vi-note. Wajaze zile fomu ili majina yaweze kuwekwa vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo!

**NAIBU SPIKA:** Nitataja Wajumbe watakaoanza huo mchana ili waweze kuwahi. Kuna Mheshimiwa Ally Hassan Kingi, Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe na Mheshimiwa Catherine Magige. Hawa ndio watakaoanza, kwa maana ya kwamba hiyo ndio *list* niliyonayo hapa kwa sasa.

Halafu wachangiaji wengine ni Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Salma Mwasa, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage. Wachangiaji wengine ni Mheshimiwa Kasuku Bilago, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Japhary Michael na Mheshimiwa Peter Msigwa.

Waheshimiwa Wabunge, siyo kwamba hawa ndio pekee watakaochangia mchana, nimetaja tutakaoanza nao. Kwa hiyo, *list* ya mchana pia italetwa.

Waheshimiwa Wajumbe, nadhani tumeelewana. Basi tunasitisha shughuli za Bunge mpaka jioni saa 10.00.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

**NDG. RAMADHAN I. ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali; Hoja ya kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoitao wakati wa ufunguzi wa Bunge la Kumi na Moja, tarehe 20 Novemba, 2015, majadiliano yanaendelea.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilitaja majina kadhaa wakati tukisitisha Bunge asubuhi. Naona tuko wachache lakini ngoja nitaje hawa kama wapo, Mheshimiwa Kasuku Bilago, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Selasini, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Mwasa, yupo? Haya nitaendelea kutaja majina kwa kadri tunavyoendelea. Basi tumsikie Mheshimiwa Kasuku Bilago.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mwongozo Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo Mheshimiwa Paresso.

### MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nasimama kwa mujibu wa kanuni ya 68(7). Naomba kupata Mwongozo, Mkutano wa Bunge huwa unarushwa *live* kupitia Televisheni ya Taifa (TBC), lakini leo baada ya Kipindi cha Maswali na Majibu na baada ya muda kidogo matangazo yakakatwa. Sasa tunaomba kupata sababu ni kwa nini matangazo haya hayarushwi *live* ili wananchi wafuatilie mjadala wa Bunge.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso, nimepata ujumbe wako nitatoa Mwongozo baadaye kidogo. Tuendelee na Mheshimiwa Kasuku Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Awali ya yote, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Buyungu kwa imani kubwa waliyonipa ya kuniamini, kuwawakilisha katika Jimbo la Buyungu na nina uhakika wamepata mwakilishi makini na sahihi.

Kabla sijaanza kuzungumzia vipengele kadhaa nitakavyovizungumzia, nataka niseme kwa ujumla wake, Hotuba ya Rais imesheheni matatizo ya Watanzania. Matatizo makubwa sana waliyonayo Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili nilidhani tungkuwa pamoja kama itawezekana, tuone namna ya kuondoa haya matatizo na matatizo yenyewe, hata Watanzania nawashangaa, kwa matatizo yote haya yaliyosababishwa na Chama cha Mapinduzi, wameendelea kukiamini na kukirudisha madarakani. Hapa ndipo ninapopata mashaka makubwa sana. Kwa matatizo lukuki yaliyoko ndani ya Hotuba ya Rais, Watanzania hawakutakiwa kukiamini Chama cha Mapinduzi na kukirudisha madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza maelezo yote hayo, nataka niulize style ya nchi hii sasa hivi tunayokwenda nayo ni ipi? Kuna style imeanza sasa hivi ya kuvamia. Mawaziri wetu wanavamia, wanaweza wakaja Mkoani hata Mkuu wa Mkoaa hajui, sasa ni style ipi tunayokwenda nayo. Maana sekta zote tukubaliane zianze kuvamia, walimu nao wawe wanavamia, ukiingia darasani ilikuwa Kiswahili uvamie na wewe ukafundishe somo lolote tu. Madaktari nao wavamie, yaani sijui ni style ipi ambayo haina work plan. Niwashauri Mawaziri, mtumie work plan, acheni kuvamia vamia. Aliyevamia mmoja tu yule alifanya tu vile msi-copy na ku-paste. (Kicheko)

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasuku naomba ukae. Katibu nadhani umekuwa umetunza muda wake kiasi gani umebakia. Kuhusu utaratibu endelea!

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumejielekeza hapa katika kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais na lengo kubwa hapa tumekuja kwa niaba ya wananchi na Mheshimiwa Rais aliainisha yale mambo ya msingi kwa Watanzania, matarajio yangu ni kwamba mzungumzaji aliyekuwa anazungumza sasa hivi ni bora angejikita kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais na sio kujadili mambo ya kisiasa. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasuku naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani ni ushauri tu, kwamba katika mjadala kila mtu ana namna yake ya kujadili, lakini kama unatoa ushauri kwa sababu wakati huu siyo wa Maswali na Majibu, kwamba utauliza swali halafu utajibowi. Kama una ushauri kuhusu hii hotuba unapoijadili ndiyo unatoa ushauri wako ili utakapomaliza unakaa na mwингine anaendelea, ukiuliza maswali hatutapata huo muda wa kuanza kujibizana humu ndani.

Kwa hiyo, unapojadili hii Hotuba; jadili sawa kwa namna yako, lakini jadili kwa namna ambayo unatoa ushauri ama unatoa yale yaliyomo kwenye hii hotuba na wewe unavyoona, lakini usiifanye kwa namna ya kuuliza maswali, kwa sababu hakuna mtu atakayekujibu hayo maswali. Ahsante, naomba uendelee kwa dakika zako zilizobaki.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba dakika zangu zitunzwe, lakini naomba kutoa tahadhari nisifundishwe namna ya kuchangia. Mimi ni Mwalimu, nina uzoefu mkubwa sana na hizi shughuli. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nilitaka nitoe tu angalizo hili, nadhani wamelichukua na watalifanya kazi. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais, suala la elimu bure limetajwa, lakini limeleta mkanganyiko kwa wananchi. Sasa hivi hali ya neno elimu bure, nafikiri tungetafuta utaratibu wa ku-define neno bure, kama linaonekana linaleta utata. Kwa mujibu wa maelezo yanavyotolewa na inavyotekelvezeka kule, hata Jimboni kwangu kule Buyungu hali ni ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, walioko shule za kutwa, wanaona hawajapata ule ubure unaotajwa kama bure. Walikuwa wanalipia chakula shule za kutwa, walikuwa wanachangia michango mbalimbali, chakula kimeendelea kubaki gharama kubwa, kuliko 20,000/= ilioondolewa, sasa wanatusumbua na sisi Wabunge, hivi kweli hii ni elimu bure? Kama tunasema neno elimu bure, tusiwe na double standard, shule zote ziwekwe elimu bure na kama ni chakula kitolewe kwa wote, hata shule za kutwa wapewe chakula na Serikali na wao ni Watanzania wanahitaji kula ili waweze kupata masomo vizuri darasani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kwenye elimu kuna matatizo lukuki, bado kuna wazabuni wanadai hawajalipwa, bado kuna walimu wanadai madai mbalimbali ambayo yameshaelezwa na baadhi ya Wabunge waliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nizungumzie habari za kilimo. Katika kilimo nitajikita kwenye pembejeo. Pembejeo ni tatizo kubwa tunaweza tukasema ni la Kitaifa. Pembejeo zinakuja wakati ambao huwezi kujua huu ni wakati wa kulima, ni wakati wa palizi, itafika wakati tutaleta mbolea ya kuvunia, kama itapatikana baadaye, lakini naona wakati wa kupanda DAP haipatikani. Unapofika wakati wa palizi ndio DAP inapatikana, yaani mbolea ya kupandia, inapatikana wakati wa palizi. Muda wa palizi unakwenda wakati mwингine, sijui mbolea ya kukuzia inakuja wakati gani?

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ilikuwa ni hivi, wakati wenyewe wa kuleta mbolea ile siyo wakati muafaka. Wananchi hawana fedha kabisa, ni miezi ambayo siyo ya mavuno, mbolea ikifika wakati wananchi wamevuna, watakuwa na uwezo wa kununua hiyo mbolea na itatumika muda muafaka majira ya kutumia mbolea yanapofika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, nataka nizungumzie, mtaniwia radhi natumia miwani wakati fulani, kodi kubwa kwenye mishahara ya wafanyakazi. Ifikie hatua, Watanzania, wananchi, wafanyakazi wanalamika kuhusu kodi kubwa. Hili bila kuliangalia, wafanyakazi tunawapa mkono wa kulia, tunachukua mkono wa kushoto. Lazima tufike mahali tuangalie nchi zinazotuzunguka, tusiwe kisiwa, nchi za wenzetu katika Afrika Mashariki hii wameshafikia *single digit*. Sisi hapa Tanzania kwenye Vyama vya Wafanyakazi walipoulizia habari ya *single digit* kwenye Kodi ya Mapato ya wafanyakazi wanaambiwa itafikiwa mwaka 2018, kuna tatizo lipi? Wafanyakazi hawana amani nalo wanalipwa mshahara, halafu unarudi Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyininge ni ya suala la kuimarisha Muungano. Nilitegemea Waheshimiwa Wabunge, suala la Zanzibar tungeliangalia wote kwa pamoja. Zanzibar siyo kwamba siyo sehemu yetu, lakini kunakotokea matatizo Zanzibar, tuyabebe wote kwa pamoja, tuyajadili kwa pamoja. Hapa imefikia hatua ukizungumzia habari ya Zanzibar, unaonekana wewe una matatizo. Hivi kati yetu hapa nani hakuwa kwenye uchaguzi? Baada ya uchaguzi matokeo yako yangefutwa, ungejisikiae? Wenzetu wamefanya chaguzi tano, zikafutwa nne, ikabaki moja ndiyo salama.

(Hapa kengele ya kwanza ililia)

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, niliibiwa muda mtakumbuka hilo. Kama uchaguzi mmoja ulikuwa salama, hizi nne zinakosaje usalama? Tuwe na huruma kwa wenzetu!

Mheshimiwa Naibu Spika, tufike mahali tukubaliane uchaguzi ulio huru na haki, siyo lazima ishinde CCM, muwe tayari kumeza pini, ifike hatua mseme hapa, ngoma *ime-tight*, tunakubaliana nayo, tunasonga mbele. Mataifa yanatucheka, tunachekwa na Mataifa kufuta uchaguzi wa nchi nzima mwanzo mwisho, halafu mnabakiza Wabunge wa Jamhuri wenyewe hawa ni halali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda haraka haraka, fedha za Jimbo zimezungumzwa kwenye hotuba hii, nashauri na niungane na Wabunge wengine, fedha hizi ziangularie ukubwa wa Jimbo. Kama hazitaangalia ukubwa wa Jimbo, zitakuwa haziwezi kukidhi mahitaji yaliyokusudiwa katika Jimbo. Kazi yangu siyo kulinganisha ukubwa wa Majimbo, lakini uhalisia wa Jimbo. Fedha zifanane na uhalisia wa ukubwa wa Jimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa afya, hali ni ngumu sana upande huo, bado wananchi hawana dawa kabisa, hali ni ngumu dawa hazipatikani. Niwaombe Mawaziri waliopo washughulikie hili wananchi waanze kupata dawa. Nakaa karibu na Burundi, kule Burundi hospitali zake ni nzuri kuliko pale kwetu Kakonko na Watanzania wanaougua wanakwenda kutibiwa Burundi badala ya kutibwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi Burundi, yaani nchi ndogo kama ile ambayo ina vita ya asubuhi, mchana na jioni, ina dawa nzuri, kwetu tuna amani na utulivu, lakini dawa hatuna! Naomba hili tuliangalie kabisa, Watanzania waanze kupata huduma za afya ndani ya nchi yao, inaweza ikatusaidia vilevile kurudisha imani kwa Serikali yao, pale ambapo inaanza kupotea. (Makofi)

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa  
muda wa mzungumzaji)

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia na suala la maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bilago tafadhali, naomba ukae muda wako umekwisha. Nilikuwa pia nimemtaja Mheshimiwa Selasini ameshafika? Tafadhali endelea!

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi, ingawa ndiyo nimeingia, lakini niseme kidogo, nisije nikakosa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Rais na kabla sijasema chochote kuhusu maudhui ya hotuba hii, nimefurahishwa na jambo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mmoja kati ya Wabunge wa upande huu tulioanzisha mageuzi miaka 20 plus iliyopita na tulipoanza kuna Mzee mmoja anaitwa Ndimara Tegambwage, aliandika kitabu kinachosema kwamba Upinzani Siyo Uadui.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hilo kwa sababu, baada ya kupitia hotuba ya Mheshimiwa Rais, nimegundua kwamba mambo mengi ambayo tumeyasema kwa muda mrefu Mheshimiwa Rais ameyazingatia katika hotuba yake na jambo hili linanifurahisha sana, linaonesha kwamba alah, kumbe sisi sote ni Watanzania na kwamba mawazo tunayoyatoa huku, siyo mawazo mabaya, ni mawazo ya kuisaidia nchi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukuke nafasi hii kuwaomba viongozi wengine, Mheshimiwa Nape yupo pale, Mheshimiwa Jenista na wengine, muige mfano wa Rais, siyo kwamba kila kinachosemwa upande huu ni kitu kibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, mimi nitachangia mambo matatu; la kwanza ni viwanda. Wazo la kufanya nchi yetu kuwa nchi ya viwanda ni wazo ambalo limechelewa sana. Mwalimu Nyerere alijitahidi, enzi za Mwalimu Nyerere tulikuwa na viwanda karibu katika kila zao, katika kila sekta, lakini bahati mbaya ndiyo hivyo viwanda vikachukuliwa, wengine wakavifisadi, wengine wakaviua na kadhalika. Sasa wazo hili, nadhani ndiyo wazo pekee ambalo litaisaidia nchi hii, kwa sababu ukiangalia sasa hivi ni bidhaa chache sana ambazo tunauza nje na kwa sababu hiyo, hata upatikanaji wa fedha za kigeni, unakuwa wa shida, ndiyo maana hali yetu ya uchumi inayumba mara kwa mara, dola inayumba mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri ambao ningependa kutoa, maana yake Mheshimiwa Rais amesema kwamba, atajitahidi kufanya nchi yetu iwe nchi ya viwanda, lakini ningefurahi zaidi kama mwelekeo ungeanza kuonekana, kwamba ni viwanda vipi tunaanza navyo ili watu waandaliiwe. Tusije tukaanzisha viwanda halifu matokeo yake tukauwa kilimo. Kama tunaanza viwanda ambavyo vitawasaidia watu wetu kujiardaa ili malighafi za hivi viwanda zitoke hapa hapa, litakuwa jambo bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu ukiangalia sasa hivi watu wanatoka vijijiini, vijana wanatoka vijijiini wanakuja mijini kuja kubangaiza na wanafanya hivyo kwa sababu kilimo sasa kinaanza kudharauliwa. Kijana anaona akifika mijini akishika soksi mbili, tatu akizitembeza, anarudi kijijiini anaonekana ni wa maana zaidi kuliko wale aliowaacha vijijiini. (Makofii)

## Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tuangalie vile viwanda ambavyo vitawafanya wakulima waweze kupata hamasa ya kuweza kuandaa malighafi kwa ajili ya viwanda vyenyewe ndiyo tuanze navyo. Nami nasema kwamba, Mheshimiwa Rais, pamoja na Serikali yake, kama mtajitahidi kuanza kufufua Viwanda vya Nguo, Viwanda vya Pamba, kwa sababu tunajua hapo nyuma jinsi Urafiki ilivyovuma, jinsi Mwatex ilivyovuma na viwanda vingine na mkifanya hivyo ni kwamba mnawahamasisha wakulima wa pamba kulima zaidi na vilevile kuweza kuona manufaa ya kilimo kwa sababu pamba yao itapata soko hapa hapa, pamoja na viwanda vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kwa sababu najua muda ni mchache, nisemee kuhusu maji. Utagundua na sidhani kama kuna Mbunge atasimama hapa bila kusemea suala la maji. Ningeomba sana suala la maji liwekewe kipaumbele kikubwa sana kwa sababu ndilo suala ambalo linawatesa watu wetu ukiacha na mambo mengine. Pale Jimboni kwangu shida ya maji ni kubwa kuliko ambavyo mtu unaweza ukaelezea na hasa inapokuja wakati wa kilimo. Ilisemwa hapa Bungeni kwamba sasa hivi mvua zinanyesha, lakini kwa experience ya pale Rombo maji yote yanakwenda nchini Kenya. Kule wameweka utaratibu wa kuyazuia. Matokeo yake kiangazi kikija, wale wa Kenya ndiyo wanatuuzia mboga na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishasimama hapa Bungeni mara nyingi nikiomba kwamba, jamani wale wanaohusika na Wizara ya Maji, sisi tuna makorongo mengi sana pale Rombo, tusaidieni tuweze kuzuia yale makorongo ambayo yanapitisha maji mengi sana wakati wa masika ili baadaye wakati wa kiangazi yatusaidie. Yatatengeneza hata ajira kwa vijana wetu, vijana watalima mbogamboga, vijana watalima kilimo cha msimu wa kiangazi na kwa sababu hiyo tutapunguza umaskini wa hali ya juu sana mionganoni mwa vijana wetu na tutatengeneza ajira mionganoni mwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Ziwa pale linaitwa Ziwa Chala, lile Ziwa niliomba hapa nikaambiwa yale ni maji ya Kimataifa, ni maji ya Kenya na Tanzania, kwa hiyo, utaratibu utafanyika ili tuweze kupata maji yale yatumike pia na kwa watu wangu pale Rombo. Sasa cha kushangaza watu wa Kenya wanatumia maji ya lile Ziwa, lakini sisi tunahangaika na uhaba wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana katika hii mipango mizuri ambayo Rais ameeleza kwenye kitabu chake itufikishe maeneo kama hayo, mahali ambapo tunayo maji, maji ambayo Mwenyezi Mungu ametupatia na maji ya Ziwa Chala ni maji ya Mlima Kilimanjaro. Theliji ile pale Kilimanjaro inapoyeyuka imetengeneza *underground rivers* ambazo zinakwenda mpaka pale Chala. Sasa wenzetu wa Kenya wanayatumia sisi tunabaki tunayaangalia. Kwa hiyo, wakati tunapoendelea kutengeneza sera zetu, mipango yetu kufuatana na hotuba hii ya Mheshimiwa Rais, naomba sana maeneo kama hayo yaangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize tu kwa kurudia ule wito wangu kwamba, jamani wote tunajenga nchi, nchi yetu hii ya Tanzania, kwa hiyo, mawazo ambayo yanatoka pande zote tuyapokee na tuyafanyie kazi, badala ya kupigana vijembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ulionipa. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Selasini. Tuendelee sasa na Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Ngonyani halifu baada ya huyo atafuata Mheshimiwa Haji Khatib Kai!

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na neno la shukrani. Shukrani hizi nazielekeza katika maeneo matatu. Nimeanza na neno la shukrani nikizingatia na Mheshimiwa Rais wetu alianza na neno la shukrani, kwa maana kwanza

## Nakala ya Mtando (Online Document)

kumshukuru Mwenyezi Mungu, nikiamini yeye ndiye muweza pekee na nafahamu ndugu zangu kutoka kule Jimbo la Mpanda Mjini sikuyawenza kwa nguvu zangu, ni kwa uwezo wake yeye Mwenyezi Mungu, kupitia kwa waja wake ametusaidia leo kuwepo mahali hapa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme nikiungana mkono na Mheshimiwa Rais, nitawashukuru wananchi hawa, lakini namna ya pekee ya kuwashukuru ni kuwafanya kazi na ndiyo maana hata Mheshimiwa alijikita katika hilo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani hizo naomba nizielekeze kwa wananchi wote kwa ujumla wao. Tutasema maneno mengi, lakini utulivu tuliouna wakati wa uchaguzi ni kwa sababu wananchi walikuwa tayari kushiriki uchaguzi ule na kutoa amani hiyo tunayoendelea kuiona hapa. Kwa hiyo, naomba na nikiamini mwananchi ndiye bosi wangu, ndiye Afisa wangu, hivyo, naendelea kuwashukuru wananchi hao. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru viongozi mbalimbali wa dini, lakini naomba nivishukuru vyombo mbalimbali nya ulinzi na usalama. Katika hili naomba niwe muwazi, nimeushuhudia weledi hasa kule kwangu Katavi, Askari Polisi na vyombo vingine vingine nya dola vimeshiriki kutufanya tushiriki uchaguzi salama. Kwa hiyo, nisipowashukuru nitakuwa siwatendei haki. Viongozi wa dini nafahamu kwa muda wote wamekuwa wakiliombea Taifa hili, nchi hii amani, kwa hiyo, nimesema ni vizuri nikiwashukuru hawa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu, amejikita kwenye ahadi na kuna neno moja zuri ambalo nimelipenda katika rejea yake, ametuambia, anaomba atutoe wasiwasi, tulivyoahidi tumeahidi na anaahidi kwamba ahadi ni deni. Hili ametukumbusha sisi Wabunge, lakini akawakumbusha wenzetu ambaa ni Madiwani, tumeahidi na ahadi ni deni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimkuta kiongozi mkubwa kama huyu analizungumza hili na hakuna kitu kingine ambacho nimeendelea siku zote kukifuatilia na nikasema huyu mtu kweli Mwenyezi Mungu kamsimamia, pale ambapo muda wote anamtanguliza Mwenyezi Mungu na anasema katika haya yote mema ya kufanya nchi hii tumuombee. Naamini, hakimu mwenye haki ni Mwenyezi Mungu, ndiye pakee atatusaidia kumlinda Mzee huyu ili atimize azma ya haya ambayo amekusudia kuwafanya Watanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwakumbushe ndugu zangu Wabunge, lakini niwakumbushe Madiwani tunayo kazi, tuna ahadi kwa watu wetu, wananchi kwa sasa hivi wameendelea kuonyesha utulivu. Nimekuwa nikisikiliza kupitia vyombo nya habari, ukipita katika makundi mbalimbali, wanatushauri wanasema hata mkibahatika kuwepo hapo jengoni, hebu toeni nafasi ya utulivu kwa Mzee huyu ili tuone ataifikisha wapi nchi yetu. Kwa hiyo, niwaombe sote tulipo hapa, tutoe nafasi, hata namna yetu ya kuchangia, kushiriki katika shughuli mbalimbali, tutoe nafasi ili tuone wapi tutaipeleka nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kulisema hilo, naomba nijikite katika suala la amani na utulivu. Tuna wajibu wa kuilinda amani, ni wajibu wetu mkubwa kuilinda amani na nashukuru katika hotuba yake Mheshimiwa Rais amezungumzia hatokuwa na simile kwa wale watakaochezea amani na utulivu wa nchi hii. Kwa hiyo, ili tuweze kujikita kwenye suala la viwanda, ambayo ni azma kubwa ya kutoa nchi hii kufikisha kwenye uchumi wa viwanda, bila amani na utulivu hatuwezi tukafika huko. Nilikuwa najaribu kuangalia usemi mmoja wa Kichina, lakini tafsiri yake ni ya Kiswahili unasema hivi; nikisikia nasahau, nikiona nakumbuka, nikitenda naelewa au nafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunasikia habari ya Mheshimiwa huyu kuhusu suala zima la kwamba hapa ni kazi tu, watu wakawa wanashahau, lakini baada ya kuona yale

## Nakala ya Mtando (Online Document)

anayoyafanya sasa hivi kuhakikisha mapato ya nchi hii yanapatikana na maeneo mengine watu wamekumbuka, ahaa, kumbe yale tuliyokuwa tunasikia ni sahihi, lakini kwa hili ambalo tunaendelea kuliona elimu bure ambayo ni matendo yametendeka sasa hivi, ndio tunaendelea kufahamu kwamba Mzee huyu anamaanisha na anatembea kwenye yale aliyokuwa akiyasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la elimu, nishukuru kwa sababu zifuatazo:-

Tunapo zungumzia habari ya elimu bure changamoto haziwezi kukosekana, huu ni mwanzo, tumeanza na hilo na changamoto ni kitu cha kufanya kazi. Siku zote ni muumini wa jambo moja, unapokuwa ni mtu wa kulalamika muda wote, wewe unakuwa ni sehemu ya tatizo, kwa hiyo naogopa kuwa sehemu ya tatizo, niwe sehemu ya kutatua tatizo. Kwa hiyo, changamoto tutakazoziona katika suala zima la elimu bure ambayo hiyo ni sehemu ya kuchangia hotuba ya baba huyu. Nasema kwamba tukiwa wawakilishi wa watu tutakuwa na wajibu wa kusema hapa, maana ukiwa na chai kama haina sukari utafanya zoezi la kuongeza sukari na kama sukari imezidi, unaweza ukaongeza hata maji, lakini tofauti na kutokuwa na chai kabisa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la huduma ya afya, nishukuru na niseme kwamba, kule ninapotoka Katavi eneo hili la huduma ya afya ni jambo muhimu. Watu wetu akinamama na watoto, wazee tuendelee kama alivyozungumziwa Mheshimiwa Rais kuangalia makundi hayo, kuangalia akinamama, watoto na wazee na ile sera yetu ya afya bure kwa makundi hayo tuendelee kuizingatia na naomba niendelee kumkumbusha Mzee huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la barabara, bila kuiunganisha nchi hii na ninashukuru hata kiongozi aliyejita aliongelea habari ya kuunganisha mikoa kwa mikoa, mikoa na maeneo mengine ya Wilaya kwa maana ya barabara kwa kiwango cha lami. Mimi ndugu yenu ninayetoka Katavi, mkoa amba leo hii tuna zaidi ya tani 3000 za mazao, natamani kuona mazao haya yakienda kwa Watanzania wengine waliopata uhaba wa chakula, lakini ili tuwafikishie ni kwa kuiunganisha eneo lile na barabara. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hapo niseme Mheshimiwa kwa nia yake njema na nashukuru aliniambia ndugu yangu Kapufi ukibahatiwa kuwa Mbunge, kanikumbushe katika haya. Naendelea kusema alilolisema kuhusu barabara ni jambo jema, aliyoyasema kuhusu maji ni mambo mema, aliyoyasema kuhusu afya ni mambo mema na wakati akiyafanya hayo akumbuke kule Katavi aliahidi suala hilo na ndio mkoa pekee uliobakia. Katavi, Kigoma na Tabora hatujaunganishwa kwa kiwango cha lami, tunatamani kuyaona maendeleo hayo na kushiriki uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kusema, unapokuwa na sehemu nyingine anavunja barabara kwa sababu ni nyembamba ili aipanue, mwagine hata hiyo nyembamba hana, hapo ni eneo la kufanya tafakari ya kina. Watu wa maeneo hayo wazalishaji wazuri eneo la utalii wa nchi hii tuna maeneo mazuri ya kuweza kufanya shughuli hizo za kitalii niendelee kumwomba Mzee huyu na kwa kuwa haya yote ameyaainisha katika hotuba yake kwamba, tutaangalia maeneo hayo ya utalii, tutaangalia masuala ya barabara na tutaangalia huduma za afya. Katika huduma za afya niendelee kumkumbusha Mzee huyu, tujikite katika vifaa tiba.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, najua kengele hiyo ni ya mwisho, nashukuru kwa kuniskiliza. (Makofii)

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tumsikilize Mheshimiwa Stephen Ngonyani, yupo!

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipo. Kwanza nianze kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Korogwe Vijijini kwa kuniamini na leo nipo hapa kwa mara ya pili Mungu awabariki sana, sitawaangusha, nitafanya kazi kwa jinsi walivyonituma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nataka nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano pamoja na Mawaziri, safari hii wametupa nguvu ya kuonesha kabisa kwamba safari hii hapa ni kazi tu. Naomba kazi hii isiishie mijini iende vijijini ikaangalie kero za wananchi.

Mimi nitajikita katika mambo matatu au manne makubwa. Sasa hivi Serikali ya Mheshimiwa Pombe Magufuli imeamua kufanya kazi, lakini naomba sana Serikali ihakikishe inamaliza kwanza zile ahadi za nyuma ambazo zilitolewa kwa wananchi. Kwa mfano, sasa hivi watu wana mpango wa kujenga Bandari ya Bagamoyo, wangeacha kwanza Bandari ya Bagamoyo wangezijenga Bandari za Tanga pamoja na Mtwara ili iwe kiegesho kikubwa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiyaafanya haya Watanzania watatuelewa vizuri sana. Hatuwezi kila siku kuwa tunaanzisha vitu halafu vinaishia njiani. Kwa mfano, suala la reli, reli ni kitu muhimu sana kwa Watanzania, lakini inaangaliwa sana reli ya kat, inaachwa reli ya kutoka Tanga kwenda Arusha kwenda Musoma. Huko pia kuna maeneo ambayo wananchi wanafanya biashara, wananchi wana mizigo wanataka kubeba, wananchi wanataka kuona na wao wanapanda treni kama wanavyopanda wenzetu wa kat. Hii Tanzania ni moja, Watanzania ni wamoja, wakati wakiwa nje tunakuwa tofauti, lakini tukiwa hapa ndani wote tunatetea haki za Watanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nataka tuzungumzie mambo ya viwanda. Sasa hivi tunasema kwamba Tanzania ya viwanda, lakini kuna viwanda vingi vimekufa hakuna mpango wa aina yoyote ambaa unaweza kuanzishwa naomba tusijenge viwanda vingine tuanze kwanza kuvifungua viwanda vya Mponde ambavyo vimfungwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawapati chai, chai hakuna mahali pa kuipeleka, Watanzania wamekosa kabisa kuamini. Naomba kwanza tuhakikishe tunawafungulia viwanda Watanzania, vile vilivyokuwa vimfungwa kule Tanga, kwa mfano, Kiwanda cha Chuma, Kiwanda cha Omo, Kiwanda cha Mbao na viwanda vingi mpaka Kiwanda cha Blanketi kimefungwa. Sasa leo tukisema tunataka kuanzisha viwanda, wakati vya zamani bado, naomba kwanza Serikali yangu Tukufu, naipenda sana na safari hii imetupa nguvu sisi Wabunge, tunafanya kazi kwa kujiamini, wahakikishe kwanza vile viwanda vya zamani vyote vinaamshwa na Watanzania wengi wanapata kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni suala la mama ntilie na vijana. Serikali ya Mheshimiwa Pombe Magufuli iliamua kwamba, mama ntilie na hawa wanaofanya biashara ndogo ndogo wasishikwe ushuru. Sasa hivi inashangaza sana, watu badala ya kushika ushuru mkubwa mkubwa katika maeneo, wanawakimbiza watu wa bodaboda na mama ntilie na wale akinamama ambaa wanaauza hata vitu vidogodogo, nyanya pia mtu analipa risiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye Jimbo langu aliwahakikishia Watanzania wanaoishi Korogwe kwamba ushuru mdogo mdogo utafutwa, lakini cha kushangaza watu wanauona huo ushuru mdogo mdogo wa kuwasumbua Watanzania wa hali ya chini.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali hii, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mchezaji wangu wa mpira, anajua kabisa kero hizo kwa sababu huko kote tulizunguka naye na hata kwenye Jimbo langu alifika kunifungulia shule. Naomba sasa wale wanaoshika ushuru mdogo mdogo waache, kwa sababu wakifanya hivyo na sisi Wabunge tuna nguvu sana ya kujenga hoja hapa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la barabara ni suala muhimu sana. Kuna barabara ambayo toka mwaka 2010, Serikali ya CCM tulisema kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami, naomba iangaliwe sana hii barabara ya kutoka Korogwe kuititia Bumbuli kwenda mpaka Soni ili iwe kwa kiwango cha lami. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile katika suala la maji, tusianzishe miradi mingine, kuna mradi mkubwa wa kutoka Kilimanjaro kuja mpaka Mkoa wa Tanga kuititia Kata ya Mkomazi na Tarafa ya Mombo. Naomba Waheshimiwa Mawaziri mliopo, ni majembe ambayo tunayaamini kabisa, safari hii hakuna tena lelemama ni kazi, naomba mradi ule umalizie ili Watanzania tuendelee kuipenda, maana sasa hivi Watanzania wote wanaipenda Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa nini? Kwa sababu ya Jembe Magufuli. Sasa kwa haya naomba pia tuhakikishe kwamba tunakamilisha bila tatizo la aina yoyote. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umeme ni muhimu sana. Mheshimiwa Profesa mwenzangu Muhongo umeshanahidi leo hapa, nimekuufata kwako umeniambia vile vijiji vyangu vyote vilivyokosa umeme, safari hii vinapata umeme vyote. Sasa isiishie tu katika mazungumzo yetu ya mimi na wewe, maana hapa tupo maprofesa wawili tu tuliohitimu kama wewe, naomba unikamilishie hilo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona niyaseme haya kwa sababu, leo hapa tumekuja kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Pombe Magufuli. Naamini kabisa Watanzania wanataka kuona Tanzania ile ya juzi siyo Tanzania ya kesho. Nikiongea mpaka kesho sitakuwa na lolote la maana la kuwasaidia ila ni kuimba Serikali yangu kwamba yale yote yaliyoahidiwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais, tuyatekeleze kwa kipindi ili mwaka 2020, tuteremke tu maana safari hii tumepata shida kweli kweli. Mungu awabariki sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Haji Khatib Kai!

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameweza kuniamsa salama siku ya leo nikiwa na afya tele na kuweza kutoa mchango wangu katika hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ambayo Rais John Pombe Magufuli akilihutubia Bunge na kulifungua, aliwajengea wananchi wa kawaada matumaini makubwa kwa kule kusema kila alipokuwa akizungumza kwamba anawaomba wananchi na kuwataka wamuunge mkono kwa kazi kubwa ambayo ataifanya ya kutumbua majipu ili nchi yetu iweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya game ilizunguka, majipu yaliyotumbuliwa yaliwagusa wananchi hawa kwa kuvunjiwa makazi yao, wananchi hawa wanyonge hawajui kwa kwenda hadi sasa, hawajui la kufanya na vilevile kusababisha maafa na kusababisha vifo kwa watu wengine. (Makofii)

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme kwamba Mheshimiwa Rais amewatelekeza wananchi ambao alisitisiza kila alipokuwa akizungumza kwa kutaka wamuunge mkono na kwa kutaka wamwamini kwa kazi kubwa ambayo amekusudia kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie hali ya kisasa Zanzibar. Wakati Rais John Pombe Magufuli siku ya tarehe 20/11/2015 akilifungua Bunge hili alimtanguliza Mungu mbele kwa kusema kwamba atautatua mgogoro wa Zanzibar kwa utulivu na amani. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kusema kwamba baada ya yote hayo, Mheshimiwa Rais kumtanguliza Mungu mbele na wakati Mheshimiwa Rais akienda kwenye maadhisho ya Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari, 2016 Mheshimiwa Rais alikwenda kutangaza kurudia Uchaguzi wa Zanzibar. Nimeamua kusema hili kwa sababu kiongozi yejote wa chini ki-protocol anapozungumza jambo mbele ya Kiongozi Mkuu, basi kauli ile inakuwa siyo ya kiongozi wa chini bali ni ya kiongozi wa juu. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar siku zote tumekuwa tukisikia kauli aina mbili ambazo zikitolewa na Chama cha Mapinduzi (CCM), kauli zinazosema kwamba Serikali ya Mapinduzi haiwezi kutolewa kwa makaratasi, hatutoi, hatutoi, hatutoi labda wapindue. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ya pili ambayo imekuwa ikitolewa na Chama cha Mapinduzi inasema kwamba Serikali ya Mapinduzi haiwezi kutolewa kwa kura, hilo wasahau. Masuala ya kujuliza ni kwamba, kwa nini Zanzibar iendelee kufanya chaguzi ikiwemo hiyo ya marudio. La pili, milioni ngapi zinatumika kugharamia chaguzi ambazo majibu yake yanajulikana? Nini tija ya kufanya hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, chaguzi ngapi zimefanyika huko nyuma ambazo zimekuwa zikilalamikiwa lakini hazijawahi kurudiwa? Seuze chaguzi huu wa mwaka huu ambao matatizo yake yamekuwa madogo na yangeweza kushughuhulikiwa kwa gherama ndogo sana. Yote haya ya kulazimisha kurudia uchaguzi ni kwa sababu ya watu wachache kwa maslahi yao binafsi. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashindwa kuelewa ni kwa nini Serikali ya CCM na viongozi wa CCM hawawezi kujifunza kwa yanayotokea duniani kama vile Somalia, Afghanistan, Misri, Libya na kwingineko. Raia wa nchi hizi hawakutaka kufikia hapa walipo, lakini walisababishwa kufikia hapa walipo na uongozi dhalimu wa nchi zao kama vile uongozi dhalimu wa CCM na viongozi wao ambao wamekusudia na wamepanga sasa kutupeleka ambako siko, kule Zanzibar.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma naomba ukae.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma naomba ukae.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya CCM na viongozi wa CCM wamekuwa wakituhulumu kule Zanzibar; mwaka 1995 walituhulumu, mwaka 2000 walituhulumu, mwaka 2010 walituhulumu na mwaka 2015 wanapanga kutuhulumu!

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kai, naomba ukae. Naomba uzime microphone.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu zimeweka wazi mambo ambayo hayaruhusiwi kufanywa humu Bungeni. Waheshimiwa Wabunge Kanuni ya 64(1)(d), inaongelea kutokutumia vibaya jina la Rais kwa dhihaka na (g) inasema hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wa hotuba ya Mheshimiwa Rais, naomba tujadili kwa heshima kwa sababu Kanuni zinatutaka hivyo, tusijaribu kutumia maneno yale ambayo yanaleta shida, kwa mfano, Mheshimiwa Kai anatumia maneno kama kutelekeza wananchi kwa maana kwamba Rais ametelekeza wananchi, siyo maneno mazuri kwa mujibu wa Kanuni hii. Hayo ni mambo ambayo hayaruhusiwi, kwa sababu ukisema kawatelekeza wananchi mwingine anaweza akaelewa tofauti, lakini pia haileti picha nzuri, kwa sababu hii Kanuni sisi wenyewe ndiyo tuliojiwekea na imetakaza. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye maneno mengine ambayo umeyatumia Mheshimiwa Kai, kama uongozi wa kidhalimu umetoa mifano mingi, nadhani utafute maneno ya kuyatumia ambayo yana staha, kwa sababu ukisema namna hiyo ni kama unatumia haya maneno ambayo hii kanuni imekataza. Tafadhali endelea kuchangia kwa dakika zako zilizobaki kwa kufuata kanuni zinavyosema. (Makofii)

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokuwa nakizungumza hapa ni hali ya kisiasa Zanzibar, kwa hivyo sioni sababu kusema kwamba kuzungumzia chaguzi zilizopita ili tujue nini tufanye.

Nilichokuwa nasema, Serikali hii ya CCM na viongozi wake ambao wamekuwa wakituonea, wakitudhulumu, siku zote haikubaliki. Serikali ya CCM na viongozi wake walituhulumu 1995, wakatuhulumu 2000, wakatuhulumu 2005, wakatuhulumu 2010, na 2015 mmepeanga kutuhulumu! Haikubaliki, inauma sana, Mheshimiwa Waziri mkuu inauma sana hii. (Makofii)

**MBUNGE FULANI:** Ushahidi.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. HAJI K. KAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimalizie kwa kusema, endapo suala la Zanzibar halitapatiwa ufumbuzi wa haraka, nchi inakokwenda siko. Tumevumilia Wazanzibar vyta kutosha vyta kutosha na sasa mazungumzo yanakwenda, mazungumzo mnatudanganya, mnamdhalilisha kiongozi wetu, mnampelika huku na kule, kumbe hamna nia njema na mazungumzo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kai, nadhani nimeshatoa maelezo, kwa sababu namna yako ya uchangiaji inavuruga utaratibu, ukisema hayo maneno ataamka Mbunge mwingine kwamba uthibitishe. Utautoa wapi uthibitisho, wakati matokeo unayoyataja yalikwishatoka na walioshinda walishatangazwa wakati huo.

Kwa hiyo, ndiyo maana nimetoa ushauri kwa nia njema kabisa, kwamba uongee mambo ambayo kanuni zinaruhusu. Mbunge mwingine atasimama atakwambia uthibitishe utakuwa huna uthibitisho; tafadhali malizia hizo dakika zilizobaki na uchangie kwa ustaarabu.

**MBUNGE FULANI:** Amemaliza bwana, anatupotezea muda huyo amemaliza bwana! Mbona unambembeleza!

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MBUNGE FULANI:** Amemaliza.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, hili limeonekana kwamba linagusa hisia za watu...

**MBUNGE FULANI:** Wewe mbishi.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Basi niseme tu kwamba kwa hapo nilipofikia, nasema ahsante.

### TAARIFA

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 64(a) kinakataza kwamba Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. Sasa kwa mujibu wa mchangiaji ameeleza kwamba walidhulumiwa, je, anaweza akaleta mbele ya Bunge ushahidi kwamba alidhulumiwa?

**WABUNGE FULANI:** Aaaa!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Tuendelee Mheshimiwa Joseph George Kakunda!

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kabla sijachangia naomba niwashukuru sana wananchi wa Sikonge kwa kuniamini kuwa Mbunge wao kwa mara ya kwanza. Naomba niwatoe wasi wasi, wasiwe na wasiwasi wowote hapa kazi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia katika hotuba, naomba nieleze kwamba nikiwa Mbunge nilifadhaika sana siku Mheshimiwa Rais alipotoa hotuba yake. Wakati Mheshimiwa Rais anaingia humu ndani, zilizuka fujo ambazo zilinifanya ninyong'onyee kwa muda, nikishangaa kwa sababu sikutegemea hadi wenzetu wakatoka wakisusia, hawakutaka kumsikiliza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini leo...

**NAIBU SPIKA:** Tafadhali, Mheshimiwa Kakunda naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani tipeane heshima inayostahili. Anapochangia mtu aliyeekaa upande wangu wa kushoto huwa upande wa kushoto upo kimya, anapochangia mtu kutoka upande mwingine kelele zinakuwa nyingi na majibizano, kila mtu atapewa nafasi ya kuchangia, atapewa fursa ya kujibu. Kwa hiyo, naomba tuheshimiane, mtu anapochangia apewe hiyo fursa tusipige kelele, tafadhali. (Makofi)

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Leo nimefarijika kuona badala ya kumsikiliza siku ile Mheshimiwa Rais, leo wenzetu wamesoma vizuri hotuba yake na wakisimama wanamsifu bila vurugu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ustaarabu huu uliooneshwa leo Watanzania wanauona na sisi Wabunge wote kwa ujumla naomba tuuzingatie ustaarabu huu siku zote, ili kama kuna hoja ijibiwe kwa hoja badala ya vurugu ambazo zinatufanya sisi wote tupoteze heshima yetu nje ya Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nije kwenye hotuba. Kiwango cha commitment kilichooneshwa na Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ni cha hali ya juu sana. Ni kiongozi

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

ambaye yuko tayari kwa kauli na vitendo kupambana na vikwazo vyote ambavyo kwa muda mrefu vimekua vikimsababishia Mtanzania kero nyingi katika juhudzi za kujikwamua kutoka kwenye umaskini. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, matumaini ya sasa ya Watanzania ikiwemo Wanasi Konge ni makubwa mno, kwamba, baada ya miaka 10 ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli akiwa Rais uwezekano wa kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ifikapo mwaka 2025 si wa kutilia shaka tena, kinachotakiwa kila mtu kutimiza wajibu wake. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Rais ya tarehe 20/11/2015 na utendaji wake wa Rais na Serikali yake hadi sasa, umeongeza matarajio ya wananchi kuhusu kufanikiwa katika mapambano dhidi ya rushwa na ujisadi, kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Serikali, kudhibiti matumizi, kuimarisha uadilifu, uaminifu na uzalendo na vyote hivi vinaashiria matokeo makubwa katika kupunguza umaskini. Ili tufanikiwe katika yote hayo, yale majipu ambayo Mheshimiwa Rais aliyahidi kuyatumbua, majipu makubwa, majipu madogo na hata vijipu uchungu, vyote lazima vitumbuliwe bila kuona huruma. Mheshimiwa Rais ameahidi na tayari utekelezaji unaendelea, tunamshukuru sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Sikunge walifurahishwa sana na hotuba ya Rais na wamekaa mkao wa hapa kazi tu, wanatimiza majukumu yao hususani katika sekta ya kilimo kwa kulima sana mashamba ya tumbaku na mazao ya chakula, kutengeneza mizinga kwa ajili ya asali na nta na kutumia fursa nyingine zozote zilizopo kupambana na umaskini. Wanakumbuka ahadi nzuri zinazojenga matumaini za Mheshimiwa Rais kwamba Serikali itawaboreshea zaidi mazingira ya kufaidika na jasho lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo ningependa kukumbusha kwa sababu yako katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, la kwanza, linalohusu eneo langu, kuondoa kero kwenye zao la tumbaku kwa kumwezesha mkulima apate pembejeo kwa urahisi na kwa muda muafaka na kwa bei nafuu kwa kutumia mfumo rahisi ambapo mkulima kupitia Chama chake cha Msingi, akae kitako na mnunuzi ili waingie mktaba wa mnunuzi kukopeshwa pembejeo au pembejeo zitolewe kwa mkulima wakati wa msimu wa malipo kabla kilimo hakijaanza. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mfumo wa malipo uboreshwewe kuondoa malipo kuchelewa kwa zaidi ya miezi mitatu na Serikali imlinde mkulima asiibiwe wakati wa kubadilisha viwango vya fedha kutoka kwenye dola ya Kimarekani kwenda kwenye shilingi ya Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kilimo kuna mambo mengi sana ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi. Watu wa Ushirika wanahitaji kuwasaidia wakulima katika maeneo mengi, COASCO ambao ni auditors wa ushirika ni tatizo kubwa, wamekuwa siyo wa kweli, ni bora tu kuwaondoa ili mfumo wa ukaguzi ubaki chini ya ukaguzi wa ndani wa Halmashauri na CAG, hili litatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mengi mno kwenye kilimo yatazungumzwa na wengine, naomba wakulima waonewe huruma, wasaidiwe na Serikali pamoja na wadau kuondokana na adha wanazipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni kuboresha uhusiano kati ya wananchi na maeneo ya hifadhi, kwa mfano, mfugaji wa nyuki ni rafiki mkubwa sana wa misitu kwa sababu yeye anategemea kuweka mizinga yake kwenye misitu, kwa nini mfuga nyuki aonekane adui kwenye hifadhi eti tu kwa sababu tu anatumia mizinga wa gome la mti! Kwa nini Serikali isitoe elimu na huu ni ushauri kwa wafuga nyuki, ili watumie mizinga

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

ya kisasa itakayofanya hatimaye wawe na uhuru wa kuingia hifadhini kwa sababu watakuwa wamesajiliwa, hata wavuvi wadogo wadogo nao wanahitaji kusaidiwa kwa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda kuzungumzia kama kukumbusha kwa sababu liko kwenye hotuba, ni miundombinu. Barabara za lami na sisi tunahitaji kuunganishwa na Mikoa mingine kama Tabora - Katavi, Tabora - Mbeya - Singida, Tabora - Kigoma, kuboresha reli ya kat, miradi ya umeme vijiji na mitandao ya simu. Wilaya yangu ya Sikunge karibu 70% ya maeneo ya makazi hayajaunganishwa na mitandao ya simu. Ni muhimu sana kwenye awamu hii suala la mtandao lishughulikiwe kwa jicho kamilifu. Naomba maeneo yote yaliyo nyuma kwa miundombinu yapewe kipaumbele na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Serikali iendelee kuwekeza kwenye elimu. Katika Wilaya yangu kuna maeneo 49 ambayo yanahitaji shule mpya kabisa za msingi. Katika maeneo 19 wananchi wamejenga madarasa, Halmashauri haina fedha za kukamilisha, kwa hiyo, Serikali Kuu bado tunaomba iendelee kuwekeza kwenye elimu ya msingi, siyo kwamba MMEM ilikwisha, basi hakuna uwekezaji mpya unao endelea, tunaomba tuendelee kuwekeza kwenye elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye afya tuna upungufu mkubwa sana wa zahanati, watumishi na dawa, vyote viendelee kuwa katika mipango ya Serikali. Kwenye maji tuna matumaini makubwa na mradi wa Ziwa Victoria, tunaomba ukamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naomba nimalizie kwa kusitiza kuhusu barabara ya lami kutoka Tabora-Ipole-Mpanda. Tunaomba fidia ilipwe mapema, barabara ijengwe mapema kuondoa adha wanayoipata wananchi amabo ni watumiaji wa barabara hiyo. Design yake ifanyiwe mapitio ili tuta la barabara ya lami liwe juu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda muda wako umekwisha.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia, yaongezwe madaraja na makalvati...

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae tafadhali...

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** ...ili barabara itakayojengwa iwe ya kudumu. Naomba kuwasilisha, ahsante sana. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa ngoja nisome wachache watakaofuatia. Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan King, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwambaliaswa, halafu Mheshimiwa Cecilia Paresso. Mheshimiwa Munde Abdallah!

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kuwapongeza Mawaziri wote, Mawaziri wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya, wasitishwe na watu wanaowaambia wanavamia vamia. Wafanye kazi kwa kujiamini, ni Serikali yao, wawatumikie Watanzania kama Mheshimiwa Rais John Pombe alivyowaaamini kuwapa Uwaziri huo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kidogo kuhusu uchaguzi wa Zanzibar tarehe imetangazwa. Niwaombe Wazanzibari wote wasubiri siku ya uchaguzi iliyotangazwa wakapige kura. Acheni kuwatisha Watanzania, acheni kuwatisha wananchi na kuwajaza jazba ambazo

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

hazina msingi wowote na baadaye mtatuhatarishia amani ya nchi yetu, tunaomba sana. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuipongeza hotuba ya Mheshimiwa Rais, kwa kweli hotuba ya Mheshimiwa Rais imesheheni mikakati ya kuijenga Tanzania mpya, imesheheni mikakati ya kuijenga Serikali ya Awamu ya Tano. Nampongeza sana Rais John Pombe Magufuli kwa hotuba yake nzuri kabisa. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisite kusema tu, kwa kweli Mheshimiwa Magufuli amewashangaza Watanzania, kwa muda mfupi tu ameanza kutekeleza ahadi zake alizozitoa Novemba hapa Bungeni. Ni vyepesi sana kukosoa na kulaumu, lakini kwa muda alioanza kutekeleza ahadi, ahadi zenyewe ni kubwa sana, zinahitaji utaalamu, zinahitaji pesa, ameanza kuzitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu amesema kwamba, mambo elimu bure ni *double standard*, siyo kweli, mwanzo ni mgumu. Mheshimiwa Simbachawene ametuambia, wamepata hesabu vibaya ya wanafunzi, lakini wanaamini watakwenda vizuri huko mbele. Tuwatakie kila la heri kwenye mipango yenu, tuwatie moyo, tumsaidie Rais wetu, tuwasaidie Mawaziri kuhakikisha Watanzania wanapata huduma alizozisema Rais wetu. Tunawatakieni kila la heri na Mwenyezi Mungu atawasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongee kidogo kuhusu maji. Niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, ilituahidi maji ya Ziwa Victoria watu wa Tabora, iko kazini inafanya kazi vizuri na imeahidi kuanzia mwezi wa sita itaanza kukarabati maji kutoka Ziwa Victoria kuleta Tabora, tutafaidika sana. Nzega mpaka Tabora Manispaa vijiji 86 vitapitiwa, vitapata maji ya Ziwa Victoria. Niiombe Serikali yangu, iende na *action plan* yake isije katikati ikakatiza. Tunaambiwa kufika 2019, Tabora tutapata maji ya Ziwa Victoria. Naiomba sana Serikali ya Awamu ya Tano ambayo tuniamini, Serikali ya hapa kazi tu, 2019 itupatia maji ya Ziwa Victoria. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Tabora kwenye maji ya Igombe, tulikuwa na shida ya pampu, tulikuwa na shida ya machujio, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshatuletea sasa na tunategemea kupata lita milioni 30 za maji badala ya lita milioni ishirini nne ambazo tunazihitaji. Tunaipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri inayoifanya na tunaomba wananchi wa Mkoo wa Tabora mwendelee kutuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi kati hapa maji yalikatika tulipigiwa simu kama Wabunge, lakini tatizo kubwa ni umeme, umeme kwa kweli Tabora umekuwa na mgao mkubwa sana, lakini niwaombe wananchi wa Tabora mtulie. Tumepata mwarobaini wa umeme ambae ni Profesa Muhongo. Profesa Muhongo yuko kazini, ameingia juzi, atafanya kazi, tunamwamini sana na tunaamini baada ya muda mgao huu utapotea. Tunamwamini na tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu afanye kazi yake kama tulivyomzoea. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara, kuna kilometra 80 ambazo tunaziombea lami, Mheshimiwa Rais ametuahidi kutuvekea lami. Tunamwomba Waziri husika aiwekee lami hiyo katika hizo kilometra 80. Sasa hivi barabara ya Itigi-Tabora hakuna mawasiliano, imekatika, tunaomba pesa za dharura, magari yamekwama pale, watu wanazunguka Singida, hali ni mbaya, nauji ni kubwa, watu wanashindwa kusafiri kupeleka wagonjwa wao na kuwashudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali, namwomba Waziri wa Ujenzi, tunaomba pesa ya dharura, tutengeneze madaraja hayo yaliyokatika Itigi-Tabora na pia tunaomba ufuatilie hiyo lami ya kilometra 80. (Makofij)

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, naongelea sasa suala la zima la reli. Hakuna Mtanzania wala Mbunge asijejua reli ni uchumi, reli inaleta maendeleo, reli inapunguza bei ya bidhaa. Tunashangaa kwa nini kila tukipanga masuala ya reli yanaishia njani.

Nashindwa kuelewa, naiomba sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, ihakikishe tunaboresha reli, ihakikishe reli hii inakuwa kama ni kitega uchumi cha Tanzania. Tukiboresha reli tutasafirisha mizigo ya Congo, Rwanda na Burundi. Nashangaa tatizo ni nini? Tunapata habari za mitaani kwamba kuna watu wenyewe malori wanatufanyia vitu fulani kiasi kwamba reli yetu isiendelee. Naomba sana kama hilo suala lipo basi liangaliwe na lichukuliwe hatua. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vitu vinavyoudhi sana kwenye suala zima la reli. Reli ni mbovu kwa muda mrefu, matengenezo yaliyofanyika ni Dodoma mpaka Igulula tu, lakini Kaliua-Mpanda hajatengenezwa, Tabora-Mwanza, Tabora-Kigoma, Igulula-Tabora reli hii hajatengenezwa. Kuna kilometra 35 kutoka Igulula kwenda Tabora Manispaa, hali ni mbaya sana, tunaiomba sana Serikali iangalie suala zima la reli. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye reli kuna majipu ya kutumbuliwa, hii ndiyo kazi ya Mheshimiwa Magufuli na Mawaziri wake. Tunaomba sana, kuna watu wamepewa miradi ya kukarabati reli. Kwa mfano, kuna mradi wa kukarabati reli kuanzia Kaliua-Mpanda, kuna watu wapo pale wanaikarabati hii reli, lakini reli hii toka imeanza kurabatiwa na watu wanaojiita ni Wahandisi waliostaafu, wana Kampuni yao inaitwa ARN, wanaikarabati bila kokoto bila chochote na mabehewa yanaendelea kuanguka na hakuna chochote kinachokarabatika. Tunaomba sana hili ni jipu na Serikali yangu sasa hivi ina mpango mzima wa kutatua matatizo haya basi ikafanye. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi wa kukarabati reli ya Godegode. Godegode pale kuna watu wanakarabati reli kila mwaka, lakini ndiyo kuna ajali kila mwaka za treni, kwa hiyo, nashindwa kuelewa watu wanalipwa pesa za nini wakati ajali zinaendelea. Kuna Wamalaysia walikuja kututengenezea injini zetu, injini zetu za muda mrefu zilikuwa mbovu, wametutengenezea injini, ni jambo jema, tunawashukuru kwa kututengenezea injini zetu, lakini kinachonishangaza, tuna mafundi wa railway, lakini bado hawaa Wamalaysia wanakuja kila mwezi eti kufanya service za zile injini. Kwa nini service hizi zisifanywe na mafundi wetu wa railway ambao wanalipwa mishahara na Serikali ya Chama cha Mapinduzi? Leo Wamalaysia wanakuja kufanya service kila mwezi, hili ni jipu Mheshimiwa Waziri tunakuomba sana uliangalie.

Kuna Injini 9010 mpya imenunuliwa kwa mamilioni ya shilingi. Juzi tu imeanguka Zuzu kwa sababu reli ni mbovu. Naumia sana kukwambia kwamba katika mabehewa mapya yaliyonunuliwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa gharama kubwa, mabehewa 70 yameshaanguka katika mapya na yako porini mpaka leo hayajanyanyuliwa. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri afuatilie mabehewa haya mapya yaliyoanguka huko porini na yarudishwe, yakarabatiwe ili yaendelee kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naongelea suala zima la wafanyakazi, wafanyakazi hawa wanakatwa mishahara yao ya kwenda kwenye Mifuko ya Jamii mfano NSSF, lakini wanakatwa kupelekwa kwenye SACCOS zao, wanakatwa wale waliokopa NMB. Hata hivyo, makato haya hayapelekwi NSSF, hayapelekwi kwenye SACCOS zao, tunashindwa kuelewa pesa hizi zimekatwa kwenye mishahara yao zinakwenda wapi. Naomba sana Serikali ifuatilie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna afisa amezuka anaitwa afisa wa kumsindikiza dereva, afisa huyu anapanda pamoja na dereva wa treni, analipwa laki moja na nusu kwa trip, dereva halipwi hata senti tano, eti yeye anaangalia treni isikimbie. Treni isikimbie wakati tuna vituo?

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, inajulikana kutoka Dodoma mpaka Zuzu ni dakika fulani, akiwahi ataulizwa? Kwa nini awekwe mtu ambaye analipiwa pesa nydingi? Kwa hiyo, huu ni mpango wa wakubwa, tunaomba ukomeshwe mara moja na pesa hizi walipwe madereva. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumezuka utaratibu ambao siuungi mkono, anayekwenda kukata tiketi ya kuondokea treni anaambiwa aende na kitambulisho. Sisi wote hapa asilimia kubwa tumetoka vijijini, tunajua ndugu zetu wa vijijini hawana utaratibu wa kutembea na vitambulisho. Unakuta mtu amemleta stesheni moja ya Kintinku siku moja, anaumwa, wanamkatalia kumpa tiketi eti hana kitambulisho au anaambiwa aende na picha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine nitaandika kwa maandishi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde, muda wako umekwisha.

**MHE. MONDE T. ABDALLAH:** Ahsante sana. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Sasa tumsikie Mheshimiwa Ali Hassan Kingi!

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ametujaalia uhai na kutupa afya tukahudhuria hapa kutekeleza wajibu wetu huu ambao tumeuomba kwa wananchi.

Pili nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Jang'ombe kwa kunichagua kwa kura nydingi na kwa kumchagua Rais Dkt. Magufuli kwa kura nydingi na hatimaye leo tumepata fursa hii ya kusimama hapa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kwako, kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia hotuba ya Rais aliyoitoa wakati akilihutubia Bunge siku ya ufunguzi wake.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kufanya baadhi ya maeneo ambayo tayari ameshayafanya kazi baada ya kuhidi kwa kipindi kifupi sana. Hii tayari tumeona jinsi alivyokuwa na nia ya dhati ya kuifikisha Tanzania hapa ilipo. Hii imeonyesha kwamba nia yake ataipeleka Tanzania pale tunapotaka. Maana tukichukulia hotuba tutapata ushahidi wa kutosha kwamba hivi sasa maeneo mengi yameshafanyiwa kazi na tumeyaona. Ni kweli hapa kazi tu, maneno na fitina baadaye. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, sasa nimsifu Rais wangu, huyu ni muungwana. Kuna usemi wa Kiswahili unasema kwamba ada ya mja hunena, muungwana ni vitendo, tenda watu wataona, majisifu weka kando. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais baada ya kuapishwa aliahidi katika ukurasa wa 10 wa kitabu cha hotuba, kwamba atashughulikia ule mgogoro watu wanaouita wa Zanzibar. Kwa hiyo, alifanya hivyo, tumeshuhudia sote, alimwita Makamu wa Pili wa Rais, Rais wa Zanzibar, Makamu wa Kwanza wa Rais ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Chama cha CUF, akaenda akazungumza nao na hatimaye matokeo tumeyaona kwamba Tume ya Uchaguzi imeshatangaza tarehe ya uchaguzi, nayo ni tarehe 20 Machi, 2016. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, napenda kulizungumza hili kwa sababu inawezekana kuna watu wakawa wanakosa njia za kuzungumza, wakafkiria kwamba Zanzibar kuna mzozo kiasi

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

ambacho kwamba hakuna amani na usalama, kitu hicho siyo kweli. Ndugu zangu tufahamishane kabisa hapa, Zanzibar kuna amani na Tume ya Uchaguzi wa Zanzibar ndiyo yenyé mamlaka ya kufanya uchaguzi na kutoa matangazo ya uchaguzi. Hao waliosema kwamba aliyeshindha atangazwe, atangazwe nani? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, matangazo yako mengi, kuna matangazo ya vifo yatatangazwa yote, lakini suala la kutangaza matokeo ya uchaguzi liko chini ya Tume, kifungu cha 42(1) mpaka (5), hakuna mwininge. Sasa katika suala hili la amani na mgogoro wa Zanzibar, Mheshimiwa Rais amelishughulikia vizuri sana na kwa sababu anafahamu yale mamlaka yaliyokuwepo ndani ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu walikuwa wakijinadi kwamba wanataka mamlaka kamili, leo wanakimbilia Marekani, wanakwenda Uingereza, wanakwenda kwa Papa, sasa hapo mamlaka hayo kamili ya ndani unayakataa mwenyewe. Wewe umetaka upate mamlaka kamili, basi tumia Tume yako ambayo imepewa mamlaka kamili. Kwa hiyo, Tume ya Uchaguzi wa Zanzibar ina mamlaka kamili kwa mujibu wa Ibara ya 104 ya Katiba ya Tanzania na pia kwa mujibu wa Ibara ya 119 ya Katiba ya Zanzibar, hilo limeelezwa wazi na halina utata wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuhusiana na habari hiyo ya matangazo nani anagombea Urais, Mwenyezi Mungu ndiyo anaamua nani awe Rais, hatuwezi kuamua hapa. "Qul-allahumma maalika'lmulki tuuti-lmulka mantashaa'u watanzi'u-lmulka mimman tashaa'u." Mungu yeye ndiye anayetoa ufalme, hakukupa Mungu huwezi kuupata kokote; sema, toka mapovu, zunguka, hutoweza kupata chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mshairi mmoja anasema, kutapatapa haachi mfa maji baharini, ashika kila mahali aokoke maskini, kafa angali mbichi, mfa maji buriani. (Kicheko)

Sasa ndiyo maana watu wanashika kule na huku wapate hayo mambo. Watu labda hawaelewi, kwa nini Tume ya Uchaguzi ilifuta matokeo ya uchaguzi au ilifuta uchaguzi na matokeo yake hawajui. Kwanza yale ni mamlaka ya Tume, hakuna ye yote wa kuingilia Tume, ile ni Tume Huru, mambo yametangazwa wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataa mfano mmoja, mnawenza mkalia nyinyi. Kura ambazo zimepigwa Zanzibar, nyingine zimepigwa za watu waliokufa. Watu wote wanaelewa kwamba ilitokea ajali ya MV. Spice, watu zaidi ya 6,000 lakini baadhi ya waliokufa mle wamepigwa kura zao, sasa huu ni ukiukwaji kwa mujibu wa Tume na Tume ndiyo imetoe takwimu hizo. Sasa wako watu hata vitambulisho hawana...

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Hata vitambulisho hawajachukua, lakini kura zao zimepigwa, katazameni katika taarifa ya Tume.

### TAARIFA

**SPIKA:** Mheshimiwa King naomba ukae. Taarifa iko wapi?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Hoja iliyoko mezani ni kuijadili Hotuba ya Rais, msemaji anayezungumza anatuambia mambo ya Tume ya Zanzibar, tunajadili hotuba ya Rais, anahama hoja.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Kaa chini!

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa King naomba uendelee.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Muda wangu uniongezee.

**MBUNGE FULANI:** Hapana Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Hapo hapo ndipo aliposema Rais mzozo na ndipo hapo hapo walipojadili watu na sisi tunajadili hapo hapo. Kwa hiyo, Tume ndiyo yenyenye mamlaka kamili, watu amba...

**NAIBU SPIKA:** Nimempa nafasi Mheshimiwa King amalizie, Mheshimiwa Bobali una nafasi yako ya kuchangia, utachangia.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bobali, naomba ukae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza muda wangu uulinde. Sasa wamepigishwa kura maiti, sasa hawa wanakaa wapi? Leo mnasema kama uchaguzi ule halali, hawa watu mnaweza kuturejeshea, tukawaona? Kule kwetu kuna kitu kinaitwa giningi au wamewekwa giningi? (Makofii/Vigelegele)

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa anasema uongo, Mheshimiwa anasema uongo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, naomba ukae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiki ndicho kilichotokea, kama hamjui, mnashabikia mnacheza ngoma si yenu, huo ndio ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, napenda kuipongeza Hotuba hii ya Rais na napenda Rais aendeleee kutufanya mambo mazuri. Miiongoni mwa mambo mazuri katika Mfuko wa Jimbo, Rais ameahidi kwamba atautoa mapema na haraka iwezekanavyo. Kwa hiyo, tunasubiri ili tuweze kwenda kufanya maendeleo yetu. Ombi letu katika Mfuko huu wa Jimbo uwe unawiana kwa thamani ya sasa hivi kwa sababu ulifanyiwa thamani muda wa nyuma kidogo, kwa hiyo, uende na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo tunamsitiza Mheshimiwa Rais, kwa sababu tunafahamu yeye ni mzee wa hapa kazi tu, ni kwamba katika mchakato huu wa Katiba Mpya, amesema amepokea kiporo, kwa kuwa ni kiporo kipashwe moto tu, halafu tuendeleee, kwa sababu mchakato wa Katiba ulikuwa umeshafikia mahali pake, tuanzie pale mahali ambapo tuliamachia ili tumalize.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine katika ukusanyaji wa mapato. Tumeona jitihada zake Mheshimiwa Rais, lakini pia, tunapenda ashirikiane na taasisi au zile Professional Bodies ambazo wamo wadau wa ukusanyaji wa mapato. Mle mna Wahasibu, mna na ma-auditors wa Kampuni, ili kusifanyike udanganyifu katika ukusanyaji wa mapato na mapato yasivuje. Kwa hiyo, hii tunasitiza sana aweze kutumia Sheria, hebu wapewe hizi Professional Bodies zipewe meno.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote haya, tunapenda Rais awe na mashirikiano mazuri na wafanyabiashara au Serikali iwe na mashirikiano mazuri, lakini siyo kwa ajili ya kufanya kodi isikusanywe. Kwa hiyo, wakiwa na mashirikiano hayo, Serikali itaweza kukusanya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika suala la ulinzi na usalama; katika suala la ulinzi na usalama, nafikiri najilipalipa dakika zangu hapa! Katika suala la ulinzi na usalama hili ni jambo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kingi, muda wako uliingiliwa hapo katikati, dakika moja ukae!

**MHE. ALI HASSAN KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Bado dakika moja!

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Vyombo vyta Ulinzi na Usalama hili suala liangaliwe, kwa sababu katika baadhi ya maeneo, watu wanavikebehi vyombo vyta ulinzi na usalama. Yako maeneo ambayo vyombo vyta ulinzi na usalama havifanyi kazi vizuri kwa sababu ya nature ya maeneo yale.

Kwa hiyo, hili Mheshimiwa Rais alichukulie hatua, alisema ataboresha makazi kwa wana ulinzi wetu, watu wa ulinzi na usalama. Kwa hiyo, afanye makazi yapatikane ili waepukane na kukaa kwenye nyumba za kupanga katika maeneo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sehemu moja siitaji, alikatwa kichwa Askari akitoka kweke kwenda kazini. Kama watakuwa wanapewa makazi, basi Askari hawataweza kufanyiwa mambo haya ambayo yako kinyume na Sheria. Ahsante. (Makofij)

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa!

Waheshimiwa Wabunge, niliwakumbusha wakati Mheshimiwa Kai akichangia kwamba, Kanuni ya 64(1)(a) ina mambo inayokataza. Inasema; "Bila kuathiri masharti ya Kanuni ndogo ya, bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:-

(a) Hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli."

Waheshimiwa Wabunge, naomba tunavyojadili hii Hotuba ya Mheshimiwa Rais, tusiwekeane mazingira ya mtu kuanza kuambiwa aende akalete taarifa, ili tuanze kuthibitisha hayo ambayo ameyasema. Nadhani haya nimeyasema jumla wakati Mheshimiwa Kai anachangia, wote tuyazingatie wakati tunaendelea kuchangia.

Nitawataja wanaofuata, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Pareso, Mheshimiwa Adadi Rajabu, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe.

Mheshimiwa Victor Mwambalaswa!

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hoja iliyo mbele yetu.

Kwanza, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Lupa waliokichagua chama changu kwa kura nyingi sana, kuanzia Rais, Mbunge na Madiwani, kura nyingi sana nawashukuru sana. (Makofij)

## Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema na kama alivyosema Mheshimiwa Rais, hatutawaangusha. Uchaguzi umekwisha, sasa iliyobaki ni kufanya kazi, ni kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ni kutekeleza ahadi ambazo wagombea tuliahidi kwenye majukwaa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimboni kwangu kuna genge limeibuka linaeneza uongo kwamba barabara ya lami kutoka Chunya kwenda Makongolosi alioahidi Mheshimiwa Rais haitajengwa! Eti haitajengwa kwa sababu kuna watu wamekula hela na hao watu wamekimbia nje ya nchi!

Mheshimiwa Naibu Spika, wale ni waongo, ni watu ambaa kwenye uchaguzi walishiriki na walikuwa wanatamba kwamba wangeshinda kwa kishindo! Wameshindwa kwa kishindo! Wanashindwa pa kutokea, wanaeneza uongo! Hilo wananchi wa Lupa ni jipu, mtajua namna ya kulitumbua wakati ukifika. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia Hotuba ya Mheshimiwa Rais nalinganisha sana na maneno, yaani nikiangalia hotuba yake na matendo yake, nalinganisha sana na maneno na matendo ya Yohana Mbatizaji zaidi ya miaka 2000 iliyopita. Kwa ruhusa yako, naomba nisome paragraph moja aliyoosema Yohana Mbatizaji kwenye Injili ya Luka 3:7-14. Siyo maneno yangu haya, maneno ya Yohana Mbatizaji:

"Basi aliwaambia makutano ya wale waliomwendea ili awabatize. Enyi wazao wa nyoka, ni nani aliyeaonya ninyi kuikimbia hasira itakayokuja? Basi toeni matunda yapatanayo na toba, wala msianze kusema miyoni mwenu tunaye baba, ndiye Ibrahim, kwa maana nawaambia kwamba katika mawe haya Mungu aweza kumuinulia Ibrahim watoto. Na sasa hivi shoka limekwisha kuwekwa penye mashina ya miti na kila mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni.

Makutano wakamuuliza, tufanye nini basi? Akawajibu akiwaambia, mwenye kanzu mbili na ampe asie na kanzu na mwenye vyakula na afanye vivyo hivyo. Watoza ushuru nao wakaja kubatizwa wakamuuliza, Mwalimu tufanye nini na sisi? Akawaambia, msitoze zaidi kitu zaidi kuliko mlivyoamriwa. Askari nao wakamuuliza wakisema, na sisi tufanye nini? Akawaambia, msidhulumu mtu wala msishtaki kwa uongo tena mtoshewe na mishahara yenu."

Mheshimiwa Naibu Spika, haya maneno ni ya miaka 2000 iliyopita! Ni maneno ambayo yako kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Rais Magufuli, yanafanana; anawaambia Watendaji wa Serikali, Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi, wote timizeni wajibu wenu, vinginevyo shoka liko shinani. Mti usiozaa matunda utakatwa! (Makofii)

Sasa msianze kulalamika, aah mimi, hapana! Timizeni wajibu wenu. Yohana Mbatizaji alikuwa anawaambia hawa, ili warithi Ufalme wa Mbingu.

Mheshimiwa Rais Magufuli anawaambia Watendaji wa Serikali ili tuondoe umasikini kwa Watanzania, ili tulete maendeleo kwa Watanzania. Kwa hiyo, timizeni wajibu wenu, vinginevyo shoka liko shinani, mti usiozaa utakatwa na kutupwa motoni. Ninaomba hotuba hii hasa pale kwenye vipaumbele ambavyo ameweka Rais, Serikali mhakikishe Wakuu wa Mikoa wanayo, Wakuu wa Wilaya wanayo, Watendaji wanayo waangalie Rais ameweka vipaumbele gani kwenye hotuba yake. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba hii anasema wakulima na wavuvi, hasa wakulima, wataletewa pembejeo kwa wakati, watawekewa huduma za ugani, watatafutiwa masoko panaposumbua! Jimboni kwangu mwaka uliokwisha wakulima wa tumbaku

## Nakala ya Mtando (Online Document)

wamesumbuka sana, soko la tumbaku halipo. Naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo hili ni jipu lako la kwanza, uhakikishe wakulima wa tumbaku wa Jimbo la Lupa na hasa nchi nzima, watafutiwe soko la zao lao kwa wakati. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, iko nchi ya Zimbabwe ambayo yenyewe imeingia ubia na Jamhuri ya Watu wa China kwamba tumbaku yote ya Zimbabwe inanunuliwa na China. Unajua Wachina wako wengi sana, wako watu *1.6 billion* kwa hiyo, chakula kinahitajika kingi, vinywaji vingi, hata tumbaku ya kuvuta inahitajika nyingi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, naomba jipu hili ulishike vizuri ili wakulima wa tumbaku wa Jimbo la Lupa na nchi nzima mwaka huu wapate soko la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Hotuba hii ya Mheshimiwa Rais aliongea kwamba anataka kuleta Muswada Bungeni kubadilisha vipengele fulani vya Sheria ya Manunuzi, ili iharakishe, iletu unafuu wa kuleta huduma kwa Watanzania. Nawaambia wadau wote, nimeongelea Sheria ya Manunuzi miaka 10 Bungeni hapa kwamba jamani eeh, bajeti yetu inatakiwa ni triliuni 20! Ujue kwamba 70% ya hela hizo inaenda kwenye manunuzi! Sasa mkiona Rais mwenyewe wa nchi ameshtuka anasema tuongelee manunuzi, muichukulie very positively watendaji wote, ili mlete mapendekezo mazuri ya kuirekebisha sheria hiyo, ili iweze kuharakisha kupeleka huduma kwa Watanzania. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, pale ambapo muda wa tender ni siku 60, kwa nini, inachelewesa kupeleka huduma kwa Watanzania. Pale ambapo *tender sum* ya kujenga barabara kutoka hapa kwenda Iringa ni shilingi milioni 200, lakini *variations* zinazotolewa hapo inafika milioni 600, ni vitu vya kuiyangalia hivyo. Pale ambapo Mtendaji au Accounting Officer kwenye Wizara, kwenye Idara, anasema ikifika shilingi milioni 50 lazima akapate kibali kwa Accountant General! Hilo ni la kuliangalia, ili hiyo nayo *threshold* iongezwe kutoka milioni 50 iende 500 au bilioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, sera ya magari; nimesema sana Serikali iwe na sera ya magari. Kuwe na sera ya magari siyo kwamba huyu ananunua hili, huyu ananunua hili, hapana, kuwe na sera ya magari kabisa. Kenya, Rwanda, Zambia na Malawi wana sera ya magari! Kwingine kote kuwe na Sera ya Magari! Hiyo Sera mkiandika vizuri na mkaitia kwenye Sheria, kuna kitu Watendaji wa Serikali wanafanya sana hapa, una-acquire property ya Serikali by tender, lakini sasa katika kui-dispose sheria inasema u-dispose by tender! Magari wanajiuza! Hiyo naomba isimamishwe kwenye mapendekezo ambayo yataletwa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, mwaka jana Serikali yetu nzuri ilitangaza kupitia kwa Rais na kwa Waziri Mkuu kwamba Mkoo wa Mbeya utagawiwa kuwe na Mkoo wa Songwe na wa Mbeya na kwamba Wilaya ya Chunya itagawiwa kuwe na Wilaya mbili; Wilaya ya Songwe na ya Chunya. Namwomba sasa Mheshimiwa Simbachawene atekelze ahadi hiyo haraka, ili kila Wilaya katika hizo Wilaya mbili itengeneze Halmashauri yake ili kuharakisha kuwapelekea huduma wananchi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kuna kitu kinanisumbua sana, kinanisumbua kweli, consistency! Nimeshindwa namna ya kusema Kiswahili, consistency! Wakati wa mjadala wa kusema Jamhuri yetu ya Tanzania tuwe na Serikali ngapi, mbili, tatu! Wanasema aah, hapana, Zanzibari bwana wakae mbali kule, wakae mbali! Hapana, hapana, kuwe na Serikali yao huko! Sawa bwana! Wakati wa uchaguzi, wanasema aah, wale ndugu zetu bwana, lazima tuwasaidie wale, consistency! Nakushukuru sana. (Makof)

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja iliyoko mezani. Nianze kwa kusema Serikali nyingi duniani

## Nakala ya Mtando (Online Document)

huongozwa kwa Katiba iliyojiwekea, Sheria zilizopo, Kanuni zilizopo, Taratibu zilizopo au Dira ambayo imejiwekea kama nchi, lakini katika Serikali ya Awamu ya Tano tunaona mnaongozwa kwa kauli mbiu ya hapa kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtanielewa tu! Nasema mnaongozwa kwa hapa kazi, bila kufuata Sheria zilizopo, Kanuni zilizopo, utaratibu uliopo na Katiba mliyojiwekea. Nasema haya kwa mifano nitakayoitoa; Rais anafukuza watumishi wa umma! Ni kweli kwamba kuna baadhi ya watumishi wa umma sio waaminifu na wana upungufu. Pia, ni kweli kwamba kuna baadhi ya watumishi wako kwenye mamlaka ya Rais, wale alioivateuwa anaweza kuwaondoa, lakini kuna wale ambao wameajiriwa, ni sharti taratibu na sheria za kiutumishi zifuatwe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwengine; mmesema mnatoa elimu bure, mtapeleka takribani shilingi bilioni 18 kwa Halmashauri! Mnapeleka kwa bajeti ipi ambayo hatujapitisha ndani ya Bunge? Bunge la Kumi, tulipitisha Bajeti, ni lini mmeleta Supplementary Budget ndani ya Bunge, ili mtekeleze hili? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwengine, Rais alifuta sherehe za Uhuru! Ni kweli kwamba katika Bunge la Kumi kati ya mambo ambayo Upinzani tulikuwa tunapigia kelele, ni kufuta sherehe mbalimbali ambazo hazina tija, ni jambo jema. Amefuta sherehe za Uhuru akatoa agizo fedha zipelekwe kwenye ujenzi wa barabara ya Morocco; amefanya fedha hizo zimekwenda, taratibu za manunuzi, kutangaza tender, Sheria mliyojiwekea ya Manunuzi, mmefuata au mnasema tu hapa kazi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, kupitia vyombo vya habari, jana au juzi, Afisa mmoja wa Serikali amesema watapeleka shilingi milioni 50 kwa kila kijiji! Nawauliza kwa Bajeti ipi? Kwa Sheria ipi? Kwa Supplementary Budget ipi mliyojiwekea? Au mnaongozwa tu kwa hapa kazi, bila kufuata sheria zilizopo? Mtakuwa ni Serikali ya ajabu duniani kuongozwa na kauli mbiu badala ya sheria mlizojiwekea. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba ya Rais ameelezea kwa upana suala la amani na utulivu na mmekuwa mkijivunia amani na utulivu. Mnawaambia Watanzania kuna amani na utulivu, wakati hakuna demokrasia ndani ya nchi hii, demokrasia zinaminywa zinakanyagwa. Kuna migogoro ya ardhi, wakulima na wafugaji, halafu mnasema amani na utulivu! Hakuna ajira kwa vijana, halafu mnasema amani na utulivu! Mahakama hazitoi haki kwa wakati, halafu mnasema amani na utulivu! Hospitalini hakuna dawa, kinamama wakienda kupata huduma zipo mbali au wakati mwengine hazipatikani, mnasema amani na utulivu! Tumeona utumiaji wa nguvu za kidola wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi, halafu mnasema amani na utulivu! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, itafika mahali Watanzania hawatathubutu tena kuvumilia amani na utulivu wakati wana shida lukuki! Hakuna haki, watu wanakandamizwa, watu wananyanyaswa, halafu mnang'ang'ania kusema amani na utulivu! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie machache kwa kusema katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais, ameellezea hali ya kisiasa Zanzibar. Hili tunamwambia nalo ni jipu alitumbue, alifanyie kazi! Mshindi atangazwe! Si mmesema ninyi hapa kazi! Fuateni basi Sheria, Katiba na Taratibu mlizojiwekea. Mtangazeni mshindi wa Zanzibar, kwa nini mnaogopa? Mkiambiwa hili mnaogopaaogopa na mnaanza kupiga-piga kelele, kuna nini kimejificha hapa? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka suala la mgogoro wa kisiasa, kama amesema yeye atakuwa ni Rais wa kutumbua majibu basi atumbue na hili, Wazanzibari wapate haki yao waliyemchagua aweze kutangazwa. Ahsante. (Makofi)

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MBUNGE FULANI:** Tarehe 20 Machi!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Adadi Rajab, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, halafu Mheshimiwa Catherine Magige. Mheshimiwa Adadi Rajab!

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa leo kuniweka hapa.

Pili, ningependa kuwashukuru Wanamuheza ambao wakati wa kampeni niliwaomba wanileté kwenye jengo hili na wamenileta, nawashukuru sana tena sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Rais moja kwa moja kwa asilimia mia moja. Mheshimiwa Rais kwenye hotuba hiyo ameainisha mambo chungu nzima; nilikuwa nasoma mstari kwa mstari na nilikuwa na-underline, nilipofika mwisho wa kitabu nikakuta nime-underline mistari yote kwenye kitabu hicho. Kwa sababu kila point, kila mstari ambao nilikuwa nauona, niliuona ni wa msingi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba hiyo, lakini ningewaomba Waheshimiwa Wabunge waangalie namna Mheshimiwa Rais aliyokuwa anai-present hotuba hiyo, seriousness aliyokuwa nayo, commitment aliyokuwa nayo siku ambayo alikuwa anaiwasilisha hotuba hiyo na baada ya hapo matendo yake baada ya hiyo hotuba! Jamani mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni! (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameainisha matatizo ambayo sijui ameacha tatizo gani kwenye hii hotuba. Ameanzia na huduma za jamii, matatizo yote yapo pale, matatizo ya maji, umeme, barabara, kila kitu kiko pale. Tatizo moja kubwa sana ambalo wote humu Waheshimiwa Wabunge tunalo, isipokuwa wananchi wa Muheza wanalo zaidi ni la maji. Wanamuheza wana shida ya maji! Yapo matatizo ya umeme, lakini umeme umefanyiwa kazi kubwa sana, REA imefanya kazi kubwa sana! (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali iangalie uwezekano, utaratibu ambao umetumika kwa REA, utaratibu huo utumike kwa maji vijijini. Wananchi wana taabu, sikupata nafasi ya kuchangia jana, lakini nina hakika Waziri wa Maji yuko hapa atahakikisha kwamba, kweli suala la maji linapewa kipaumbele kwenye bajeti inayokuja. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuangalia matatizo hayo; sasa hivi tunakwenda kwenye sera ya Tanzania ya viwanda. Hatuwezi kujenga viwanda bila kuangalia kwanza haya matatizo ya umeme na maji tuyashughulikie, matatizo ya barabara, hivyo viwanda vitakavyopelekwa huko, barabara zitapita wapi. Naamini Mheshimiwa Rais kutokana na ahadi zake alizozisema, kutokana na commitment ambayo anayo kwamba ahadi alizozitoa zitatekelezeka. Tumeona ahadi zinaahidiwa nyuma, kuna barabara yangu kule ya Amani mpaka Muheza kilomita 40, awamu mbili zilizopita zimeahidi kwa kiwango cha lami barabara hiyo, lakini hakuna lami iliyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Amani wanavuna, sasa hivi kuna viungo, kuna chai ambapo sasa ni wakati wa kuvuna viungo hivyo, wanashindwa kuteremsha mazao hayo, wanapata taabu kila saa magari yanakwama. Naamimi kabisa kwamba Waziri wa Ujenzi yupo hapa na ataliangalia suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia suala la viwanda, Tanzania ya viwanda, lakini naamini kwamba Waziri wa Viwanda ataangalia kiwanda kipi ambacho kinatakiwa kiwe wapi na mkoa gani ambao unatoa zao gani. Tuanze kufufua viwanda ambavyo vilikuwepo kabla ya

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

kufikiria kuanza kujenga viwanda vingine, lakini Kiwanda cha Machungwa Muheza kianze kujengwa mapema. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanga kulikuwa na viwanda chungu nzima, viwanda vimekuwa pale; ningefurahi sana kuona kwamba viwanda vile vinaaza kufufuliwa na wananchi wa Mkoa wa Tanga basi wanaanza kufaidika na viwanda hiyo. Kuna mazao chungu nzima ambayo yako Tanga na ambayo naamini kabisa kwamba kama viwanda hivyo vitafufuliwa basi tutakuwa na uwezo wa kujenga uchumi wetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo kuna mambo mengi ambayo yamezunguka Tanga, hapa imezungumzwa reli ya kati tu, reli ya Tanga - Arusha mpaka Musoma hadi Nairobi imesahauliwa kabisa. Ningefurahi na ningeshukuru kama ningekiona kitu hicho kwenye Mpango huu wa Bajeti ambaa unakuja. Vivyo hivyo pamoja na Bandari ya Tanga, tunazungumzia mambo ya Bandari nyingine tunaacha Bandari ya Tanga ambayo ni bandari kubwa kabisa pale, kwa nini hatuizungumzii? Naomba Waziri anayehusika aliangalie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu; Serikali imeanza vizuri kabisa. Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya elimu bure na imeanza kutekelezwa. Lazima tuwe na pa kuanzia, matatizo madogo madogo yanaweza kuwepo, lakini lazima tuweke sehemu ya kuanzia. Tumeanza vizuri na naamini wananchi wote nchi hii wamefurahi kwamba elimu imekuwa bure. Hayo matatizo ambayo yanatokea hapo yatarekebishwa. Tusiikatishe tamaa Serikali hii kwa jinsi walivyoanza, tuwaunge mkono Waheshimiwa Wabunge. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna shule nyingi ambazo zinaishia darasa la kumi na mbili (*form four*), lakini tuna shule chache sana za Serikali za kidato cha tano na cha sita. Umefika wakati sasa hivi Serikali iondoe ukiritimba ambaa upo wa kusema kwamba lazima shule za Serikali za *form five* na *six* ziwe *boarding*. Tunahitaji sasa hivi iwe day, watoto wetu waweze kusoma kwa sababu sasa hivi shule zimekuwa nyingi, lakini za *form five* na *six* zimekuwa ni chache, naomba mliangalile.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Mheshimiwa Rais ameongelea suala la wawekezaji, lakini ni lazima tuangalie na tukubali kwamba maandalizi yetu ya wawekezaji *not friendly*, bado kuna matatizo mengi sana EPZA, TIC, bado kuna ukiritimba mkubwa sana ndiyo maana wawekezaji wanatoka hapa wanarudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Mabalozi tuna Sera ya Diplomasia ya Uchumi, tuliambiwa tulete wawekezaji, tunawaleta wawekezaji, wanarudi. Kuna leseni sijui karibu 18 mara ya mwisho nilipokwenda TIC pale au vibali ambavyo mwekezaji anatakiwa apewe. Unategemea huyo mwekezaji atawekeza kweli, jamani tuangalie hilo suala na kama mnataka Mabalozi watekeleze kweli *Economic Diplomacy*, basi tuhakikishe kwamba huu ukiritimba na huu urasimu unaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la utulivu na amani, Waheshimiwa Wabunge, lazima tukubali kwamba uchaguzi huu tumeufanya kwa utulivu na amani. Kama kulitokea uvunjiju wa amani, ni kidogo, lakini kazi ambayo wamefanya vyombo vyamini dola ni kubwa jamani. Ninyi hamuelewi namna ya kutuliza utulivu wa amani, ni kazi kubwa, vyombo vyamini dola vilikuwa havilali, ni lazima tuvipongeze na tuviunge mkono vyombo vyetu jamani.

*(Hapa kengele ilipigwa kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Balozi muda wako umekwisha.

**MHE. BALOZI. ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu kumalizia kwa kusema kwamba....

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha naomba ukae tafadhalii.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Magige, baada ya Catherine atafuata Mheshimiwa Peter Msigwa.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa uzima na uhai mpaka siku ya leo niko mahali hapa, namshukuru sana Mungu.

Pili naomba niwashukuru akinamama wote wa Mkoa wa Katavi walionipa fursa ya kuingia kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kuwatumikia. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Rais wetu, kwa kazi nzuri ambayo anaifanya na mpaka sasa hivi wananchi wa Tanzania wamemkubali kutokana na kazi nzuri anayoifanya. Si kazi rahisi kutumbua majibu makubwa makubwa ambayo yalikuwa hayalipi kodi...

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walikuwa  
wakiongea bila utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Endelea.

**MBUNGE FULANI:** Ingekuwa UKAWA wamefanya hivyo wangepiga kelele. (Kicheko)

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, wale watu ambaa walikuwa hawalipi kodi, lakini Mheshimiwa Rais wetu amethubutu kufanya kazi hiyo na matokeo yameonekana na kodi sasa zimeonekana mpaka hatimaye sasa watoto wetu wameweza kwenda kusoma bure kwa sababu ya mambo mazuri ambayo Rais wetu alituahidi. (Makofii)

**MBUNGE FULANI:** Wewe ongea tu.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ni kazi, mimi nitaendelea. Kuna kazi ambayo tunatakiwa tuifanye na Serikali inatakiwa iangalie kwa makini kuhusu Halmashauri zetu upande wa Wakurugenzi pamoja na Watendaji. Kuna sehemu nyingine watendaji wanakaimu na kama Mkurugenzi mara nyingi anakaimu siyo Mkurugenzi kamili inakuwa kazi kufanya kazi ya maendeleo katika maeneo husika. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta sehemu nyingi kuna miradi mbalimbali ambayo Serikali iliainisha ili iweze kufanyika. Katika maeneo mengi miradi hiyo haikuweza kukamilika kutokana na utendaji. Ukienda pale anasema mimi Kaimu, Mkurugenzi kasafiri siwezi kufanya jambo lolote. Hilo limekwamisha sana miradi yetu tuliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kazi inaendelea, kuna Wakurugenzi wengi wamesimamishwa kutokana na majipu, lakini bado kuna maeneo mengi ambayo uaminifu ni

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

mdogo. Naomba kazi hiyo iendelee, tuweze kusafisha ili fedha za maendeleo tukipanga bajeti ziweze kufikia malengo yale tunayoyatarajia. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende upande wa wakulima na wafugaji. Kifike kipindi sasa Serikali, iainishe maeneo ya wakulima na wahainishe maeneo ya wafugaji. Limekuwa tatizo kubwa sana kiasi ambacho sasa hivi kuna vitu ambavyo vinaashiria siyo vizuri, wanapigana, wanaauana na sisi nchi yetu ni nchi ya amani na utulivu. Naomba Serikali yetu ijipange vizuri kwa ajili ya eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Waziri wa Ardhi, ametuandikia barua Wabunge wengi tuainishe migogoro ya ardhi. Naomba nikupongeze sana Waziri wa Ardhi kwa kuliona hilo, tuweze kukusaidia na tuainishe maeneo yote yenye migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kwenye reli, watu wengi wamezungumza kuhusu masuala ya reli. Kwangu Mpanda ni kitu muhimu sana kutokana na na hali halisi ya sasa hivi barabara zote hazifai, wananchi wa Mpanda wako hewani, mambo yao hayaendi vizuri. Namwomba Mheshimiwa Waziri reli hii ya Mpanda hata treni ianze kwenda kwa sababu wananchi wa Mpanda wanapata shida, taabu kwa ajili ya mahitaji yao binafsi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye masuala ya uchumi, uchumi hauwezi kukua bila miundombinu. Maeneo ya Tabora, Kigoma, Mpanda ni maeneo ambayo yana uchumi mkubwa, wanalima sana, wana mazao mengi, ambayo yanatakiwa yatoke kwa ajili ya Watanzania wote, lakini kutokana na miundombinu mibaya, barabara hazifai. Mtu anatoka Tabora kwenda Mpanda anatumia siku tatu, analala njiani, kusema kweli tunasikitika sisi Wabunge tunaotoka maeneo hayo kuwa tumesahaulika muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, mtuangalie kwa jicho la huruma wale wananchi ni Watanzania kama Watanzania wengine, wanahitaji mahitaji muhimu. Shughuli zao za kilimo, basi waweze kutoa mazao yao ili waweze kupata mahitaji yao binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja upande wa polisi, nawapongeza sana polisi wetu, wamefanya kazi nzuri, lakini kuna maeneo mengi nyeti hakuna vituo vya polisi, wananchi usalama wao unakuwa mdogo, maeneo mengi utakuta wana mazao mengi, lakini usalama wao haupo kutokana na kukosekana kwa kituo cha polisi katika maeneo hayo. Tunaomba Serikali ijipange basi kupeleka vituo vya polisi katika maeneo hayo ili wananchi waweze kupata usalama wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye mapato tena. Zamani kulikuwa kuna Shirika lilikuwa linaitwa NASACO, Shirika la NASACO lilikuwa linakusanya mapato bandarini, ile mizigo yote inayotoka kwenye meli, lile shirika sasa hivi halipo. Sasa naomba kama kuna uwezekano Serikalini, lile lilikuwa linasaidia sana mapato yalikuwa hayawezi kupotea ndani ya bandari zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi Serikali ijipangwe vizuri, kuona ni jinsi gani ya kuweza kuitisha makontena ndani ya bandari zetu, maana kuna maeneo mengine hakuna usalama mzuri, watu wanaingiza mizigo bila kulipa ushuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia Tanga, bandari bubu nyingi, lakini na Mpanda, Kalema kuna bandari, mpaka leo hatuwezi kujua hatima yake itaisha vipi. Kuna sehemu nyingi muhimu, nyeti ambazo zinaweza kulilettea Taifa hili mapato, lakini tumeliacha wazi. Tunaomba basi na sisi bandari ile ya Kalema ifanyiwe kazi, ina miaka sijui sita sasa hivi, majengo yalianza,

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Mkandarasi sijui ka-disappear wapi hatufahamu. Tunaomba basi ili uchumi uweze kukua, bandari, reli na barabara ziweze kutengenezwa vizuri kwa kiwango cha lami. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Serikali ijipange, mnapoteza hela nyingi...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha, tafadhali naomba ukae

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige!

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa naomba niwashukuru akinamama wa Mkoa wa Arusha kwa kuniamini na kunipa kura kwa ajili ya kuwawakilisha Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba nzuri aliyoleta wakati wa ufunguzi wa Bunge la Kumi na Moja. Hotuba hiyo iligusa maeneo mengi katika nchi yetu. Vilevile ilitupa mwelekeo na dira ya Serikali ya Awama ya Tano. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze moja kwa moja katika mchango wangu, nimefarijika sana Mheshimiwa Rais aliposema kuwa Tanzania itakuwa nchi ya viwanda. Katika Mkoa wangu wa Arusha, miaka ya 1970 na 1980 kulikuwa na viwanda vingi sana vyta Serikali pamoja na watu binafsi kama vile Kiwanda cha Tanelec, Kiwanda cha Biskuti na cha Matairi cha General Tyre. Viwanda hivi vyote kwa sasa hivi havifanyi kazi, hali iliyopelekea madhara makubwa sana kwa wakazi wa Arusha na maeneo jirani na Mkoa wetu wa Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Matairi cha General Tyre kilikuwa kiwanda kikubwa sana cha kuzalisha matairi Afrika Mashariki. Kiwanda hiki kilikuwa kimeajiri watu zaidi ya 400, kiwanda hiki kilikuwa kinaingiza mapato shilingi bilioni 100 kila mwaka na takwimu hizi ni kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2008. Kiwanda hiki kilifikia stage kikawa kinaajiri watu hadi milioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1971, Kiwanda cha General Tyre kilikuwa kiwanda namba moja Afrika Mashariki kwa kuzalisha matairi 1,200 kwa siku. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama kipindi hicho kiliweza kuzalisha matairi 1,200 kwa siku, sasa hivi tunashindwa kitu gani? Kwa sasa hivi soko la matairi lipo kubwa sana, kwa sababu tukianza kikitumia Kiwanda cha Matairi cha General Tyre, tutaanza na Serikali na taasisi zake zote kununua matairi ya General Tyre pamoja na mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile soko la matairi bado kubwa sana, watu wengi sasa hivi wanatumia magari, magari yote hayo yanahitaji matairi. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ikianzishe upya Kiwanda cha General Tyre ili kiendelee kuleta mapato katika nchi yetu. Kiwanda cha General Tyre kimepunguza ajira kwa vijana wa Arusha, wananchi wa Arusha, vijana wa Arusha, wanahitaji ajira, ajira hii itapatikanaje? Itapatikana kwa kurudisha viwanda vyetu ambavyo vilikuwa havipo tena. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Arusha hawaamini kama Serikali imeshindwa kufungua kiwanda kile. Wananchi wa Arusha tunaamini kuna hujuma za baadhi ya wafanyakishara ambao wana-import matairi kutoka nje kwa ajili ya faida zao wenye hali ambayo inapelekea sisi kukosa uwezo wa kufungua kiwanda kile cha General Tyre.

## Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa taarifa nyingi za kipolisi zinaonyesha ajali nyingi zinatokea kutokana na matairi yasiyokuwa na ubora ambayo tunayaagiza kutoka nje. Tumekuwa tunapoteza ndugu zetu katika ajali kwa sababu ya matairi. Sasa naona ni wakati muafaka kwa Serikali kukifungua upya Kiwanda cha Matairi cha Arusha (General Tyre) ili tuweze kutumia matairi yale ambayo yana ubora. (Makofii)

Naomba niende moja kwa moja katika suala la maji. Tatizo la maji limekuwa kubwa sana kabla ya uhuru na baada ya uhuru. Kina mama wa Mkoa wa Arusha wamechoka kuhangainka na tatizo la maji. Kuna maji Ngorongoro, Monduli na Longido. Wamenituma niombe Serikali yao, wanamwamini Mheshimiwa Magufuli, wanaimani kubwa na Serikali ya Mapinduzi. Tunaomba sana kina mama hawa wa Arusha wasahau shida hii ya maji. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi wa maji wa West Kilimanjaro. Serikali ikitusaidia kuanzisha mradi ule vijiji kadhaa vitapata maji. Mradi ule tunaomba upelekwe mpaka Longido ambapo vijijini vya njiani kama Tingatinga, Singa, Kerenyai, Engiraret, Orbebe, Orpesi, Ranchi mpaka Longido navyo vipate maji. Vilevile Monduli, Monduli kulikuwa na mabwawa matatu na yenyewe yamepasuka. Wananchi wa Monduli wanakunywa maji ya mabwawani pamoja na mifugo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana Serikali iangalie suala hili la tatizo la maji katika Mkoa wa Arusha. Naomba sana Waziri wa Maji unisaidie sana kutatua tatizo hili. Nakuamini najua ndio maana Mheshimiwa Rais wetu tunayemuamini akakuchagua, tunaomba utusaidie. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na migogoro ya wakulima na wafugaji. Kila siku wananchi wamekuwa wakiuwawa, mifugo imekuwa ikiuwawa lakini migogoro hii imekuwa haishi, nenda rudi migogoro hii inaendelea na wananchi wanazidi kuisha kwa ajili ya kufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini sana wateuzi wa Rais, namwamini sana Mheshimiwa Lukuvi. Mheshimiwa Lukuvi nakuomba baada ya Bunge hili uje Mkoa wa Arusha kuna matatizo mengi ya ardhi, kuna tatizo la ardhi Loliondo, wananchi wamekuwa wakipata shida hawajielewi, hatujui Serikali inataka nini, hatujui wanavijiji wanataka nini, hatujui wafugaji wanataka nini? Tunaomba sana Serikali iliangularie suala hili. Wananchi wamekuwa wanachomewa nyumba zao, mifugo yao inauliwa lakini sasa hivi Awamu ya Tano, tuna imani kubwa sana na Serikali na ukizingatia hotuba ya Rais wetu imeeleza kila kitu, tunaimani hawatatuangusha watatusaidia sana. (Makofii)

Naomba niongelee pia suala zima la Polisi. Polisi tumekuwa tukiwalaumu sana lakini vilevile Polisi wanaishi katika mazingira magumu sana. Nikitolea mfano Arusha Mjini kuna zile nyumba za Fire, ukipita pale ni aibu. Nyumba za Polisi ni chafu sana, ni nyumba ndogo na mnajua familia zetu za Kiafrika tunavyoishi. Polisi wale wanaishi katika mazingira ya shida sana na hata kwa kupita tu kwa mbali nyumba ni chafu sana. Tunaomba sana Serikali iangalie jinsi gani ya kuwasaidia Polisi katika suala zima la nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mabadiliko ya tabia nchi limekuwa linasababisha matatizo makubwa sana ya malisho ya mifugo pamoja na maji. Nakumbuka mwaka 2007 kulikuwa na ukame. Wilaya za Monduli, Longido, Ngorongoro, wafugaji walikosa malisho, mifugo yao ilikuwa inakufa na wenyewe wakawa wanaishi kwa kuhamahama. Tunajua wafugaji wanaishi kwa kuhamahama siyo kwa kupenda bali kutokana na mazingira wanayokuwepo, unakuta mifugo yao haipati maji, haipati huduma kwa hiyo, inabidi wahame. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, tunaomba sana mliangularie wafugaji wa Mkoa wa Arusha kwa ujumla. (Makofii)

## Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana hotuba ya Rais imegusa mambo mengi sana. Nashangaa sana watu wanapokaa na kuikejeli hotuba ya Rais. Mmeona hata juzi Mheshimiwa Magufuli amefika Arusha wananchi walivyomlaki kwa furaha. Mbunge mwenzangu wa Arusha pale awe makini sana, kwa kauli alizozitoa hapa wananchi wa Arusha wanaweza wakampiga mawe na kumzomea kwa sababu wamemkubali Magufuli na Serikali ya Chama cha CCM. Nilitegemea Mbunge mwenzangu atasimama na kumsifu Mheshimiwa Rais Magufuli na kusifu wananchi wa Tanzania pamoja na wananchi wa Mkoa wa Arusha kwa kumpa kura za kutosha Rais Magufuli. Naomba sana tukubali, upinzani siyo kupinga kila kitu. (Makofi)

(Hapa kengele *ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magige muda wako umekwisha.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Sasa tutamsikia Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Khatib Said Haji.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2012, Mheshimiwa Mnyika alisimama hapa Bungeni akasema tumefika hapa tulipo kwa sababu ya udhaifu wa Bunge. Akasema tumefika hapa tulipo kwa sababu ya udhaifu wa CCM na tumefika hapa tulipo kwa sababu ya udhaifu wa Rais Kikwete, mlimzomea, mkachukua Polisi mkamtoa. Leo wale wateule wa JK toka Magufuli ameingia amewaporomosha zaidi ya 30. Leo mnapiga makofi mnasema majibu yanatumbuliwa lakini miaka mitano iliyopita tulizungumza mambo ya safari za JK, mlitetea humu ndani na mkapiga makofi. Miaka mitano iliyopita tulizungumza sherehe, kofia, miavuli isiyo na tija mlipiga makofi, leo wengine mnajitoa ufahamu mnasema majipu yanatumbuliwa. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza hotuba ya Mheshimiwa Rais hii nchi ni ya wote. Mheshimiwa Rais tumempa kazi na Bunge hili lina wajibu wa kumsimamia, Tanzania ni yetu sote. Kwa hiyo, hatujaja hapa kumpambapamba, ana kazi anayotakiwa kuifanya kwa Watanzania. Nikisema simuungi mkono katika mambo mengine anayofanya nitakuwa mwongo na nitakuwa mnafiki. Sisi kama Wabunge tunawajibu wa kutimiza wajibu wetu wa kuisimamia Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge liliopita liliikubali kutokuwa na meno na Mnyika alisema mkamzomea akatoka nje, tunataka turudie makosa yale yale ya kuwa na Bunge butu. Wananchi wametutuma tuisimamie Serikali pamoja na kumwambia ukweli Mheshimiwa Magufuli. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Magufuli anasema anataka kubana matumizi, jambo ambalo ni zuri na Mbunge yeoyote mwenye akili ataunga mkono. Hata hivyo, matumizi anayoyabana tumezungumza sana hapa, kuna idadi kubwa ya Wakuu wa Wilaya wanaendesha mashangingi hawana tija katika nchi hii akitaka kupunguza matumizi awatooe hao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, unamkuta Mkuu wa Wilaya naye ana chumba cha mikutano, kikao kikubwa anachoweza kufanya ni cha kuwa na wale walinzi na kazi yao ni kudhibiti mikutano ya CHADEMA. Hiyo kazi anaweza akafanya OCD, hatuhitaji Mkuu wa Wilaya. Wala

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mkuu wa Mkoa hatumhitaji, kama ni kupunguza matumizi tumtoe huko. Kazi za Wakuu wa Wilaya wameishia kuomba hela kwa Wakurugenzi, abishe mtu kama haombi hela kwa Wakurugenzi hapa. Haya ndiyo mambo tunatakiwa tujadili kama tunataka tuisaidie Serikali ipunguze matumizi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia masuala ya utawala bora, Mheshimiwa Mbarawa, wewe ni Mzanzibar na wenzako ambao hamjaapishwa, mnaondoka Zanzibar mnakuja kutaka kupiga kura Dar es Salaam, kuna utawala bora hapo? Hayo ndiyo majibu mnatakiwa mumwambie Magufuli ayatumbue na muanze kutumbuliwa wenyewe. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Kilombero.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina kaka yangu Maige kutoka Iringa, mwanadiplomasia, ameshiriki kwenye vikao vingi vya kutatua migogoro duniani hapa na ye ye anaondoka mwanadiplomasia, Waziri wa Nchi za Nje, hajaapishwa anaenda kutaka kupiga kura Kinondoni, huo ndiyo utawala bora? (Makofi/Kicheko)

**MBUNGE FULANI:** Kilombero, Kilombero.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni *hypocrisy of the highest order*. Kama Rais anataka utawala bora haya ndiyo mambo tunatakiwa tujadili ili Taifa tuliweke katika misingi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kesho Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje kama ingemwagika damu Dar es Salaam angekwenda Rwanda kusuluhisha migogoro? Hebu tuwe wa kweli, tusijitoe ufahamu hapa. Hii nchi wote tunaipenda tuzungumze mambo ya msingi, hayo ndiyo mambo ya utawala bora?

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Kilombero Mbunge mwenzetu anapigwa na kubebwa mzobemzobe na Polisi kwenye Jimbo lake mnakuja mmapiga vigelele hapa mnasema, utawala bora! Mbunge anazuilliwa kupiga kura kwenye Jimbo lake, haya ndiyo mambo tunayotakiwa tuzungumze hapa lakini tunarudi kwenye mambo yale yale kwa akili ileile. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, mnasema utawala bora, rafiki yangu Kigwangalla anaondoka hata hafuati taratibu za Utumishi wa Umma unaenda kufungia watu kwenye ofisi. Najua nia nzuri ya Rais ya kutaka tulete mabadiliko lakini kama hatuja-change mindset za wafanyakazi wetu ni tatizo? Kama gari lako unaweza kuliendesa lina speed ya 120 hata unune, ukemee, haliwezi kwenda speed 200. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mmewajengea uwezo kiasi gani hawa watu? Human resources tulyonayo ndiyo hii, hamjawajengea uwezo wa kufikiri vizuri, hamjawa-motivate, hamjawa-inspire, hamjajenga uwezo wa kwenda na kasi hii. Sasa hivi tunakwenda kwenye transformation hamjafanya hayo mambo kazi yenu ni kufukuzafukuza. Inawezekana nia ya Rais ni nzuri ya kutaka kuleta mabadiliko sasa wengine kwa sababu mmepewa vyeo siyo kwa merit mnataka muonekane eti mnafanya kazi, mnafungia watu milango, mnawafokea watu, anatoka hata Mkuu wa Mkoa anaenda kufokea watendaji wa mitaa ambao hawako chini yake wako chini ya Mkurugenzi, huo ni utawala gani bora wa sheria? Hebu tujihoji ndugu zangu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumekuja hapa tunapoanza hebu tuache kujitoa ufahamu. Tena nashukuru sasa hivi wengi mmekuja mnaufahamu, tuisimamie Serikali kama kweli tunataka maendeleo katika nchi hii. (Makofi)

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, akina Wassira wameondoka walikuwa hivyo hivyo, akina Malima walikuwa hivyo hivyo walikuwa kimbelembelé, hebu tuwe wakweli tusijitoe ufahamu hapa. Kiukweli watu mnajitoa ufahamu matokeo ya Zanzibar yanaelewaka kabisa tunaanza kuongea ngonjera na mashairi, tunaacha kusimamia ukweli. Kama tunataka tumsimamie Rais majipu ndiyo hayo, tuanze na majipu hayo, tusimame kiukweli tuitetee Serikali. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, unasema tunapunguza matumizi lakini matumizi yako pale pale. Wakuu wa Mkoa wana kazi gani? Mnasema msimamizi wa usalama kwani RPC hawezi kufanya? Ni kazi ipi ambayo hawezi kufanya RPC mpaka awepo Mkuu wa Mkoa, ndiyo kazi kubwa wanayofanya. Hawa hawana kaz, kama kweli tunataka tupunguze matumizi ndiyo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hatutabadilika na hatutasimama kama Bunge ambalo wajibu wetu ni kuisimamia Serikali siyo kumpambapamba tu Magufuli na Serikali ya CCM, hizi ni kodi za wananchi na wananchi wametuleta hapa tuisimamie Serikali. Kwa hiyo, niombe tusijitoe ufahamu ndugu zangu. Tulizungumza haya mambo mkatuzomea, mkaimba ni walewale na Kinana aliwaambia muisimamie Serikali lakini leo Mbunge wa CCM unasimama hapa unaipamba, unajikombakomba kwa Rais baada ya dakika mbili barabara ni mbaya, maji hayapo. (Kicheko/Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninayezungumza pamoja na figisufigisu ambazo Chama cha Mapinduzi kilijaribu kuleta, nina barabara nzuri Iringa Mjini, nina maji asilimia 98, taa barabarani zinawaka, halafu wewe unakuja unajikombakomba hapa badala ya kuisimamia Serikali iwasaidie wananchi wako. Unajikomba kwa lipi, hiyo siyo kazi ya Kibunge! Wengine wamegeuka hapa wamekuwa *Procurement Management Unit*, siyo kazi yenu. Hata Halmashauri nimechukua pamoja na figisufigisu, nadhani Nape salamu anazipata hizi. Kwa sababu nimefanya kazi ya kuwatumikia wananchi tuache unafiki, tuache kujikombakomba, tuisimamie Serikali.

**MBUNGE FULANI:** Kabisa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naona naishiwa muda, Mungu akubariki sana. (Makofii/Kicheko)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Khatib Said Hajji na Mheshimiwa Ally Keissy ajiandae.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nianze kutoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kunijalia leo kusimama hapa nikiwa na afya njema. Pili, niwashukuru kwa dhati sana wananchi wa Jimbo la Konde kwa kunirejesha tena hapa ili niweze kuwawakilisha. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, kwa umuhimu mkubwa sana natoa pongezi kwa wananchi wa Zanzibar kwa maamuzi mema na ya dhati ya kumchagua Maalim Seif Sharif Hamad kuwa Rais wa Zanzibar. Suala la Jecha kasema nini, Mwenyezi Mungu ataisimamisha haki hapa duniani na watu wote wataona. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ilikuwa ni bashrafu, sasa nataka nianze kuchangia. Ukurasa wa nane wa hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyeitoa hapa alisema, naomba ninukuu:-

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

"Eneo lingine linalolalamikiwa ni Polisi. Kuna malalamiko mengi ya wananchi kubambikiwa kesi, upendeleo, madai ya Askari kutotimizwa, ukosefu wa nyumba za Maaskari na kadhalika".

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko ya raia wa nchi hii juu ya Polisi ni mengi sana. Wakati mwingine tunaweza kuwalaumu Polisi wakati amri hizi wanazozitekeleza Polisi zinatoka kwa viongozi wa CCM. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchaguzi mkuu ilitoka amri ya Kiongozi Mkuu wa Serikali, Waziri Mkuu akiwaambia ni marufuku vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara hasa kwa wale waliokuwa hawakushinda. Kiujumla tangazo lile lilhusu kutubana sisi vyama vya upinzani kuonana na wananchi wetu kuwaeleza ukweli juu ya yaliyotokea katika uchaguzi mkuu, hii siyo sawa! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vyama vya siasa viro kwa mujibu wa Katiba. Tunapoapa hapa kabla ya kuanza kazi hizi tunaapa kuilinda, kuitetea na kuiheshimu Katiba hii. Leo unapokurupuka na amri zako zilizo kinyume na Katiba hii, wewe ndiyo unayesababisha fujo, tukubaliane! Kuna mambo tunayoinishiwa kama vyama vya siasa kwa mujibu wa Katiba tuna haja ya kuyatenda. Hatulazimiki kuomba vibali kwa Polisi tunapotaka kufanya mikutano yetu ya hadhara, tunalazimika kutoa taarifa, leo imepotea hii na badala yake twende tupige magoti kwao wao ni nani? Hilo ni moja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa kumi wa hotuba ya Mheshimiwa Rais alizungumzia suala la Zanzibar kwa kifupi sana kana kwamba si jambo muhimu sana. Naomba ninukuu sehemu tu:-

"Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na wadau wa siasa hususan vyama vya CUF na CCM, tutahakikisha majaribu ya kisiasa yanayoikabili Zanzibar yanamalizika kwa usalama kabisa".

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya neno hili alilolisema Rais mpaka leo hii Mheshimiwa Magufuli hajasema tena neno lingine lolote linalohusiana na Zanzibar, hajasema! Ameishia kuwaalika lkulu baadhi ya viongozi na pale alipokuwa akitoka hakuna lolote alilolizungumza kuweka njia ya kuonyesha kwamba analichukulia uzito suala la Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nieleze sisi ni wawakilishi wa wananchi. Mimi kabla ya kuja hapa Bungeni nilikutana na wananchi wangu wa Jimbo la Konde na kimoja walichotaka niseme nitakisema hapa bila kujali kwamba litawapendeza au litawakasirisha. Sikuja hapa kwa mapenzi ya yeyote, nimekuja hapa kwa mapenzi ya Mungu kwa uwakala wa watu wa Konde. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mnaposimama mkasema kwamba uchaguzi wa Zanzibar, wengine wamesema hapa, utarudiwa tarehe 20...

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Tulieni mgangwe maradhi si kitu. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tuijulize hao waliosimamia hilo waliapa kutii Katiba wanarudia uchaguzi, Tume ya Uchaguzi, Jecha alipofuta uchaguzi ule alifuta kwa aya ya ngapi ya kanuni na sheria za nchi hii?

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MBUNGE FULANI:** Akamuulize.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Akamuulize, nitawauliza ninyi mliomuweka. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, alivunja sheria za nchi, mtu anayestahiki kuweko gerezani, Magufuli anakwenda Zanzibar kwenye sherehe za Mapinduzi anakaa ubavuni kwake, anatujojea Wazanzibari. Tunasema haki itasimama kuwa haki hata mfanye nini hamtaipinga. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, anayepigwa, anayedungwa sindano kila mmoja anahisi maumivu anayopata mdungwa sindano lakini tako linalodungwa sindano ndiyo linaloathirika zaidi na maumivu ya sindano hiyo.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, mambo ya Zanzibar yanachukuliwa kiutani, mnalifanya jambo hili utani ndugu zangu. Ni wajibu tujue kwa mfano Jimbo langu la Konde uchaguzi uliopita CCM mlipata kura 700 mwaka huu mmepata kura 500.

Kwa mujibu wa sensa Jimbo lenye wananchi 50,000, CCM wako mia tano. Leo mnapofanya masihara ya kusema kwamba uchaguzi unarudiwa, kwa wana CCM 500 walioko kwenye Jimbo la Konde mnatutakia amani kweli ninyi? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliangalia jambo hili kwa ujumla wake. CCM katika Kisiwa cha Pemba hakuna, vurugu ikianza wale watu hata tukisema nyumba kumi zizunguke nyumba moja, haiwezekani hawatafika popote. Msiweke mazingira ya kuitia nchi ile kwenye joto la uhasama na uwaji. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu Nyerere aliwahi kunukuliwa katika miaka ya sitini akiwa Marekani au Uingereza, akisema kwamba: "Laiti angekuwa na uwezo angevihamisha visiwa vile vya Zanzibar vikawa mbali na Bahari ya Hindi kwa sababu anahisi vitakuja kutuletea shida hapo baadaye". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo halikuwezekana. Nawauliza CCM mliobakia, nia yenu sasa ni kutuua Wazanzibar wote ili lengo lile mlilolikusudia Wazanzibar wasiwepo duniani mlimitize? Kama lengo si hilo, kwanza kabisa nachukua nafasi hii nikiwa mwakilishi wa wananchi wa Konde na Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuziomba Jumuiya za Kimataifa, walioshuhudia ukweli na uhalali wa kazi waliyofanya Wazanzibar ya kuchagua Rais wanayemtaka walismamie hili kwa nguvu zao wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Watanzania wanahukumiwa kwa kukosa msaada wa mabilioni ya shilingi kwa kuwalinda wahuni wa Zanzibar wasiozidi kumi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge liliopita, kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja, alitamka yafuatayo naomba kunukuu, alisema na akamuomba Rais Kikwete, nia yake ya kuiona Zanzibar inabaki na ustawi ni wakati wa utawala wake tu. La pili..

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Ole wenu...

**SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha, naomba ukae.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Ally Keissy atafuatiwa na Mheshimiwa Shangazi, Mheshimiwa Bashungwa na Mheshimiwa Salma Mwasa. Mheshimiwa Ally Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ila na mimi nichangie hotuba ya Mtukufu Rais Mheshimiwa John Pombe Magufuli.

Hotuba ya Rais kwanza kutoa muda wa kuchangia ni kama vile tunapoteza muda, ile hotuba haina matatizo. Mwelekeo wake ni mia kwa mia hakuna mtu anaweza kuipinga. Ya kukazia ni yale mambo aliyoyaeleza mwenyewe tuyafuate na yatekelezwe haraka iwezekanavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuunda Mahakama ya Mafisadi ifanywe kwa haraka sana. Pili, wakati wa bajeti hapa Bungeni wanakuja Wakurugenzi, Wakuu wa Mikoa, Ma-RAS wanakuja kufanya nini? Hilo nalo liondoke. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kufuta Sherehe za Uhuru na ikiwezekana afute na Sherehe za Mwenge iwe hata mara baada ya miaka mitano. Tunabana matumizi, Mwenge kila mwaka unapita na tunapoteza pesa. Nimezungumza mimi Mwenge ukipita Wilayani kwangu siku tatu kazi hakuna. Siku ya kwanza wanalaki Mwenge, Ofisi za Halmashauri zinafungwa. Siku ya pili wanapokea Mwenge kwa hiyo wanakesha kwenye Mwenge. Siku ya tatu Mwenge ulipopita wanalala wamechoka. Sasa ndugu zangu ni uharibifu, ni lazima twende kama anavyosema kazi tu, hiyo ndiyo kazi tu. Hatuwezi kufanya sherehe wakati watoto wanalia, hawana madawati, dawa, viatu na chakula, tupunguze sherehe za ajabu ajabu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilishangaa sherehe za Mapinduzi Zanzibar wanapakia watu elfu moja kutoka Pemba. Sasa kulisha chakula watu elfu moja ni gharama wakati wananchi hawana hela? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tupunguze Majimbo yamekuwa mengi, Wabunge wamekuwa wengi gharama za kuendesha Bunge ni kubwa Rais alizungumza hapa.

**WABUNGE FULANI:** Sema.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Bunge linatumia gharama kubwa. Mabunge mengine ni watu ishirini na tano au watu kumi na tano. Ndugu zangu hatuendi namna hiyo. Twende na Bunge la kisasa, tumekalia kusema ma-DC wapungue, Wakuu wa Mikoa wapungue na Wabunge tupungue kutoptaka na idadi ya ukubwa wa Majimbo. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta Jimbo kama la Kwela kwa Mheshimiwa Malocha ukubwa wake ni sawa na Rwanda, anapewa pesa za kuendesha Jimbo sawa na Mbunge mwenye watu elfu mbili. Hapa uhalali uko wapi? Lazima twende na sera ya 'Hapa Kazi Tu' na kazi ianzie kwa Wabunge. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wanaunda mpaka vikosi vya michezo wanakwenda na ndege ya Rais na kurudi na ndege ya Rais, huu ni ubadhirifu wa hali ya juu.

**WABUNGE FULANI:** Sema.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani wakati wa bajeti wanatoka wataalam wa Nkansi wanakuja Dar es Salaam wanakaa wiki mbili, wao na madereva wao, gari sita, zinakuja Dar es Salaam eti bajeti. Karne ya 21, Namanyere ije ifanyiwe

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

bajeti Dar es Salaam! Mkurugenzi na kundi lake atoke Bukoba aje Dar es Salaam, atoke Tarime aje Dar es Salaam, ndugu zangu hii haiwezekani, kuanzia sasa bajeti zifanyike Wilayani itumike mitandao tu. Haiwezekani Madereva na Wakurugenzi wa kila Wilaya kuja Dar es Salaam kuchezea hela za Serikali wakati wananchi hawana maji, dawa wala barabara. Tunafanya sherehe kubwa kama nchi za Kiarabu, haiwezekani lazima tubanane, tule kwa jasho letu, hatuwezi kwenda kienyejienyeji. (Makofi/Kicheko)

Kisa kingine kuhusu madereva wa Serikali, madereva hawa wanapunjwa, madereva wa Mashirika ya Umma wanakuwa kama wako peponi madereva wa Serikali hawapati chochote. Hata akistaafu anapewa shilingi milioni mbili, itamtosha nini shilingi milioni mbili?

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wa marine service wa Lake Tanganyika, Lake Victoria, Lake Nyasa, hawaajiriwi, ni vibarua miaka yote. Hawana likizo, hawana insurance yaani wamekaakaa tu, wanaona bora wagongeshe meli watu wafe kwa sababu hawathaminiwi kabisa. Kwanza hii marine service ni shirika la nani, ni la umma kweli? Lazima anayehusika alichunguze hili shirika la marine service. Nimekutana na wafanyakazi wa Liemba wanasema Mzee hatuna hata likizo, insurance, mishahara duni, wakistaafu hawapewi chochote wakati TRA, Shirika la Nyumba wao ni kama wako peponi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu NASACO amezungumza Mheshimiwa Mbunge mmoja, turudishe NASACO i-control mali bandari. Leo kuanzia Bagamoyo mpaka Dar es Salaam bandari bubu nyangi. Wazanzibar ndiyo wamefanya pa kupitishia mali na kufanya huku Bara ndiyo soko. Tunaibiwa mchana mchana! Mali yote inatoka Zanzibar inapitia vichochoroni hawalipi ushuru. Zinaletwa mali za ajabu ajabu, sukari, mafuta na kila kitu. Wanastarehe kuinyonya Bara hawalipi ushuru, hiyo haikubaliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuweke mikakati anayekamatwa mara moja mali yake itaifishwe hamna kwenda Mahakamani. Pia chombo kinachopakia mali ambayo hailipii ushuru kitaifishwe, watashika adabu. Wote ambao wanahisiwa kwamba wanashirikiana na wafanyabiashara kutuibia, cha kwanza kabisa mali zao zinyang'anywe kabla ya kupelekwa mahakamani. Apewe form aulizwe hii mali umeipataje, akishindwa kujieleza anyang'anywe kabla hajaenda Mahakamani. Akienda Mahakamani, Mzee mlango chini anapita anafungwa miezi sita, anabakia anachezea ile mali. Kwanza mali yake inyanganywe mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mambo ya kuendelea kuleana yaishe sasa. Nimezungumza sana habari ya Namanyere, miradi ya maji wanahamishwa Wakurugenzi, Maafisa Ugavi na Wahandisi wa Maji, naomba majibu yakatumbuliwe Wilayani Namanyere kuna watu wameiba pesa. Kule kwa vile tuko karibu na DRC-Congo wafanya kama hamna Serikali, wanafanya mambo wanavyotaka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza hapa Bungeni, mtu anaandika gharama ya gari Namanyere Dar es Salaam gari tani kumi shilingi milioni kumi na mbili badala ya shilingi milioni tatu. Anaandika mabomba yameingia ndani gari tisini na nane milioni wakati bomba hakuna yaani gari hewa, mabomba hakuna, Serikali imelala usingizi. Tunataka tutumbue majipu tupeni idhini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya mbolea haya, mbolea hazifiki kwa wakulima wanaandika hewa tupu mpaka majina ya marehemu wanaandika. Hatuwezi kukubali safari hii, namwambia Waziri wa Kilimo, Kamanda wangu Mwigulu, anipe kibali nitembee kijiji kwa kijiji, nikague mimi mwenyewe simwamini DC, simwamini OCD, siiamini TAKUKURU maana ndiyo wamefanya njia za miradi yao. Nitatembea mwenyewe, Mheshimiwa Mwigulu nipe kibali

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

nikakague kijiji kwa kijiji, nyumba kwa nyumba kama mbolea au mbegu imefika. Serikali ya CCM inatukanwa ni kwa sababu ya Watendaji hawa, wamefanya miradi yao binafsi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu ni hayo, kuanzia sasa bajeti ijayo hakuna kuja cha Mkuu wa Mkoa, hakuna kuja cha RAS, hakuna bajeti za Wilaya kupangiwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tutamsikia Mheshimiwa Shangazi atafuatiwa na Mheshimiwa Bashungwa na Mheshimiwa Salma Mwasa. Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwanza, napenda kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Mlalo kwa imani yao kubwa ambayo imenifanya leo nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niungane na Wabunge wenzangu kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais kama alivyoitoa tarehe 20 Novemba, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na zoezi zima la utunzaji wa mazingira. Duniani kote sasa hivi tunazungumzia mabadiliko ya tabia nchi. Nadhani tutakubaliana sote kwamba hata haya matatizo ya maji tunayoyazungumza kutoka kwenye Majimbo tofauti yamesababishwa na namna ambavyo tumeharibu mazingira yetu. Tunapozungumzia utunzaji wa mazingira, tunamaanisha pamoja na utunzaji wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano katika Jimbo langu la Mlalo, tunaor Msitu wa Asili wa Shagayu mwaka 2012 uliungua moto takribani hekari arobaini na tisa lakini ni hektaki kumi na moja tu ndizo ambazo zimepandwa. Cha kusikitisha mvua za Desemba zimesababisha maafa makubwa kwa sababu ardhi imekuwa *loose*, imesababisha maporomoko na mafuriko katika kata za Mtae, Shagayu, Mbalamo na Mnazi. Hii yote ni kwa sababu ya uoto wa asili ambao umeondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na tatizo la uharibifu wa mazingira katika maeneo ambayo yanazunguka msitu wa Shagayu vilevile kuna tatizo la nguvu kazi. Msitu wa Shagayu unazungukwa na takribani vijiji kumi na tano lakini wako Watendaji wawili pekee na wanatumia pikipiki moja. Nimucombe Waziri wa Maliasili kuititia Serikali yetu sikivu ahakikisha kwamba anawasaadidha Watendaji ili waweze kufanya kazi hii ya utunzaji wa mazingira na misitu kwa ufanisi unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili nitajikita kwenye kilimo. Kama sote tunavyotambua kilimo ndiyo mhimili wa uchumi wa nchi yetu ya Tanzania. Kwa wakazi wa Jimbo la Mlalo na Halmashauri ya Lushoto kwa ujumla wake, ni takribani asilimia tisini na nane wanategemea kilimo. Tunaomba kuititia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais, Wizara inayohusika itufanyie yafuatayo katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto. Tunayo maeneo ya aina mbili, ya milimani ambapo tunaendesha kilimo cha mbogamboga na matunda katika kata za Lukozi, Malindi, Rangwi, Sunga na Shume. Kuna tatizo kubwa la wakulima kunyonywa pindi wanapovuna mazao yao kwa kutumia mtindo wa lumbesa. Lumbesa imekuwa ni sehemu ya unyonywaji wa wakulima, hivyo mwisho wa siku hawaoni faida ya yale mazao ambayo wanayavuna. Hivyo, naomba Bunge lako Tukufu, tuisimamie Serikali kuhakikisha kwamba kunakuwa na udhibiti wa ufungaji wa mazao kwa njia ya lumbesa. Tunatambua Wizara ya Viwanda na Biashara ina Wakala wa Mizani na Vipimo, tunaomba ilisimamie suala hili ili liweze kupatiwa ufumbuzi wa mwisho.

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni ukanda wa tambarare. Ukanda huu tunapata changamoto kwamba mvua zinazoshuka katika mabonde yetu na makorongo zinaelekeea bahaarini na maji yanapotea bure. Tunaomba Wizara ya Kilimo ije na mpango wa kutujengea mabwawa ili tuweze kuhifadhi maji yanayotiririka wakati wa msimu wa mvua. Maji haya yatasaidia wananchi kuendesha kilimo chenyeh tija kwa msimu mzima wa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika maeneo hayo tunayo mapori mazuri ambayo yakinumika vizuri kwa kuzingatia rasilimali ardhi, tunaweza tukaanzisha benki ya ardhi ambayo itakuwa ni kivutio kimojawapo kwa wawekezaji ambao wanatafuta maeneo ya kuwekeza. Pia kwa kutumia mipango ya ardhi, tunaweza pia tukawatengea wafugaji ambao nao pia wanapatikana katika eneo hili, wakapata maeneo ili waachane na kasumba ya kuswaga ng'ombe kila mahali. Tutakuwa tumewajengea uwezo wa kukaa mahali pamoja ambapo hata Serikali inaweza ikapata kodi yake stahiki. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia hotuba hii nzuri ya Rais lazima pia tufungue fursa mpya za kuwawezesha wananchi wetu. Jimbo la Mlalo, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto inapakana na nchi jirani ya Kenya. Tunao mpaka kule ambao unatumwa kwa ajili ya shughuli za kuitisha magendo pamoja na kuitisha Wasomali ambao wanapita kwa njia za panya. Niombi Serikali ione kwamba hii ni fursa ya kufungua kituo cha mpaka katika eneo la Kata ya Lunguza ili tuweze kufanya biashara na nchi jirani ya Kenya. Ni jambo jema kabisa kwamba ulinzi wa mipaka yetu ni jukumu ambalo halikwepeki lakini tukiweza kuweka kituo cha biashara na mpaka itasaidia wafayabiashara kuweza kwenda nchi jirani na pia itatusaidia na sisi kuza mazao yetu katika nchi jirani ya Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua suala zima la umeme vijijini. Tunashukuru umeme vijijini umesambazwa kwa kiwango cha kutosha lakini pia niombi Waziri anayehusika na nishati katika Jimbo langu bado kuna kata zaidi ya nne hazijaguswa na nguzo hata moja. Naiomba mamlaka inayohusika kupeleka umeme vijijini atambue Kata za Shagayu, Mbaramo, Mbaru na Sunga ili nazo ziweze kupewa kipaumbele katika usambazaji wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni rushwa. Mheshimiwa Rais ameanza vizuri, anapambana na majipu makubwa katika ngazi ya kitaifa. Kupitia Bunge lako Tukufu, naomba pia Waziri wa TAMISEMI, ashuke huku chini katika Halmashauri zetu, miradi mingi inafanywa chini ya utekelezaji uliokusudiwa. Huku nako kuna mchwa wanatafuna pesa, miradi haina tija, miradi haikamiliki kwa wakati, wanawazungusha Madiwani kwa sababu wanatumia uelewa hafifu wa Madiwani wetu walioko huko vijijini pamoja na Watendaji wa Vijiji. Naiomba Wizara husika ilisimamie hili kwa jicho la karibu zaidi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo naomba kuwasilisha, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Bashungwa, Mheshimiwa Salma Mwasa ajiandae atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda. Mheshimiwa Bashungwa hayupo, basi Mheshimiwa Salma Mwasa halafu Mheshimiwa Gulamali na Mheshimiwa Stella wajiandae. Mheshimiwa Salma Mwasa.

**MHE. SALMA M. MWASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuteuliwa kuwa Mbunge wa Mkoa wa Dar es Salaam. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kupewa ridhaa hii na wananchi pamoja na wewe Mheshimiwa Naibu Spika kuweza kuteuliwa kuwa Mbunge.

## Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais katika maeneo yafuatayo. Kwanza, napenda kuchangia katika eneo la elimu. Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli aliahidi kuboresha elimu katika maeneo mengi na kusema kwamba elimu ni bure. Labda kabla hatujafikia kwenye elimu bure, napenda kufafanua yafuatayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo mengi juu ya mpango huu wa elimu bure. Kwanza, miundombinu ni tatizo. Ni wazi idadi ya wanafunzi inaongezeka kwa kuwa elimu ni bure lakini haiendani na miundiombinu iliyopo katika shule zetu. Kwa mfano, katika Wilaya ya Kinondoni kuna jumla ya wanafunzi wa shule za msingi 152,000 na vyumba vya madarasa 1,500 hivyo tunapata wastani wa wanafunzi 98 kusoma darasa moja. Idadi hii ni kubwa sana na haiendani kabisa na udhahiri wa kauli hii kwamba elimu itaboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba upungufu wa madarasa katika Halmashauri ya Kinondoni ni jambo ambalo litadhoofisha suala hili la elimu. Halmashauri ya Kinondoni inahitaji vyumba vya madarasa 3,018 vilivyopo ni 1,656, pungufu ni 1,362. Inahitaji nyumba za walimu 452 zilizopo ni 280 pungufu ni 172. Ofisi za walimu ni 222 zilizopo ni 104 pungufu ni 118. Vyoo vya walimu vinahitajika 452 vilivyopo ni 280 pungufu ni 172. Vyoo vya wanafunzi vinahitajika 6,338 vilivyopo ni 1,382 pungufu ni 4,956. Maktaba nazo ni tatizo, zinazohitajika ni 1,446 zilizopo ni 32 tu pungufu ni 114. Kwa hali hii, sasa elimu itakuwa bure kama kutakuwa na mipango thabiti wa kuongeza miundombinu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Rais pamoja na kwamba elimu ni bure lakini aangalie tatizo la miundombinu kwani wanafunzi wengi wanarundikana kwenye darasa moja ambapo haitaleta ufanisi wa kutosha. Tukiangalia kwa mfano jinsia ya kike inapata shida sana kutokana na upungufu wa vyoo. Tunajua matatizo mengi ya watoto wa kike kwani wanahitaji kutumia vyoo safi. Hivyo basi, tatizo la miundombinu liangaliwe ikiwemo vyoo, madarasa na maktaba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite tena kwenye elimu ya sekondari hasa katika Wilaya ya Kinondoni. Kwa mujibu wa taarifa ya makabidhiano ya Serikali ya Awamu ya Tano Wilaya ina matatizo makubwa. Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ina shule za sekondari 137 tu kati ya hizo sekondari 48 tu ndizo sekondari za Serikali na 16 ni za mijini na 32 ni za vijijini. Hivyo basi, kuna upungufu wa nyumba za walimu, walimu wengi wanakaa mijini na kufundisha vijijini hali inayosababisha adha kubwa kwa walimu hao kutoka mijini kwenda vijijini na kudhoofisha elimu katika eneo hili la sekondari. Walimu hawa wanaishi kwenye mazingira magumu mno naomba tatizo hili liangaliwe. (Makofî)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inadhahirishwa katika taarifa hiyo, kati ya mwaka 2011-2014, wanafunzi waliofanya mtihani walikuwa 34,000 lakini waliofanya vizuri ni 11,000 na waliofeli ni 22,000 amba ni sawa na asilimia 63. Hivyo eneo hili liangaliwe tena katika kuboresha elimu ya watoto wetu ili tuweze kukidhi mahitaji yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha. (Makofî)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kabla sijaingia kwenye kuchangia, natamani niwakumbushe Wabunge wenzangu, maana nimeona wakitoa maoni kwamba Wapinzani tulitoka nje siku ya hotuba ya Rais. Waheshimiwa Wabunge, kuna njia nydingi za kufanya advocacy. Tunafahamu fika Bunge letu ni moja ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola, tunapotoka nje, ni pale ambapo umeona hoja ulizokuwa nazo aidha zimeskilizwa

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

au hazijasikilizwa. Hivyo kutoka nje siyo dhambi, ni dalili ya kuonesha hisia na mawazo ambayo tunayo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza kuzungumzia hotuba ya Mheshimiwa Rais, amezungumza mambo mengi na hata wengine wamesema kwa sababu hatukuwepo hatuwezi kujuu ni nini amezungumza. Sisi wote ni wasomi, tunasoma habari za Vasco da Gama lakini hatukuwepo na tunanakili kwenye mambo mbalimbali. Tumesoma mambo ya Hitler tunayatumia na hatukuwepo wakati wa uongozi wake. Vivyo hivyo habari hii itasomwa na sisi, itasomwa na watoto wetu wa sasa na vizazi vijavyo. (Makofii)

**MBUNGE FULANI:** Wafundishe mama.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Rais ilikuwa ni nzuri kama walivyosema wengine tatizo naloliona ni utekelezaji. Nitajikita katika mambo ya uchumi aliyoazungumzia hasa katika ukurasa ule wa 19. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika tunapozungumzia kukuza uchumi wa viwanda, nchi ambayo wasomi hatujawaandaa kuwa wabunifu, hatujawaandaa kuwaweka katika hali ya utendaji kazi, inakuwa shida.

Tunapozungumzia uchumi kilimo chetu ambacho watu wengi ni wakulima kwa asilimia kubwa, mazao wanayoyalima hatujajua ni jinsi gani ya kuwapelekea viwanda hivyo kwenye sehemu husika. Binafsi siamini kwa maana najua Magufuli ni mtu mmoja, mfumo wa Magufuli ndio uliooza, atawezaje kufanya kazi peke yake? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumza mengi na amezungumzia habari ya Katiba. Katiba ndiyo mama na mimi nilifikiri siku 50 za kwanza za Urais wake angeanza na Katiba. (Makofii)

**MBUNGE FULANI:** Sawa sawa.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ametamka na namnukuu, anasema, Katiba ni kiporo. Unapozungumzia kiporo kinaweza kikawa kizuri au kikakuharibu, kikawa kimechacha. (Makofii)

**MBUNGE FULANI:** Sawa kabisa.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Rais, Katiba ndiyo msingi wa kila kitu. Hata viwanda hivyo na huu uchumi tunaouzungumzia pasipo Katiba hiyo hatutaweza. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado naendelea kujikitia kwenye uchumi, amezungumzia wajasiriamali wadogo, amezungumzia wanawake na vijana ambao ni kundi kubwa sana lilio sahaulika. Tunawezaje kuwaunganisha wanawake hawa na viwanda endapo elimu yao ni ndogo? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, tunafahamu tuko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mheshimiwa Rais sijaona akizungumzia ni jinsi gani tutajua masoko haya ya watu wachache ambao ni wajasiriamali, wakulima wadogo, wataingiaje katika masoko haya na kuweza kufaidika na Jumuiya hii ya Afrika Mashariki?

## Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, sijaona akizungumzia muunganiko wa vijana kujajiri katika uzalishaji mali. Tunapokwenda kwenye viwanda, kama ni kilimo wanawezaje kujunganisha na viwanda hivyo anavyovisema? Ndiyo maana nasema nina wasiwasi na suala hili la viwanda analolizungumzia Mheshimiwa Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii imeelezea mambo mengi yanayofurahisha kwa kuyasikia lakini nafikiria, wakulima na hivyo viwanda anavyovisema, nikizungumzia Jimbo la Rungwe Magharibi kuna wakulima wa chai. Wakulima wale wanapunjwa, wanauzia makampuni binafsi kwa bei ndogo ambayo wawekezaji hao wanafanya kwa manufaa yao na kibaya zaidi wanashirikiana na watu walio katika madaraka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia viwanda, Kiwanda cha Chai cha Katumba ambacho kinaweza kutoa ajira kwa vijana wengi tumekisaidiaje kukipelekea ruzuku na kusaidia wananchi wa mji ule? Kuna viwanda vingi, Mbeya Mjini kulikuwa kuna ZZK, leo hii imekuwa ni ghala la kuwekeea pombe. Tunawezaje kusaidia vijana wetu kupata ajira? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni vyema Mheshimiwa Rais akatazama ni jinsi gani tutafufua viwanda vilivyokuwepo. Watu waliovifilisi pia wapo, tunawezaje tukarudisha vile viwanda vilivyouzwa kwa bei rahisi kwa watu ambao wamefanya maghala? Nadhani Mheshimiwa Rais angeanzia majipu ya aina hiyo kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sheria nyingi kandamizi kwa mfano Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, watoto wadogo tunasema wanapata mimba lakini sheria haiko sawa. Kabla hatujaenda kwenye mtazamo wa maendeleo lazima tubadilishe sheria kandamizi na nyinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sheria za kodi ndogo ndogo zinazowatesa wananchi tunazibadilishaje? Tunawaunganishaje wananchi kuingia katika uchumi na tukasema uchumi wetu umekua, jana tulikuwa tunaambiwa uchumi wetu umekua, kivipi? Tunawanishaje kukua kwa uchumi mnaozungumza Serikali na maisha ya mwananchi wa kawaida, tunayazungumziaje? Tuondoe siasa tuweze kufanya kazi. Magufuli anayo kazi kwa sababu watendaji wake ni walewale, pombe mpya kwenye chupa ya zamani. Namwonea huruma na sijaelewa atafanyaje kazi. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao vijana wengi ambao mpaka leo hii tumeanza kufanya marekebisho mbalimbali, kwa mfano gesi, je, Serikali imepeleka vijana hawa kusoma? Wako wachache tena wa wakubwa mnawapeleka Ulaya, kwa nini msichukue mtaalam kutoka Ulaya akaja kufundisha watoto kwa wingi hapa Tanzania? Kwa hiyo, kuna vitu vingi tunahitaji kurekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia amezungumzia haki, ataangalia makundi ya wazee, walemavu, hakuna haki kama hakuna Katiba bora. Tunaposema haki tunamaanisha ni lazima anayestahili haki apewe. Ndugu zangu wengi wamezungumza mambo ya Zanzibar na mengine lakini kuna haki ya watu wenye ulemavu wa ngozi (albino), hatuoni ni jinsi gani wakisaidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema haya, nafikiri kuna haja ya makusudi kabla hatujaendelea na safari hii tuenze na Katiba, tena siyo pale ilipochakachuliwa, tuenze na Katiba ya Warioba, tuanzie pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (Makofi)

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mwakagenda. Sasa tumsikilize Mheshimiwa Gulamali atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mheshimiwa Zainabu Mwamwindi na Mheshimiwa Savelina Mwijage.

**MHE. SEIF KHAMIS GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dokta John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, nipende kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo langu la Manonga na wananchi wote kwa ujumla wa Wilaya yetu ya Igunga, Mkoa wa Tabora kwa kunipa fursa hii adimu ya kuwawakilisha na kwa imani kubwa waliyoijenga juu yangu. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote leo tupo katika kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais na katika hotuba ile Mheshimiwa Rais alizungumza mambo mengi, mojawapo kubwa ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali, naomba ubadilishe *microphone*, hiyo uliyopo inaleta mwangwi, naomba uhamie *microphone* nydingine.

**MHE. SEIF KHAMIS GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais katika hotuba yake...

**MBUNGE FULANI:** Bado, hamia mbele.

**MHE. SEIF KHAMIS GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ile Mheshimiwa Rais alizungumzia mambo mengi na kwa uzito wa kipekee alizungumzia suala zima la utumbuaji wa majipu. Kwa kweli suala hili la utumbuaji wa majipu linaendana kabisa na suala zima la rushwa na ujisadi katika nchi yetu. Pia inaendana na kauli ya Mheshimiwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipozungumzia maadui wakubwa katika nchi yetu, ambapo alitaja maadui ujinga, maradhi, umaskini na rushwa hii sasa inaingia katika maadui wakubwa wanne. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili la kutumbua majipu Mheshimiwa Rais alisema sisi Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumuunge mkono na tumuunge mkono bila kujali itikadi ya vyama vyetu vya siasa. Tumuunge mkono kwa maana kazi hii si kazi ndogo, ni kubwa na alizungumza kwa machungu makubwa. Sasa mimi nitashangaa kama kuna watu watakuwa wanazungumza kwa kubeza hotuba ile ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini anavyokuwa anatumbua wakati mwingine utumbuaji wake hauangalii chama cha siasa. Majipu hayo aliyataja yapo ndani ya CCM lakini pia yapo kwenye vyama vya CHADEMA, CUF na wananchi wa kawaida. Maana yake mtu yeyote fisadi anajifichaficha kwenye vyama wakati mwingine hata nje ya chama ili mradi yeye aangalie namba gani atatuibia. Kwa hiyo, katika utumbuaji huu tushirikiane Wabunge wote kumuunga mkono katika jitihada ambao anazifanya. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii si rahisi na siyo ndogo. Kwa mfano, tumeweza kupata taarifa wengine tuliziona kwenye magazeti na kwingineko kuna baadhi ya watu walioenda kufanya hitilafafu katika ofisi ya TRA na kuiba computer na taarifa zingine. Maana yake nini? Yote hiyo ni kuficha taarifa ambazo tayari kuna watu ambao wanashiriki kwa namna moja ama nyininge kulihujumu Taifa letu. (Makofij)

## Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakati wanatumbuliwa na Mheshimiwa Rais anachukua hatua mbalimbali dhidi ya watumishi hawa maana matatizo haya ni kutokana na watumishi waliopo ndani ya Serikali kwa muda mrefu ambao kila zama zinazokuja wao wamo. Utawala wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere walikuwepo, utawala wa Mzee Mwinyi wapo, utawala wa Mzee Mkapa wapo, utawala wa Mzee Kikwete walikuwepo na utawala wa Mheshimiwa John Pombe wapo. Sasa katika kutumbuliwa naamini kabisa kuna wafuasi ambao wapo kwenye vyama vingine wanaumia jinsi ambavyo Rais anavyochukua hatua dhidi ya hao watapeli wetu na wahujumu uchumi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais katika hatua mbalimbali anazochukua dhidi ya watumishi ambao siyo waaminifu katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wasiseme hapa kwamba Mheshimiwa Rais anakiuka Katiba, sheria na taratibu mbalimbali hapana tumuache Rais achukue hatua dhidi ya watu hawa ambao wanatuhujumu katika Taifa hili. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, hujuma hii athari yake inalikumba Taifa letu na ndiyo maana kila siku tunakuja na kauli mbiu za kuhakikisha kwamba tunawakomboa Watanzania kutokana na hali ngumu ya maisha walijonayo. Matatizo haya yapo na yataendelea kuwepo na sisi viongozi tutamaliza miaka mitano tutaenda kuomba kura tena, maana yake matatizo mpaka tutakufa hatutaweza kuyamaliza. Kila siku ni lazima kuangalia tunapunguzaje hizi kero zilizopo. Ndiyo maana tunaomba kura kila baada ya miaka mitano mtuchague ili tupunguze matatizo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika sera ya Mheshimiwa Rais ya 'Hapa Kazi Tu' katika hotuba yake ukurasa wa 13 amesema kwamba Serikali ya Dkt. Magufuli itakuwa ya viwanda. Viwanda hivi tunavizungumza hapa vilikuwepo toka enzi ya Mwalimu lakini vingine vilikufa toka enzi hiyo ya Mwalimu, vingine vilikufa enzi ya Mzee Mwinyi na vingine vilibinafsishwa enzi ya Mzee Mkapa na vingine vilibinafsishwa enzi ya Kikwete na watendaji wengine ambao wapo dhama zote na wamefanya kazi miaka yote hii na katika ubadhirifu huu wameshiriki kwa namna moja au nyingine. Kwa hiyo, katika uchukuaji hatua, tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais aendelee kuyatumbua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili suala la viwanda, tuwaombe Mawaziri washirikiane na Rais kuhakikisha kwamba vile viwanda vilivyokuwepo awali tuanze navyo hivyo kwanza. Tujue status yake, tujue tunavezaje kuanza na hivyo kabla hatujaanza kufungua viwanda vingine. Kwa mfano, kwenye Jimbo letu la Manonga tulikuwa na ginnery ya pamba inaitwa Manonga Ginnery ambayo ilikuwa inasaidia na ku-stimulate wananchi wa maeneo yale kulima kwa wingi zao la pamba. Matokeo yake toka kubinafsishwa kwa kiwanda kile hata uzalishaji wa zao la pamba umepungua. Mwisho wa siku zao hili litapotea maana wananchi sasa wanakwenda kulima mazao ya chakula badala ya biashara na mazao ya biashara yanasadidua kuongeza pato la nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine katika hotuba ile ya Mheshimiwa Rais alizungumzia matatizo makubwa ya maji ambayo wananchi tunayo. Kila Mbunge humu anazungumzia tatizo la maji, hilo ni kweli ni tatizo sugu katika nchi yetu na tunatambua tuna vyanzo vingi vya maji. Niiombe Wizara ya Maji kwa sababu Mheshimiwa Rais anakwenda na kasi ya viwango na yenyewe ikimbie haraka, tuchimbe mabwawa kwenye maeneo ambayo ni makame ili yasadie kutunza maji kwa kipindi chote cha masika na kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Choma Chankola, Tarafa ya Manonga, walikuja watu wa Kanda ya Magharibi kufanya survey wakatuhakikishia watachimba bwawa kubwa ambalo

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

litahifadhi maji na kilimo cha umwagiliaji kitafanyika. Ni miaka mitatu toka wamekuja wale wataalam hatujasikia lolote.

Tunaiomba sasa hii kasi ya Mheshimiwa Rais na hawa waliopo chini kwenye Wizara waendane nayo sawa, wasipishane. Siyo Rais anakimbia wao wanatembea, hatuwezi tukalikubali na kuliunga mkono na tutalisema hili kuhakikisha kwamba na wao wanakimbia ikiwezekana wakimbia kuliko Rais. Tena Rais ifike hatua awaambie punguzeni kasi maana ameshawazidi kasi kwa mbali sana. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais pia aliahidi kusaidia wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu. Kwenye Jimbo la Manong, kwenye Kata ya Mwashiku, Ntogo na Ngulu kuna wachimbaji wadogo wadogo. Tunaiomba Wizara pia iangalie namna gani itaweza kuwasaidia hawa wachimbaji kuhakikisha kwamba wanajikwamua kutokana na hali ngumu ya maisha waliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote, kuna mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria ambao unatoka Mwanza kupitia Nzega unaenda Tabora lakini ukifika Nzega unakwenda Igunga, ukiwa unakwenda Igunga unapita pale katikati panaitwa Ziba ambako ni junction ya kwenda makao makuu ya Tarafa ya Manonga na Tarafa ya Simbo. Tuliahidiwa kwamba yale maji yataweza kufika katika maeneo yale. Tunaiomba Wizara maana tuliona tayari fungu lilishatengwa kwa ajili ya kazi ya kupeleka maji lakini leo kwenye taarifa zetu inaonekana kwamba usanifu utaanza mwaka 2016/2017. Niombe Wizara ipitie upya taarifa zao ili kuhakikisha kwamba...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali muda wako umeisha, naomba ukae tafadhali.

**MHE. SEIF KHAMIS GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafsi hii. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella Ikupa Alex atafuatiwa na Mheshimiwa Zainabu Mwamwindi, Mheshimiwa Sevelina Mwijage, Mheshimiwa Japhary Michael, Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali na kama muda utakuwepo tutamsikiliza Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani. Mheshimiwa Stella Ikupa Alex tafadhali.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie Kanuni ya 60(11), kwa idhini yako naomba nizungumze nikiwa nimekaa.

**NAIBU SPIKA:** Endelea Mheshimiwa.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha mahali nilipofika, kwa kupitia watumishi wake mbalimbali ambao wamekuwa wakinombea mchana na usiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda niwashukuru sana wazazi wangu Alex na Anitha Mwabusega kwa jinsi ambavyo walinilea kwa mapenzi makubwa na hata kunifikisha mahali nimefika leo. (Makof)

## Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitakuwa ni mpungufu wa fadhila nisipowashukuru mama zangu UWT, Mkoa wa Dar es Salaam, ambao wameniwezesha kufika mahali nimefika leo pamoja na mama zangu UWT taifa. Mungu awabariki sana. (Makofii)

**MBUNGE FULANI:** Amen

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa hotuba yake nzuri ambayo aliitoa katika Bunge hili Tukufu tarehe 20 Novemba, 2015. Hotuba hii ilijitosheleza kila eneo kwa maana iligusa maeneo yote ya Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumpongeza maana hotuba yake imeanza kutekelezeka haraka sana. Tumeona matunda mengi ambayo yametokana na hotuba hii, tumeona jinsi ambavyo matumizi ya siyo lazima yamepunguzwa, tumeona jinsi ambavyo mapato yameongezeka lakini pia tumeona jinsi ambavyo majipu yameendelea kutumbuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa jinsi ambavyo imeweka uwakilishaji kwa kundi la watu wenye ulemavu. Uwakilishaji ni wa jinsi gani? Ni ule uwakilishaji wa kutupatia nafasi kubwa za ngazi ya juu ikiwemo Unaibu Waziri pamoja na Unaibu Katibu Mkuu. Mungu awabariki sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaongea mengi, naomba nijikite kwenye ukurasa wa 9 ambapo Mheshimiwa Rais aliongelea makundi maalumu kwa kusema kwamba haki za makundi maalumu zimekuwa zikikiukwa, walemaru, wazee, wanawake na watoto na kadhalika. Nitajikita kuchangia kwa upande wa watu wenye ulemavu pamoja na wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli kumekuwa na ukiukwaji wa haki za watu wenye ulemavu ikiwemo haki ya kuishi. Tumeshuhudia jinsi ambavyo wenzetu wenye ulemavu wa nguzu wamekuwa wakitendewa vitendo vya ukatili ikiwa ni pamoja na kukatwa viungo vyao na kuuwawa. Ni juzi tu hapa mwezi Disemba kuna mama mmoja kutoka Tanga alikatwa kidole, ni mtu mwenye u-albinism. Kwa kweli ni vitendo ambavyo havistahili na ni vitendo ambavyo kiukweli vinatakiwa kupigiwa kelele sana. Pia Watanzania ambao muda huu wanatutazama wavikemee kwa hali na nguvu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho kimekuwa kikikiukwa kwa upande wa kundi hili ni haki ya ajira. Kuna sheria kabisa ambayo inawataka waajiri wawe na asilimia tatu ya wafanyakazi wao ambao ni watu wenye ulemavu lakini sheria hii imekuwa haitekelezeki. Niombe Serikali Tukufu ya Chama cha Mapinduzi ifuatilie utekelezaji wa sheria hii kwa kufuatilia kila mwajiri na kuhakikisha wana asilimia hii ambayo imewekwa katika sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo halitekelezeki ni haki ya habari. Kwa upande wa wenzetu ambao ni viziwi wanahitaji kupata habari. Kwa mfano tu wa haraka haraka na mfano halisi hata sisi Wabunge wakati tunaendesha kampeni zetu, ni nani ambaye katika kampeni zake alikuwa akizunguka na mkalimani wa lugha ya alama, hayupo! Mtu huyu unategemea akupigie kura, atapigaje kura na wakati hajajua kitu ambacho umekiongelea katika sera zako? Kwa hiyo, hili pia ni jambo la kuangalia sana. Pia ni endelee kuiomba Serikali ya Chama changu cha Mapinduzi kutoa agizo kwa wamiliki wa vyombo vya habari ikiwemo television waajiri haraka sana wakalimani wa lugha za alama. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho pia napenda kukiongelea ni haki ya elimu kwa watu wenye ulemavu. Tunashukuru kwamba tuna shule chache lakini hazitoshelezi kwa sababu

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

si wazazi wote ambao wanauelewa wa kuwapeleka watoto katika shule hizi. Kwa hiyo, mimi niombe Serikali zilezile shule za kawaida iziboreshe kwa kuweka mazingira ambayo yataweza kufikika ama yatakuwa ni rafiki kwa wanafunzi wenyewe ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niongelee suala la uandaaji wa shughuli za Kitaifa. Katika uandaaji wa shughuli za Kitaifa pia umekuwa hauzingatii mahitaji maalumu. Naomba nitolee mfano mmoja ambao mimi mwenyewe niliguswa. Samahani, ilikuwa ni kipindi kile cha msiba wa Mheshimiwa Celina Kombani, tulipofika mahali pale hakukuwa na mkalimani wa lugha za alama, ufinyu wa nafasi lakini ule mwili uliwekwa juu inakubidi upande kitu ambacho mimi niliogopa naweza nikasukumwa kidogo nikaanguka wakati nilihitaji kwenda kumuaga yule Mheshimiwa. Kwa hiyo, naomba panapokuwa pana uandaaji wa shughuli za Kitaifa hivi vitu vizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda niongelee haki za wazee. Tumeona wazee wetu ambao wamestaifu miaka ya nyuma wamekuwa wakilipwa pensheni ndogo sana. Kwa hiyo, niioombe Serikali iangalie ni jinsi gani ambavyo inaweza ikwapandishia pensheni wastaifu hawa ili waweze kufaidi matunda yao ya utumishi wao katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofij)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zainabu Mwamwindi atafuatiwa na Mheshimiwa Savelina Mwijage.

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, tingatinga letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nianze kama Waheshimiwa Wabunge wenzangu walivyoanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mungu mwenye rehema ambaye ametuwezesha leo na mimi Zainabu Mwamwindi kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano nawakiilisha wazazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Ni hotuba ambayo ilikuwa ina mashiko mazuri na makubwa sana, ni hotuba ambayo ilisheheni kila kitu na ni hotuba ambayo siyo tu kwamba sisi Wabunge wa CCM ndiyo tunaipongeza au tunasema kwamba ilikuwa ni hotuba nzuri bali ndiyo ukweli uliojitokeza siku Mheshimiwa Rais alipokuja kutufungulia au kutuzindulia Bunge letu la Jamhuri ya Muungano. Hotuba hii siyo sisi tu, hotuba hii kuanzia wale wengi wanaoishi vijiji waliipongeza sana. Pia wasomi baadhi yao waliipongeza hotuba hii lakini na wale ambao wanaishi mijini nao pia waliipongeza hotuba ya Mheshimiwa Rais. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenye macho haambiwi tizama na mwenye masikio haambiwi sikia, Mheshimiwa Magufuli Watanzania kumchagua hatukufanya kosa. Pia niseme tu kwamba Watanzania kukichagua Chama cha Mapinduzi ndiyo usahihi wenyewe, ni chama ambacho wamekiona kina sera nzuri, llani inayotekelzeza lakini pia ndiyo Chama kinachosema ukweli, hilo ni sahihi kabisa. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Katika hotuba yake, aliongea kwa uchungu na Wabunge wengi wamechangia sina sababu ya kurudia lakini niseme yako mambo muhimu ambayo alikuwa ameyakazia sana, alikazia sana suala la maji. Kule Tosamaganga, Kata ya Kalenga ambayo ina vijiji vitatu na vitongoji sita ule mradi wa maji

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

ni wa mwaka 1974 miundombinu imechakaa. Nitoe ombi kwa Serikali ya CCM, Serikali sikuvi, Serikali ambayo ina huruma na wananchi isaidie mradi huu. Tosamaganga ni sehemu ambayo imetoe viongozi wengi sana ambao wanalitumikia taifa hili. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1974 wakati mradi wa maji unawekwa kule Tosamaganga ulizingatia uwepo wa watu waliokuwepo kwa wakati ule. Sasa Tosamaganga imekuwa na idadi kubwa sana ya watu hivyo maji hayatoshelezi kutohana na wananchi kuongezeka kwa kiwango kikubwa. Tosamaganga pia ina shule nyngi sana ambazo watoto wanasoma pale. Imezungukwa na mito lakini kuna mlima mkubwa, watoto wanashuka kwenda kufuata maji kule wengine wanatumbukia. Hivi karibuni amekufa mtoto mmoja wa kiume anaitwa Onesmo kwa sababu alikuwa amekwenda kufua siku ya Jumamosi, kwa bahati mbaya nguo yake ikateleza kwenye maji wakati anaifuatilia akazama kwenye maji. Kwa hiyo, bomba za Tosamaganga pamoja na vijiji vyake maji hayatoki kabisa. Kwa hiyo, namuomba Waziri wa Maji uiangalie Tosamaganga kwa jicho la huruma, maji yale hayatoshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikuombe Mheshimiwa Waziri, kule Unyangwila na Irangi, wale watu wameanza wao kwa nguvu zao kuchimba mtaro kwa ajili ya kutafuta maji na wameshafikisha kilomita tatu na nusu lakini hawajui watapata wapi mabomba na maji kwenda kuyafikia ni kilomita sita na nusu. Mheshimiwa Waziri nakuomba katika ufalme wako iangalie Tosamaganga na Kalenga. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati akiwa Mbunge Marehemu Dkt. William Mgimwa, alikuwa ameahidi kupeleka gari la wagonjwa katika Hospitali ya Ipamba, ni Hospitali Teule ya Wilaya ya Iringa. Hospitali ile ni kubwa kwani inatoa huduma kwa wananchi wanaotoka maeneo mbalimbali katika Mkoa wa Iringa na pengine hata Mikoa ya jirani lakini cha kusikitisha hakuna gari la wagonjwa. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Afya, hebu tazama Hospitali Teule ya Ipamba ili waweze kupatiwa gari la wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara yangu ya kwanza leo nimeshuhudia Mbunge akilidanganya Bunge Tukufu. Mbunge wa Iringa Mjini amesimama hapa kwa kujiamini kabisa, akizungumzia habari ya Iringa Mjini yeye kama mwakilishi wa wananchi wa Iringa. Amezungumzia mradi wa maji wa Iringa Mjini na kujidai kwamba Iringa Mjini maji yanapatikana kwa kiwango cha asilimia 98 lakini akasema Iringa kuna barabara za lami, akaenda mbali zaidi akasema taa Iringa Mjini zinawaka bila shida barabarani. Mheshimiwa Mbunge amelidanganya Bunge lako Tukufu. Naomba tumwogope Mungu, Mchungaji Msingwa ni Mchungaji na nafikiri ana hofu ya Mungu lakini anapozungumzia vitu hata anaposema tunajikomba ndio tuna haki sisi tumsifu Rais wetu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iringa Mjini mpaka sasa maji ni asilimia 95, ni mradi ambao ulianzishwa na Mheshimiwa Monica Mbega wakati wa kipindi chake na hata wakati wa uzinduzi wa mradi huu alikuja Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne. Mbunge wa Iringa Mjini, Mheshimiwa Peter Msingwa hakushiriki katika uzinduzi wa mradi huu kwa sababu mradi huu alikuwa hautaki na hakuukubali. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili la barabara vilevile Mheshimiwa Msigwa amezikuta barabara za lami zikiwa tayari zipo. Ni mradi uliotoka Serikali Kuu na siyo yeye. Taa za barabarani ni package ya mradi wa barabara...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

## Nakala ya Mtandao (Online Document)

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umeisha Mheshimiwa Mwamwindi naomba ukae. Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Kubenea naomba mkae tafadhali, muda wetu umeenda sana. Mheshimiwa Savelina Mwijage tafadhali.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kuweza kurudi ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nakishukuru Chama change, Chama cha Wananchi CUF kuweza kuniamini na kunirudisha hapa Bungeni. (Makofii)

**MBUNGE FULANI:** Hongera mama.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namtaka Waziri wa Mawasiliano, kesho atuletee majibu hapa ni kwa nini wamezuia TV kuonesha Bunge. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage, hilo suala unalolizungumzia lilishaombwa kama mwongozo na Mheshimiwa Pareiso na itatolewa maelezo. Kwa hiyo, endelea kuchangia hotuba tafadhali.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia hotuba ya Rais, watu wengi hapa wanabeza mchango wa Wabunge kuhusu Zanzibar. Tukumbuke kipindi cha nyuma Zanzibar ilivyokuwa na vurugu leo hii badala ya kuomba Mwenyezi Mungu kuepusha balaa la siku za nyuma tunaendelea kubeza na Wazanzibari wenyewe wanajua matatizo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiendelee kubeza mambo ya kisiasa, tusije humu kuwasafisha au kuwapongeza watu kwa mambo ya kutuletea matatizo kama yaliyotokea siku za nyuma. Watu walikufa na walipoteza mali zao nyingi. Kwa hiyo, nawaomba tushirikiane kupiga magoti kumrudia Mwenyezi Mungu tuweze kuiombea Zanzibar iweze kuwa na amani. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Marais wengi wanavyoingia kwenye kampeni wanawalaghai watu wa Kanda ya Ziwa, nitaanza na usafiri wa majini. Wakati wa uhuru mwaka 1961, wakazi wa Mkao wa Kagera na Kanda ya Ziwa tulikuwa na chombo cha usafiri kinachoitwa MV Victoria, MV Kabilondo, MV Usoga na MV Serengeti. Kila Rais kuanzia Rais Mkapa walisema wataleta meli mpya, meli za kusafirisha mizigo na ya kusafirisha Watanzania amekuja Jakaya hivyo, amekuja Magufuli hivyo. Tunaomba msiwe mnalaghai kwa kuahidi kitu ambacho hamtaweza kukifanya. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naelekea kwenye huduma ya afya. Mkao wa Kagera una zaidi ya watu milioni 2.8. Hivi sasa Serikali ya Mkao wa Kagera inamiliki hospitali tatu na vituo vya afya 25, zahanati 207, mashirika ya dini yanaongoza kwa kutoa huduma ya hospitali ili kuwasaidia wananchi. Serikali inajivunia hizo hospitali kwamba ni za Serikali. Hospitali ya Rubya, Isingilo - Nyakanga, Bugeni ni za dini. Tunaomba kuanzia sasa na wakati huu wa Magufuli, Hospitali ya Mkao wa Kagera ipatiwe CT-Scan na Madaktari Bingwa kwa sababu haina Daktari Bingwa wala vifaa. Leo hii anasema ataboresha hospitali, aboreshe kwanza vifaa ndiyo ajenge hiyo Hospitali ya Mkao na Wilaya anayotaka. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda kwenye kilimo. Mkao wa Kagera tuna zao la kilimo cha migomba. Mgomba ndiyo zao kuu la biashara na zao la chakula. Iilitolewa taarifa kwamba zao hilo lina ugonjwa unaitwa myauko. Mpaka sasa hivi wananchi wa Mkao wa Kagera wana

## Nakala ya Mtando (Online Document)

njaa kubwa sana kutokana na ugonjwa huu wa migomba lakini Serikali haioni umuhimu wa kuwasaidia kuwapelekea wataalamu ili kutibu ugonjwa huo ili waendelee kulima migomba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1952, Serikali ya Kikoloni iliweka sheria ya kuwazuia kulima migomba bila kuweka mbolea ya chengachenga. Mwaka 2006 katika Kata ya Izigo, Wilaya ya Muleba, Mkoani Kagera ndiyo waliotangulia kupata ugonjwa huo wa mnyauko ukitokea nchi ya jirani Uganda sasa hivi umeenea Mkoo mzima wa Kagera na watu wanalia na njaa. Kipindi kilichopita mkungu mmoja ilikuwa Sh.3,000, Sh.5,000 sasa hivi umefika Sh.16,000 mpaka Sh.30,000. Naiomba Serikali inayosema Kilimo Kwanza ianze kwanza kuwaboreshea wakulima wa Mkoo wa Kagera kwa kuwaletea wataalamu kuboresha zao hilo ili waweze kupata kipato cha kuuza ndizi Uganda na nchi nyingine jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naharakisha ili muda wangu usiishe, naenda kwenye elimu, wanasema elimu ni bure. Ukiangalia elimu ni bure lakini Mwalimu anayekwenda kufundisha elimu bure analala wapi? Darasani watoto wamejazana hawana mahali pa kukaa atapaje akili ya kuweza kushinda darasa la saba au form four. Kwanza, boresha shule zilizopo, Walimu wapate sehemu ya kulala, tupate maabara za shule, wanafunzi wapate mahali pa kukaa na kusoma vizuri na Walimu wafundishe vizuri. Mwalimu hawesi kuacha mtoto ndani ya familia anakosa chakula akapata akili ya kumfundisha shuleni na anafika darasani mtoto anasinzia kwa ajili ya kukosa chakula. Kwanza, tuboreshe kitu kilichopo ndiyo baadaye tuje kusema watoto wanasoma bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona fomu ya watoto wanaoingia form one, ukiangalia michango wanayoitoa ni mingi sana. Kama Serikali imekuwa tayari kuwasaidia wanafunzi ili wasome bure waanze kwenye chakula. Mtoto akiingia darasani ana njaa atashindwa kuendelea kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali, watumishi walioajiriwa wanakaa katika Halmashauri miaka zaidi ya thelathini wanafanya kazi kwa mazoea. Juzi hapa mimi na Mheshimiwa Lwakatare tumekwenda kutoa misaada katika zahanati ambazo wanawake wanajifungua, kwa moyo safi tu lakini akatokea DMO akasema hospitali zote hazina shida ya beseni na unaangalia kila mwanamke anabeба beseni wakati huo unaona Wabunge wengine wa CCM wanatoa misaada inapokelewa. Hii ni kutokana na kufanya kazi kwa mazoea kwa miaka 30 yuko kwenye Halmashauri moja habadilishwi. Tunaiomba Serikali mfanyakazi yeoyote akikaa miaka mitano inatosha ahamishiwe kwenda sehemu nyingine, siyo kufanya kazi kwa mazoea inaonekana pale ni nyumbani na anachokifanya anaamua mwenywewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda kwenye ajira, vijana wamejajiri kwenye pikipiki lakini wananyanyasika, wanapigwa, wananyang'anywa pikipiki na Maaskari halafu wanaziwa na hili tumeshuhudia. Kama kijana huyo hana elimu ya kuendesha pikipiki anaendesha kwa ajili ya njaa na kutafuta ajira ya kulazimisha. Naiomba Serikali itoe elimu kwa vijana ambao wanaendesha bodaboda ili waweze kupata kipato chao kwa sababu ajira Serikalini hamna, inasema ajira, ajira, lakini ajira haipatikani. Kama hatuna viwanda, kama hatuna masoko makubwa, hakuna ajira yoyote vijana wataendelea kupigwa na Maaskari.

Mheshimiwa Naibu Spika...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (Makofii)

## Nakala ya Mtando (Online Document)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Japhary Michael atakuwa ni wa mwisho kuchangia kwa sababu ya muda tutatakiwa kumaliza kwa wakati. Mheshimiwa Jafari Michael au hayupo.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipo lakini hukuniambia mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Naitwa Japhary Michael, Mbunge wa Jimbo Moshi Mjini. Nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wa Moshi Mjini ambao wamenichagua kwa kura nyingi sana pamoja na Madiwani wangu kuongoza Halmashauri ya Manispaa ya Moshi. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo machache ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kabla ya hayo, nataka nitoe observation yangu niliyoiona katika kuchangia huku. Ukiangalia ndani ya Bunge hili utadhani kama vile Serikali tunayoizungumzia leo imeanguka jana, haikuwepo katika nchi hii kwa hiyo, matatizo yaliyopo hawatusiki nayo. Kwa bahati nzuri kwa zaidi ya miaka 50, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa matatizo ya Taifa hili kwa vyovypote vile yanawagusa kwa kiwango cha kutosha kabisa. Kwa hiyo, naona kama vile kuna watu wanaomba toba, sasa ni wajibu wa wanaoombwa toba kukubali au kukataa. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye hotoba ya Rais pale anapozungumzia habari ya ushirikiano wa Serikali yake na Halmashauri. Nimekuwa Diwani na nimekuwa Meya kwa miaka kumi sasa hivi. Tunapoelekea niiombe sana Serikali ijitahidi kuishi katika dhana ya decentralization, ya kupeleka madaraka kwa wananchi, izipe mamlaka ya kutosha Halmashauri za Wilaya, Majiji na Manispaa kama sheria inavyosema kwamba madaraka yatatoka kwa wananchi. Hali inavyoendelea, Halmashauri zimekuwa zikiongozwa kwa miongozo, waraka, maagizo na kusababisha leo hii watendaji wengi wa Halmashauri na Madiwani wanakosa creativity (ubunifi). Kwa hiyo, wanajikuta siku zote wataishi kwa maagizo ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais, Ofisi ya Waziri wa TAMISEMI na matokeo yake kiukweli mambo mengi yanaenda ndivyo sivyo. Kama tunataka wananchi watumikiwe vizuri na ndivyo alivyoelekeza Mheshimiwa Rais, ni vizuri mamlaka zile zipewe power inayostahili ambayo itaweza kuwafanya waweze kuzitumia rasilimali za Taifa vizuri na kuzifanya ziwe na ufanisi na tija kwa wananchi wa taifa hili. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata maslahi ya Madiwani, Wenyeviti wa Mitaa, huwezi kumwambia Mwenyekiti wa Mtaa hana chochote lakini anaithwa Mheshimiwa, ndiye anatakiwa apokee watu waliogombana kwenye ndoa zao, ndiye anatakiwa apokee kila tatizo halafu hapati chochote ambacho kimeelekezwa na Serikali, mnaziachia Halmashauri ziamue zenyewe wakati hazina hata uwezo wa kuijendesha zenyewe. Ni vizuri Serikali iliangularie hili kwa ndani sana namna gani itasaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ziweze kuijendesha vizuri. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie suala la utalii. Jimbo naloongoza lipo karibu sana na Mlima Kilimanjaro. Kama tunataka kuuendeleza utalii ili tuweze kukuza uchumi wa nchi hii ambapo tunafikiri kuwa na mawanda mapana katika viwanda, ni vizuri tujitahidi kuuboresha utalii na hasa tuutumie vizuri Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Uwanja wa Ndege wa Moshi umekuwa kama gofu lakini hautumiki vizuri. Uwanja huu ungeweza kusaidia watalii wanapotoka kwao waje moja kwa moja pale na uongeze mapato na uchumi wa Mji wa Moshi lakini pia ungesababisha Mji wa Moshi ukue kwa haraka. Mji wa Moshi umekuwa kwa taratibu mno kama vile siyo Mji Mkongwe na wa zamani. Naomba sana Serikali ilione hili kwa mapana yake.

## Nakala ya Mtando (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la rushwa na ujisadi ambalo limezungumzwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais na kwa sauti kubwa sana. Naomba kwa dhati kabisa, katika Bunge liliopita wakati linamaliza muda wake, Mheshimiwa Halima Mdee, alileta kwenye Bunge hili Tukufu hoja ya udanganyifu uliofanywa na taasisi fulani kupitia RITA wa kughushi saini za marehemu na wakabadiisha Bodi ya Wadhamini wa taasisi hiyo ili wapore eneo ambalo Halmashauri ya Manisapaa ya Moshi imelikalia zaidi ya miaka 20. Hoja hiyo imekuja hapa lakini Mbunge aliyeleta hoja ile hakupewa majibu na leo watu wale wamebarikiwa, wamekabidhiwa udhamini wa ile taasisi na tayari kiwanja kile kimeshachukuliwa na hiyo taasisi na kimeuzwa kwa watu wengine. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza habari ya ujisadi, lazima tumsaidie Rais, seriously. Tukizungumza mambo kama hatuko seriously tutakuwa tunazungumza mambo yaleyale, kwa sura zilezile na matokeo yatakuwa ni yaleyale. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na jitihada za kutosha kwa yale ambayo tunataka kuiaminisha jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la hali ya watu wa chini ambalo kimsingi ukiliangalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais limeongelewa kwa mapana yake na amelenga zaidi huko, hali ilivyo na kwa namna utekelezaji wake unavyoendelea watu wa chini siyo muda mrefu wataichukia Serikali. Kwa sababu inaonekana kiukweli, kumekuwa na matamko mengi ambayo yanawaumiza watu wa chini. Ni lazima tukubaliane kuna mambo ya msingi ambayo hatuna nafasi ya kuyafumbia macho, hatuwezi kufumbia macho uhalifu wa aina yoyote katika Taifa hili wa ujisadi na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kuna mambo yanahitaji huruma ya kawaida tu hasa ikizingatiwa kuwa Serikali ni ileile kwa muda wa miaka 50 na mambo mengine mmeyasimamia ninyi leo mnapokwenda bila jicho la ubinadamu mnawafanya wananchi wasiwaelewe na hasa wa hali ya chini. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, unapokwenda ukavunja nyumba ya mwananchi wa hali ya chini ambaye pato lake ni la chini mno wakati miaka 50 amekaa katika eneo hilo ndani ya utawala wa chama hichohicho, ni hatari sana. Ni lazima tujitahidi kuwa watu wenye huruma, wenye ubinadamu kama ambavyo hotuba ya Mheshimiwa Rais imejaribu kuonesha kwamba tujielekeze huko, tuwahurumie hawa watu wa chini. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini namna gani tunaweza kuwasaidia watu wa chini kama Wamachinga na wachuuzi mbalimbali, lazima tuone kwamba hakuna Taifa lolote duniani watu wamekuwa matajiri bila kuanza katika hiyo primitive accumulation lazima tujitahidi kuona tunawasaidiaje watu hawa. Alichotuagiza Rais ni kwamba watendaji wababilishe spirit na attitude zao, wawe na tabia ya kuwa wabunifu ni namna gani watengeneze mazingira rafiki kwa hawa watu wa chini kuweza kusaidiwa na sio wawe watu wa kuwabugudhi na kuwaumiza, ni lazima hilo lifanyike kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri anapokwenda kuongea na wananchi akaongea kibabe ni hatari wakati akienda kuomba anaomba kiungwana na kama binadamu. Namna mnavyoomba kura ni namna hiyohiyo mnatakiwa muwatatumikie wananchi ili waone kwamba siku zote mko nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Serikali, lazima sisi wanasiwa maana Mawaziri hamvui vazi la siasa ninyi bado ni wanasiwa, mnapozungumza na wananchi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

## Nakala ya Mtando (Online Document)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhary muda wako umekwisha, tafadhali naomba ukae.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (Makof)

### MWONGOZO WA SPIKA

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Haya mwongozo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 68(7). Awali ya yote nitakuwa na mambo mawili, kwanza ni Kanuni na lingine ni la utaratibu. Ahsante kwa ruhusa yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo kutoka kwa kauli aliyoitoa Mbunge wa CCM, Viti Maalum aki-refer hotuba ya Mchungaji Peter Msigwa, ametaja maneno mengi tu pamoja na hayo anasema ni mwongo wakati Kanuni inaruhusu kama alikuwa ni mwongo katika hotuba yake aliyoitoa alipaswa kutumia Kanuni kuonesha uongo wake. Kwa hiyo, kama Mchungaji Peter Msigwa alisema uongo basi athibitisho juu ya uongo aliousema. Hiyo ni ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, naomba kujua utaratibu, kuna watu tulioomba kuchangia asubuhi, tulileta vikaratasi vyetu na majina yetu hayajatajwa. Je, kwa kipindi cha kesho majina hayo yatapewa kipaumbele tunapoanza kuchangia hotuba kwa siku ya pili. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umeenda na tutatakiwa kumaliza kwa wakati. Mheshimiwa Selasini nimekuona na karatasi yako niliisoma.

Mwongozo uliokuwa umeombwa na Mheshimiwa Paresso wakati tukianza kipindi hiki cha mchana utatolewa kesho asubuhi.

Mwongozo uliombwa sasa hivi kuhusu Mheshimiwa Mwamwindi alivyoongelea mchango wa Mheshimiwa Msigwa, nadhani Mheshimiwa Mbunge ulikuwa unasiliza kwa makini maneno ambayo yamekuwa yaktumika hapa hata Mheshimiwa Peter Msingwa aliyatumia hayohayo. Hakutumia neno mwongo lakini aliyatumia hayohayo akiisema Serikali.

Kwa hiyo, hayo maneno niliyaacha tu kwa sababu hiyo. Kwa hiyo, mwongozo wangu kama unataka maelezo ni kwamba wakati ule Mheshimiwa Msigwa alipokuwa anasema yeye aliachwa kwa hekima hiyohiyo na huyo mwingine aachwe tu kwa hayo aliyyasema. (Makof)

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mawili, asubuhi Mheshimiwa Spika alitoa tangazo kuhusu wataalamu wa Mamlaka wa Vitambulisho vya Taifa kwamba wangekuwepo hapa Bungeni kutoa huduma ya kupiga picha kwajili ya Vitambulisho vya Uraia kwa Waheshimiwa Wabunge amba hawana hivyo vitambulisho kwa sababu wengine wanavyo.

Waheshimiwa Wabunge, wakati huu tunasikitika kuwataarifu wataalamu hawa wameshindwa kufika kutoa huduma hiyo kama ilivyokuwa imepangwa kutohala na sababu zilizo nje ya uwezo wao. Tutawafahamisha kuhusu utekelezaji wa zoezi hili pindi tutakapopata taarifa ya utayari wao wa kuja kufanya jambo hili. Tunachukua nafasi hii kuwaomba radhi kwa usumbufu amba unaweza kuwa umetokea.

## *Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Tangazo la pili, Mheshimiwa Spika asubuhi alizungumzia kuhusu mazishi ya Ndugu Mtenda na ndilo ambalo Mheshimiwa Selasini alikuwa akisimama hapa kuliulizia. Kesho kwenye kipindi kile cha asubuhi, tutatangaziwa muda gani wale wanaoweza kwenda kushiriki wataondoka hapa. Ratiba iliyopo inataka Waheshimiwa Wabunge wafike kule majira ya saa tano, kwa hiyo, tutatangaziwa hapa kesho saa tatu, saa tutakayoanza Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano,  
Tarehe 27 Januari, 2016 Saa Tatu Asubuhi)*